# USAWIRI WA MTUME MUHAMMADI KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA MAFUNZO YAKE KWA WAFUASI WAKE.

**NA**

**SILVERIA NJERI WATHE**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M. A ) KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**IDARA YA LUGHA NA ISIMU.**

**AGOSTI, 2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Silveria Njeri Wathe

Sahihi ……………………………….. Tarehe………………….

NAMBARI YA USAJILI C50/67034/2013

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. Mohamed Abdulaziz

Sahihi……………………………………… Tarehe…………………...

Prof. Kineene Wa Mutiso

Sahihi…………………………………….. Tarehe………………………

**TABARUKU**

Tasnifu hii nawataburukia mume wangu mpendwa Justus Wathe na wanangu Brian, Mitchelle na Janiffer.

# SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Maulana kwa kunipa afya njema na fursa nzuri ya kuendeleza masomo yangu vyema, kwani bila yeye singeikamilisha kazi hii. Nimeweza kufika mwisho wa kazi hii kwa sababu ya ushauri, msaada, wema na uadilifu wa watu wengi. Ningependa kuwashukuru baadhi yao.

Ningependa zaidi kuwatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu Profesa Mohamed Abdulaziz na Profesa Kineene Wa Mutiso, kwa kuniongoza tangu mwanzo mpaka mwisho wa tasnifu hii. Waliniongoza kupitia njia nyingi za kiusomi na za kipekee. Mwenyezi Mungu awabariki.

Aidha, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuniandaa kiakademia hadi kuweza kuzikabili kazi za kitaalamu. Dkt. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt Evans Mbuthia na Dkt. Prisca Jerono. Baraka nyingi ziwafikie popote mlipo.

Pia ningependa kutoa shukrani zangu kwa mume wangu Justus Wathe, ambaye anatambua umuhimu wa masomo katika jamii ya kisasa. Amejitolea mhanga kuhakikisha kuwa nimeendelea na kukamilisha masomo yangu. Amekuwa rafiki wa karibu kwa kunielewa na kunishauri, hasa, wakati mambo yalikuwa magumu kwangu.

Shukrani zangu ziwaendee wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kiusomi na ya kijamii. Kwa kweli wamekuwa marafiki wa dhati kwa kunipa moyo. Hawa ni Agnes Waithera, Faith Njoki, Adeline Kimeu, Caroline Musyoki, Jared Onchwati, Emily Mosota, Nkanga Mishack miongoni mwa wengine. Mwisho, namshukuru Dkt Mwangangi wa Musyoka kwa ushauri wake wa kila wakati, hasa wakati nilikumbwa na changamoto si haba wakati wa kuendeleza utafiti wangu.

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

TUKI.................Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Khj.....................Kama hapo juu

N. k……………..Na Kadhalika.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchanganua usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji* na Mafunzo yake kwa wafuasi wake. Mada hii ilichaguliwa kwa misingi kwamba Mtume Muhammadi ni jagina katika dini ya Kiislamu. Mtume huyu alienda safari ya ajabu usiku mmoja katika ulimwengu mwingine, na akawaletea wafuasi wake zawadi ya sala tano. Utafiti huu ulilenga kubainisha kuwa mtunzi wa *ukawafi wa miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina wa kidini. Nadharia ya uamilifu ilitumika kwa sababu ilionekana kufaa zaidi kuchanganua usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *ukawafi wa miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake, kwani ujagina ni mojawapo wa asasi ambazo huzuka katika jamii ili kuyatatua matatizo yanayoikumba jamii husika. Shida ambazo jamii hupitia huwa haziondoki hadi pale ambapo jagina ataibuka na kuziondoa. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchanganua usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika utenzi ulioteuliwa na kueleza mafunzo yake kwa wafuasi wake. Matokeo ya utafiti huu yalilingana na nadharia tete zilizoongoza mchakato mzima wa utafiti huu. Utafiti wetu umebainisha kwamba usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika utenzi huu unadhihirisha kwamba, yeye ni jagina katika dini ya Kiislamu. Aidha, tumebainisha kwamba safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) ina mafunzo mengi kwa wafuasi wake kama vile, miji mitakatifu, mitume katika dini ya Kiislamu, tofauti kati ya dini ya Kiislamu na dini zingine na uwezo wake Mwenyezi Mungu.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA ........ v

IKISIRI ........ vi

YALIYOMO ........ vii

**SURA YA KWANZA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 2

1.3 Malengo ya Utafiti Wetu ........ 3

1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii ........ 3

1.5 Upeo na Mipaka ya Kazi Hii ........ 3

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii ........ 4

1.7 Msingi wa Kinadharia ........ 9

1.8 Nadharia Tete ........ 11

1.9 Mbinu za Utafiti ........ 11

**SURA YA PILI ........ 12**

**USAWIRI WA MTUME MUHAMMADI KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* ........ 12**

2.1 Utangulizi ........ 12

2.2 Muhtasari wa *Ukawafi wa Miiraji* ........ 12

2.2.1 Fomula ya Mtunzi ........ 12

2.2.2 Kuitwa na Kutakaswa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W). ........ 13

2.2.3 Safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi ........ 13

2.2.4 Ndani ya Msikiti wa Beti Mukaddasi ........ 15
2.2.5 Safari ya Mbingu Saba ........ 15
2.2.6 Mtume Muhammadi (S. A.W) na Mwenyezi Mungu ........ 17
2.2.7 Safari ya kurudi Makka na kukataliwa kwa habari ya Mtume Muhammad (S. A. W).... 18
2.2.8 Mwisho wa *Ukawafi wa Miiraji* ........ 18
2.3 Mazingira ya Kihistoria Anamopatikana Mtume Muhammadi ........ 19
2.4 Dhana ya Usawiri na Mbinu za Usawiri wa Wahusika ........ 21
2.5 Usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) ........ 23
2.5.1 Mtume wa Mwisho wa Mwenyezi Mungu ........ 23
2.5.2 Mcha Mungu ........ 24
2.5.3 Mwenye Akili Pevu ........ 25
2.5.4 Hana Dhambi ........ 25
2.5.5 Aliitwa na Mwenyezi Mungu ........ 26
2.5.6 Kiongozi wa Dini ya Kiislamu ........ 26
2.5.7 Mtiifu na Msikivu ........ 26
2.5.8 Anaheshimiwa na Mitume na Manabii Wengine Wote ........ 28
2.5.9 Ni Mwombezi ........ 28
2.5.10 Anapendwa na Mwenyezi Mungu ........ 29
2.5.11 Mwenye Huruma ........ 30
2.5.12 Ni Mvumilivu ........ 31
2.5.13 Ana Uwezo wa Kipekee ........ 32
2.5.14 Alionyeshwa Pepo na Jehanamu ........ 33
2.5.15 Anapenda Kufahamu Mambo ........ 33
2.5.16 Alimwona Mwenyezi Mungu ........ 33
2.5.17 Alipewa Sala Tano na Mwenyezi Mungu ........ 34

2.5.18 Mwenye Heshima ..... 34
2.5.19 Ni Mwaminifu ..... 35
2.5.20 Ni Mkweli ..... 35
2.5.21 Alionyeshwa Wanayopitia Watenda Maovu na Watenda Mema ..... 35
2.5.22 Anazungumza na Malaika wa Mwenyezi Mungu. ..... 36
2.5.23 Ni Jagina ..... 36
2.6 Hitimisho ..... 37

**SURA YA TATU ..... 39**
**SIFA ZA UJAGINA NA MATUKIO YA UJAGINA KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* . 39**
3.1 Utangulizi ..... 39
3.2 Sifa za Ujagina ..... 39
3.2.1 Kabla ya Kuzuka kwa Jagina ..... 40
3.2.2 Ubashiri wa Kuzaliwa kwa Jagina ..... 42
3.2.3 Utoto na Ujana wa Jagina ..... 44
3.2.4 Jagina kwa Kawaida Huwa ni Mwanamume ..... 46
3.2.5 Jina la Jagina ..... 46
3.2.6 Jagina Hutoka Katika Ukoo wa Kifalme ..... 47
3.2.7 Majagina Huwa na Akili Pevu ..... 47
3.2.8 Maisha na Matendo ya Jagina ni ya Kimiujiza ..... 49
3.2.9 Safari ya Ajabu Ya Dunia Nyingine Na Kurudi Kwake ..... 51
3.2.10 Majagina na Suala la Ndoa ..... 52
3.2.11 Jagina Huhusishwa na Zaidi ya Jamii Moja ..... 53
3.2.12 Wapinzani wa Jagina ..... 54
3.2.13 Jagina Huwa Kipenzi cha Wanajamii ..... 56
3.2.14 Kugura kwa Jagina Kutoka Nyumbani Kwao ..... 57

3.2.15 Majagina Aghalabu Huwa Magwiji Katika Vita.......................................................... 58

3.2.16 Maisha ya Jagina Huwa ni Dhiki Tupu............................................................................ 60

3.2.17 Majagina Huwa Hawaeleweki kwa Urahisi.................................................................... 61

3.2.18 Majagina Aghalabu Huwa Hawarithiwi na Wana Wao.................................................. 61

3.2.19 Kifo cha Ajabu cha Jagina............................................................................................... 62

3.2.20 Anamoishi Jagina na Kurudi Kwake Safari ya Mwisho.................................................. 62

3.3 Matukio ya Ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*................................................................. 63

3.3.1 Safari ya Mtume Muhammadi............................................................................................ 63

3.3.2 Kutakaswa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W).................................................................. 64

3.3.3 Kulizima Jini...................................................................................................................... 65

3.3.4 Kuvumilia Kutazama Mateso ya Watenda Maovu............................................................ 65

3.3.5 Kuwanyamazia Myahudi na Mkristo................................................................................ 66

3.3.6 Kuwa Imamu katika Beti Mukaddasi................................................................................. 66

3.3.7 Uchaguzi wa Dini ya Kiislamu............................................................................................ 66

3.3.8 Kukutana na Mitume wa Awali.......................................................................................... 67

3.3.9 Kuyaona Maajabu ya Mbinguni......................................................................................... 67

3.3.10 Mazungumzo ya Mtume Muhammadi na Mwenyezi Mungu.......................................... 68

3.3.11 Kurudi Mara Kadha kwa Mwenyezi Mungu.................................................................... 69

3.3.12 Kutonyamaza Aiporudi Makka......................................................................................... 69

3.4 Hitimisho................................................................................................................................ 71

**SURA YA NNE........................................................................................................................ 72**

**MAFUNZO YA MTUME MUHAMMADI KWA WAFUASI WAKE................................. 72**

4.1 Utangulizi................................................................................................................................ 72

4.2 Safari ya Miiraji...................................................................................................................... 72

4.2.1 Utakatifu wa Mtume Muhammadi (S. A. W)...................................................................... 74

4.2.2 Kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) .......... 75
4.2.3 Nafasi ya Mtume Muhammadi .......... 75
4.2.4 Mitume katika Dini ya Kiislamu .......... 76
4.2.5 Adhabu za Watenda Dhambi .......... 76
4.2.6 Miji Mitakatifu .......... 77
4.2.7 Tofauti kati ya Dini ya Kiislamu na Dini Zingine .......... 78
4.2.8 Siku ya Kiama .......... 79
4.2.9 Ubinadamu wa Mtume Muhammadi (S. A. W) .......... 79
4.2.10 Nguzo za Dini ya Kiislamu .......... 80
4.2.11 Wapinzani wa Mtume Muhammadi (S. A. W) .......... 82
4.2.12 Uwezo Wake Mwenyezi Mungu .......... 82
4.2.13 Umuhimu wa *Kur'ani Tukufu* .......... 83
4.3 Hitimisho .......... 83

**SURA YA TANO .......... 84**

**TATHMINI NA MAPENDEKEZO .......... 84**

5.1 Utangulizi .......... 84
5.2 Malengo ya Utafiti .......... 84
5.3 Kuhusu Nadharia Tete .......... 85
5.4 Mapendekezo ya Utafiti Huu .......... 86

**MAREJELEO .......... 87**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Katika utafiti huu, tunanuia kuchunguza usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa Miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake. Utenzi huu ni wa kidini na umejikita katika dini ya Kiislamu. *Ukawafi wa Miiraji* umetungwa na Najmu'd Din al-Ghaitty. Mhariri na mtafsiri wa kazi hii ni Jan Knappert (1971). Mswada huu ulitokana na Profesa Kineene wa Mutiso ambaye ni mhadhiri katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi.

*Ukawafi wa Miiraji* unahusu safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) katika mbingu saba. Miiraji ni neno lenye maana ya kipandio au ngazi. Mtume Muhammadi (S. A. W) alienda safari hii katika usiku mmoja. Ilikuwa ni safari ya kimuujiza. Waislamu huamini kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alienda safari hii akiwa hayuko usingizini na hii haikuwa ndoto kama vile watu wengine hufikiri, kwa sababu kama ingekuwa ndoto makafiri wangesema ni uongo kwani si muujiza kwa mtu yeyote yule kuota akiwa ameenda safari ya mbali au kupanda mbinguni. Alibebwa na Buraki (mnyama mweupe, mrefu kuliko punda na mfupi kuliko nyumbu. Mnyama huyu akipanda mlima hunyoosha miguu yake ya nyuma na akiteremka mlima hunyoosha miguu yake ya mbele. Ana mbawa mbili na huonyesha ushupavu). Malaika Jibrili aliongoza safari hii.

Lengo kuu la safari hii ni kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W). Kwanza, kupitia kilele cha safari hii ambacho ni kumwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe, na vile Mtume alipokea kazi yake ya utume kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Pili, kupitia kutambuliwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) na mitume wengine wote wa awali. Jambo hili linadhihirika wakati Mtume Muhammadi (S. A. W) anawaongoza mitume wengine wote katika sala. Aidha, sala hutambuliwa na waumini wa dini ya Kiislamu kama njia mwafaka ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Watu ambao hawana dini huamini kuwa ni vigumu kwa mtu kupanda mbinguni. Watu ambao wana dini hawana budi kuamini kuwa Miiraji ni safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) katika mbingu saba, kwa sababu wanaweza kulinganisha safari hii na safari za mitume wengine kama vile Yesu Kristo aliye jagina wa Wakristo. Majagina wanapoenda katika safari huwaletea wanajamii zawadi. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaletea Waislamu sala. Sala ni mojawapo

ya nguzo muhimu katika dini ya Kiislamu. Sala hufuata utaratibu maalumu, mara tano kwa siku: asubuhi, mchana, alasiri, jioni na usiku.

Katika utafiti wetu tumeangazia jinsi ambavyo Mtunzi wa utenzi huu amefaulu katika kumsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina katika dini ya Kiislamu. Waumini wa dini mbalimbali humchukulia Mwenyezi Mungu kuwa jagina wa majagina. Waumini wa dini ya Kiislamu wanaamini kuwa matendo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) ni kulingana na mapenzi yake Mwenyezi Mungu. Humwona Mtume huyu kama kiumbe asiye wa kawaida na alizuka kwa manufaa ya wanajamii. Waislamu wanaamini kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) hata baada ya kifo chake huendelea kuishi na kutawala hali zao zote za maisha.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alizaliwa katika mazingira yenye maovu mengi kama vile ulevi, ukabila na tamaa za kimwili. Maadili na uadilifu ulikuwa umetoweka kabisa katika jamii ya wanadamu. Wafuasi wa dini ya Kiislamu wanaamini kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni Mtume wa mwisho ambaye alichaguliwa na Mwenyezi Mungu kuwaongoza walimwengu wote. Mwenyezi Mungu baada ya kumchagua alimteremshia *Kur'ani Tukufu* iliyojumuisha elimu takatifu, njia za kutekeleza uadilifu na mawaidha yenye faida kubwa sana. Mwenyezi Mungu alimwamuru Mtume Muhammadi (S. A. W) awaite watu kuelekea maisha ya ubinadamu, na kufuata haki kwa kukitumia kitabu Kitakatifu cha *Kur'ani.*

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Majagina wa dini mbalimbali ulimwenguni husawiriwa kwa njia tofauti tofauti kwa kutegemea misingi ya imani ya dini husika. Kwa mfano, Wakristo wanaamini kuwa Yesu Kristo ni mwana wa Mwenyezi Mungu aliye na uwezo wa kuwaokoa kutoka dhambini, ili mwishowe waingie Paradiso. Aidha, wanaamini kuwa ufufuko wa Yesu Kristo unaonyesha uhuru wa milele kwani alikuwa ameshinda kifo. Kulingana na Wakristo, Yesu Kristo aliwaletea zawadi ya wokovu baada ya safari yake ya ajabu katika ulimwengu mwingine. Nao waumini wa dini ya Kiislamu wanaamini kwamba Mtume Muhammadi (S. A. W) ni Mtume wa mwisho aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu kuwaongoza wanadamu wote kuelekea maisha ya ubinadamu. Licha ya hayo, wanaamini kuwa Mtume alisafiri hadi mbinguni na akawaletea zawadi ya sala kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kila Muislamu anaamini kuwa kwa kufuata mafundisho ya Mtume huyu, mwishowe ataingia Peponi. Kwa hivyo, umuhimu wa majagina wa kidini ni kuwaongoza wanajamii kuelekea maisha mazuri.

Katika utafiti huu, tumenuia kuchunguza jinsi mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina katika dini ya kiislamu, na kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake. Kwa maoni yetu, hakuna kazi nyingine ambayo imefanywa katika kushughulikia mada hii kwa kurejelea utenzi huu. Hilo ndilo pengo ambalo tunanuia kuliziba.

### 1.3 Malengo ya Utafiti Wetu

Malengo yetu katika utafiti huu ni:

i. Kuchunguza usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji*.
ii. Kuangalia sifa za ujagina kwa jumla, na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*.
iii. Kueleza na kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake katika *Ukawafi wa Miiraji*.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii

Katika utafiti wetu tumeamua kuchagua mada hii kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, baada ya kusoma somo la Swahili Poetry katika Chuo Kikuu cha Nairobi ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili, tulivutiwa na suala zima la majagina na jinsi majagina hao huwa na umuhimu wa kipekee katika jamii husika.

Pili, tumegundua kwamba kuna tenzi za kidini ambazo hazijashughulikiwa ipasavyo. *Ukawafi wa Miiraji* ni mojawapo ya tenzi ambazo hajizashughulikiwa kwa kiwango kikubwa. Kazi ambayo imefanyiwa utenzi huu ni kuhaririwa na kutafsiriwa.

Mambo haya yametutia hamu ya kuangalia usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake, ili nao watafiti wa baadaye wapate motisha watafiti mambo mengine yanayojitokeza katika utenzi huu. Ni matarajio yetu kuwa mchango wetu utakuwa wa manufaa kwa wahakiki katika fasihi kwa jumla.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Kazi Hii

Katika utafiti wetu tumejikita katika *Ukawafi wa Miiraji*. Tumechunguza usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika utenzi huu. Tumeangalia kwa kifupi dhana ya usawiri na mbinu ambazo mtunzi anaweza kuzitumia katika kuwasawiri wahusika katika kazi za fasihi. Hata ingawa utenzi huu una wahusika wengine hatujaangalia walivyosawiriwa kwani mada yetu

inahusu usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W). Tumezichanganua sifa za ujagina kwa jumla na matukio ya ujagina katika kazi hii. Sifa zote za ujagina hazijadhihirika katika utenzi huu, kwa sababu unahusu safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) katika mbingu saba na mazungumzo baina yake na Mwenyezi Mungu. Katika kuzichanganua sifa za ujagina, tumetoa mifano mingine ya majagina wa kidini. Ili kuweza kutoa mifano hiyo, tumerejelea *Kur'ani Tukufu*, *Biblia* na vitabu vingine vya kidini. Aidha, tumeeleza na kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake kama yanavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*.

Majagina huwa hawazuki katika ombwe tupu, bali huzuka katika mazingira, kipindi na hali fulani za kijamii. Kwa sababu hiyo, tumeyachanganua angalao kwa kifupi mazingira ya kihistoria ambamo jagina huyu anapatikana. Ni katika kuulewa muundo na hali halisi ya kijamii ndiposa tunaweza kuyaelewa na kuyafasiri matukio yote yanayomzunguka jagina.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii

Katika sehemu ya tatizo la utafiti tumeonyesha kuwa hakuna ushahidi tulioupata kuhusu utafiti wa usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa Miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake. Hata hivyo, wahakiki na watafiti wengi wameshughulikia suala la ujagina na usawiri wao katika kazi zingine. Baada ya utafiti wetu tumegundua kuwa suala la ujagina na usawiri wao limeshughulikiwa na watafiti na wataalamu kama vile Mutiso (1985 na 1999 ), Carlyle (1924 ), Gichamba ( 2005 ), Achieng ( 2012 ) miongoni mwa wengine. Aidha vitabu vya dini mbalimbali vimewasawiri majagina katika dini husika kwa njia ya kipekee.

Kazi ya Carlyle (1924) imetufaa katika utafiti wetu, kwani imetuwezesha kupata mwanzo na msingi mzuri kuhusu usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa Miiraji*. Aidha, katika sura ya pili tumechanganua sifa za ujagina na kazi hii imetufaa zaidi. Mtaalamu huyu katika kitabu chake amezichanganua sifa za majagina. Kwa mfano, Carlyle (1924:193) anasema:

> Jagina huwa na moyo mpole zaidi, mwenye huruma na upendo. Jagina ni mtu ambaye hutoa maisha yake bila kulazimishwa kutumikia watu kwa ukweli na hushirikisha ulimwengu mzima katika maono yake. (Tafsiri yetu).

Licha ya hayo, Carlyle (Khj) amelinganisha mashujaa kama vile Odin, Mtume Muhammadi (S. A. W), Napoleon, William Shakespeare, Samuel, John, Martin Luther, n.k. Katika sura yenye

mada *Hero as a prophet* amempa Mtume Muhammadi (S A.W) nafasi maalum. Ameonyesha wazi mvuto wake kwa Mtume huyu wa dini ya Kiislamu. Amemtambua kama ajenti wa mabadiliko huku akitilia mkazo uaminivu wa Mtume Muhammadi (S. A. W). Carlyle (khj) anamsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina mwenye uwezo mkubwa. Anashangaa vile mtu mmoja anaweza kuleta pamoja makabila yanayopigana na kuyafanya yenye uwezo mkubwa kwa muda unaopungua miongo miwili

Reglan (1936) ni mtaalamu mwingine ambaye ametufaidi mno kutokana na kazi yake. Reglan (khj), katika kazi yake kuna sura moja ambayo imetuvutia kwa kiwango cha juu. Mtaalamu huyu aliorodhesha sifa ishirini na mbili za majagina, anawataja majagina mbalimbali miongoni mwao wakiwa Moses, Oedipus, Elijah, Zeus na Joseph. Anawapatia alama kwa kuzingatia orodha yake ya sifa za majagina. Mwishowe anayeibuka na alama za juu zaidi ni Oedipus anayepata alama ishirini na moja juu ya ishirini na mbili. Sifa za ujagina kwa mujibu wa Reglan ni miongoni mwa sifa ambazo tumezichanganua katika kazi yetu.

Mutiso (1985 ) ametufaa sana katika utafiti wetu. Katika sura ya tatu, Mutiso amechanganua hurafa linganishi juu ya majagina. Katika tasnifu yake nzima mtaalamu huyu ameshughulikia *Kasida ya Hamziyya*, ili kuona vile mtunzi anavyosema kuhusu Mtume Muhammadi (S .A. W) na majagina wengine katika hurafa ya jamii mbalimbali, ili kuweza kueleza hurafa na uyakinifu katika kasida hiyo. Kazi hii yake imetuwezesha kupiga hatua kubwa katika kuainisha sifa za majagina na usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa vile mtunzi ameziorodhesha sifa za Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina wa kidini katika kazi yake, ametusaidia kuangalia matukio ya ujagina katika utenzi tunaoutumia katika kazi yetu. Pia, kazi yake imetuwezesha kuelezea na kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S .A. W) kwa wafuasi wake.

Hatuwezi kamwe kuyasahau makala ya Mutiso (1999). Katika makala haya, mtaalamu huyu amelinganisha maisha na sifa za mashujaa wawili wa kidini, Buddha na Muhammadi, huku akirejelea sifa bia za mashujaa. Makala ya Mutiso (khj) yamekuwa msingi bora wa utafiti wetu kwani tumejikita katika utenzi wa kidini. Kwa kuyatalii makala haya kwa kina tumepata mwelekeo unaofaa wa kuangalia jinsi Mtume Muhammadi amesawiriwa katika *Ukawafi wa Miiraji*. Aidha, makala haya yametusaidia kuangalia sifa za ujagina.

Kazi ya Mberia (1989) imetufaa kwa mapana na marefu katika utafiti wetu. Mberia alihakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kutathmini sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi. Baadhi ya sifa za ujagina ambazo tumezichanganua katika sura ya tatu tumezichota kutoka kwa kazi ya mtaalamu huyu.

Gichamba (2005) na Achieng (2012) wametufaa sana katika utafiti wetu. Watafiti hawa walifafanua sifa za mashujaa wa kijamii na kudhihirisha jinsi mashujaa hawa huwa na umuhimu mkubwa katika jamii zao. Kazi za watafiti hawa zimetusaidia kuangalia mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake kama yanavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Tumepata kuwa wamezichanganua sifa za ujagina katika kazi zao kwa njia nzuri sana. Hili limetusaidia kwa kiasi kikubwa, kwa sababu baada ya kupitia kazi zao tumepata kuelewa zaidi jinsi ya kuteua matukio ya ujagina katika kazi yetu.

Ndumbaro (2012) ameshughulikia dhana ya shujaa wa tendi kwa jumla, na matatizo mbalimbali ya kijamii katika maisha ya shujaa. Katika utafiti huu, mtafiti anahitimisha kuwa shujaa hupatwa na matatizo kama wanavyopatwa watu wengine katika jamii, ila nguvu alizo nazo shujaa zisizoweza kuelezeka humfanya shujaa kuwa na upekee katika ufumbuzi wa matatizo hayo. Utafiti huu umetufaa katika utafiti wetu kwa sababu umetutolea mwanga kuhusu jinsi majagina huyakabili matatizo wanayokumbana nayo. Pia kazi yake imetuwezesha kuchanganua baadhi ya sifa za ujagina katika kazi yetu na kuteua matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Gathara (2015) ameshughulikia taswira ya jagina katika tenzi huku akilinganisha Fumo Liyongo na Nabii Isa. Katika kazi yake amezichanganua sifa za ujagina na kuelezea umuhimu wa mashujaa kwa jamii zao. Aidha, katika sura ya pili amedhihirisha kuwa shujaa huwa hazuki katika ombwe tupu bali huzuka katika mazingira, kipindi na hali fulani za kijamii. Kazi yake imetufaidi katika utafiti wetu kwani tumepata uelewa wa jinsi Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa katika *Ukawafi wa Miiraji* na kuelezea mazingira ya kihistoria anamopatikana jagina huyu.

Mulokozi (1999) amezihariri na kuzitolea maelezo tenzi tatu za kale ambazo ni muhimu katika fasihi ya Kiswahili. *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Mwanakupona*. Utenzi unaotufaidi zaidi ni wa Fumo Liyongo. Mulokozi anatoa maelezo ya kina ya shujaa Liyongo na anamsawiri kama shujaa wa Kiafrika. Mwishowe mtaalamu huyu anatupa taswira kamili ya kifo cha Fumo Liyongo. Hii kazi imetufaa katika utafiti wetu, kwani

imetuwezesha kuyateua matukio ya ujagina yanayojitokeza katika safari ya kimuujiza ya Mtume Muhammadi (S. A. W), na jinsi ambavyo mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W).

Knappert (1967) alitafsiri baadhi ya beti za *Utenzi wa Tambuka* kwa lugha ya Kiingereza. Katika utenzi huu suala la ujagina limeangaziwa. Knappert (khj) ametuwezesha kupiga hatua katika kuyaangalia matukio ya ujagina katika kazi yetu. Naye Gatakaa (2012) alishughulikia uhakiki wa Maudhui mengi katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Miongoni mwa maudhui ambayo yaliangaziwa na Gatakaa ni ushujaa. Kazi hii imetusaidia kuchanganua sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji* na jinsi ya kumsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina katika dini ya Kiislamu.

Kazi nyingine ambayo imetusaidia katika utafiti wetu ni jinsi Mtume Muhammadi amesawiriwa katika *Kur'ani Tukufu*. Mtume Muhammadi (S. A. W), tangu utotoni mwake alikuwa mpole, mtulivu, mwenye huruma, mwenye haya na mwenye sifa zote zilizowapendeza watu na kuwavutia. Alikuwa mwaminifu sana mpaka akapewa jina la Al-Amin. Wakubwa na wadogo walimuheshimu. Mwenyezi Mungu anasema kuwa kuchaguliwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni kwa sababu ya upole wake ambao ameuweka katika moyo wa Mtume. Kwa sababu hiyo, amekuwa mpole kwa maswahaba wake japokuwa walikwenda kinyume na maelekezo yake, ambapo walisababisha vifo vya maswahaba wengi, lakini pamoja na yote hayo angelikuwa na moyo mgumu na kushirikiana nao kwa hasira, basi wangemkimbia wote (*Al-Imran* 159).

Were (1974) ameangazia matukio muhimu katika historia ya Afrika Kusini. Ameshughulikia masuala mengi lakini suala muhimu katika utafiti wetu ni kuinuka kwa ufalme wa Zulu (The Rise of Zulu Kingdom). Anamsawiri Shaka Zulu kama mfalme na shujaa wa Wazulu na kueleza hali halisi ya jamii ya Wazulu kabla ya kuzuka kwa shujaa huyu, na kueleza hali ilivyokuwa baada ya kifo chake. Kwa kumsawiri Shaka kama shujaa wa Wazulu kwa kuyarejelea matendo yake, tunapata uelewa zaidi wa jinsi ya kuangalia usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji*.Naye Kunene (1979) ameyasawiri maisha ya Shaka Zulu katika kazi yake. Ameonyesha utabiri wa kuzaliwa kwake, maisha yake ya ujana, aila yake, migogoro, ushujaa wake na kifo chake. Kazi yake imetupa uelewa mzuri juu ya ujagina na maisha ya jagina. Aidha, imetuongoza katika kuzichanganua sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*.

Owallah (2011) ni mtafiti mwingine ambaye ametuwezesha kupiga hatua katika utafiti wetu. Katika sura ya tatu mtafiti huyu amehakiki maudhui kadhaa lakini suala la ujagina limetufaa sana katika kazi yetu. Owallah (Khj) ameeleza suala hili kwa makini sana. Kwa kurejelea Mberia (1989) amezitaja sifa za ujagina ambazo ni baadhi ya zile tumezichanganua katika sura ya tatu ya kazi hii. Kazi yake imetufaa kwani imetuongoza katika kuangalia matukio ya ujagina katika kazi yetu.

Hata ingawa kazi ya Muniu (2013) haishughulikii tenzi, imetufaa kwa sababu katika faslu ya pili Muniu (Khj) amechanganua dhana ya ujagina kwa njia nzuri sana. Isitoshe, mtafiti huyu ameeleza sifa za ujagina katika sura hiyo hiyo nasi tukafaidi kwa kazi yake kwani tumechota baadhi ya sifa za ujagina kutoka kwa kazi yake.

Kazi nyingine ambayo imetufaa ni yaliyoandikwa katika *Biblia Takatifu* kuhusu jagina Emanuel ambaye ni jagina wa Wakristo. Ujagina wake ulidhihirika maishani mwake kutoka utabiri wa kuzaliwa kwake hadi kifo chake.Yaliyotufaa zaidi ni habari za kifo, ufufuko na kupaa kwake mbinguni ambazo zimeelezwa vizuri katika vitabu hivi*: Mathayo* sura ya 26, 27 na 28, *Marko* sura ya 14, 15 na 16, *Luka* sura ya 22, 23 na 24 na *Yohana* sura ya 19, 20 na 21. Yuda alimsaliti Emanuel, Wayahudi Waandishi na Mafarisayo wakamkamata na kumtesa hadi kufa. Baada ya siku tatu shujaa huyu wa Wakristo alifufuka. Kama tulivyosema katika sehemu ya tatizo letu la utafiti, wakristo wanaamini kuwa ufufuko wa Emanuel unaonyesha uhuru wa milele kwani alikuwa ameshinda kifo. Kwa kuyapitia matukio ya ujagina yanayodhihirika katika kifo na ufufuko wa Emanuel tunapata mwanga zaidi wa kuchanganua sifa za ujagina katika utafiti wetu. Aidha, tunapata mwelekeo mzuri wa kuyateua mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Mengine ambayo yametufaa katika *Biblia* ni yaliyoandikwa kuhusu safari za kwenda mbinguni za watu na mitume mbalimbali. Yesu Kristo alichukuliwa juu mbinguni mbele ya macho ya mitume na wingu likampokea na hawakumwona tena (*Matendo ya Mitume* 1:9). Aidha, Mungu alimpandisha Eliya mbinguni kwa upepo wa kisulisuli (*Wafalme wa kwanza* 2:1). Paulo anaelezea kuhusu mtu aliyenyakuliwa juu mpaka mbingu ya tatu. Mtu huyu aliyasikia mambo yasiyotamkika. Kuna mjadala kama mtu huyo alikuwa na mwili au la (*Wakorintho wa pili* 12: 2-4).

Isitoshe, katika *Ufunuo* 21: 10-14, 22-23 Yohana anasema kuwa alichukuliwa kiroho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akaonyeshwa ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu; wenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ukiwa mfano wa kito chenye thamani nyingi. Ulikuwa na ukuta mkubwa, mrefu wenye milango kumi na miwili na majina yameandikwa ambayo ni majina ya makabila kumi na mawili ya Waisraeli. Upande wa Mashariki, milango mitatu, na upande wa Kusini milango mitatu, na upande wa Magharibi mitatu. Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na katika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana kondoo. Anaendelea kueleza kuwa hakuona ndani ya Hekalu lile, kwa sababu ni Hekalu la Mwanakondoo na Mwenyezi Mungu. Anasema kuwa mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana Kondoo. Matukio haya yalitokea katika jamii husika na yalikuwa ni mafunzo kwa jamii hiyo. Kwa kuyapitia matukio haya tumefaulu katika kuangalia mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake, na kuyabainisha matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*.

Vutugwa (2015) ameshughulikia sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wake katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Utenzi huu na *Ukawafi wa Miiraji* ni tenzi ambazo zimejikita katika dini ya Kiislamu. Kwa sababu hiyo, kazi ya Vutugwa (khj) imetuwezesha kupiga hatua katika utafiti wetu. Kwa mfano, mtafiti huyu katika sura ya nne, amechunguza umuhimu wa sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Nasi tumefaidi, kwa kuwa utafiti wake umetuwezesha kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kama yanavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji.*

### 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya uamilifu. Nadharia hii inahusu ufafanuzi wa asasi mbalimbali ambazo huunda jamii. Aidha, nadharia ya uamilifu hueleza uamilifu wa asasi na kuonyesha mchango au umuhimu wa kila asasi katika kuelezea na kudumisha hali nyingi zinazopatikana katika mfumo mzima wa jamii.

Kulingana na McGee na Warms (2000: 158) nadharia ya uamilifu kwa jumla hugawanywa katika mitazamo miwili, kila mojawapo ikiwa inahusishwa na mtaalamu mahsusi. Mitazamo hii ni uamilifu wa kisaikolojia na uamilifu wa kimuundo. Uamilifu wa kisaikolojia unahusishwa na Bronislaw Malinowski (1884-1942). Kwa mujibu wa mtazamo huu, asasi za kitamaduni huamili

kutimiza mahitaji ya kisaikolojia na kimwili ya watu katika jamii. Nao mtazamo wa kimuundo unahusishwa na A.R Radcliffe- Brown (1881-1955). Wafuasi wa mtazamo huu walinuia kuelewa jinsi asasi za kitamaduni zilidumisha utangamano na kuleta usawa katika hali mbalimbali za jamii.

Katika kuelezea usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake kama yanavyodhirika katika utenzi huu, tumeongozwa na mtazamo wa uamilifu wa kisaikolojia unaohusishwa na Bronislaw Malinowski (khj). Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, kila jamii duniani huwa na mahitaji yake. Ili kuyatimiza mahitaji haya, kuna haja ya kuwepo kwa asasi za kitamaduni. Malinowski aliamini kuwa asasi za kitamaduni huibuka ili kuyatimiza mahitaji yaliyopo au yanayoibuka katika jamii.

Jamii ni mfumo ulio wazi na changamano ajabu. Kama mfumo mwingine wowote ulio wazi, jamii hukumbwa na matatizo na mahitaji fulani ya kimwili na ya kisaikolojia. Ili kusuluhisha matatizo au mahitaji haya, asasi mbalimbali za kitamaduni huibuka katika jamii. Kila mojawapo wa asasi hizi huibuka ili kutimiza mahitaji fulani mahsusi. Aidha, asasi hizi huwa haziko pweke bali hushirikiana na asasi nyingine ili kutimiza mahitaji ya jamii na hivyo kulenga katika kuifanya jamii kuwa kamilifu. Asasi hizi huibuka kadiri jamii inavyozidi kuendelea. Maendeleo katika jamii huashiria kuwepo kwa mahitaji mengi ambayo bila shaka huhitaji kushughulikiwa kwa dharura ili kuepusha dosari za aina zozote zile ambazo zinaweza zikauporomosha mfumo mzima wa jamii.

Malinowski (khj) alidokeza kuwa asasi za kitamaduni huzuka ili kutimiza mahitaji saba ya kimsingi ya binadamu ambayo ni: lishe, uzazi, faraja za kimwili, burudani, mwondoko, usalama na ukuaji. Katika kutoa msururu wa mahitaji haya, alikuwa na nia ya kuonyesha namna ambavyo mila na desturi mbalimbali zilichangia katika kuona kuwa jamii inaendelea kama inavyohitajika, huku ikitimiza mahitaji ya kimwili na kisaikolojia ya watu katika jamii.

Baadhi ya asasi za kitamaduni ambazo huamili kutimiza mahitaji ya mfumo mzima wa jamii ni pamoja na: uchumi, afya, utawala, elimu, dini, kilimo, sheria miongoni mwa asasi nyingine. Katika msururu huu huu, tunayo asasi ya ujagina ambayo huzuliwa na mahitaji fulani ya kijamii katika kipindi mahsusi katika historia ya jamii yake. Shida ambazo jamii hupitia huwa haziondoki hadi pale ambapo jagina ataibuka na kuziondoa.

Jambo muhimu katika mtazamo wa nadharia ya uamilifu wa kisaikolojia ni kule kutimizwa kwa mahitaji ya kisaikolojia na kimwili ya wanajamii. Asasi ya ujagina hushirikiana na asasi nyingine katika mfumo mzima wa jamii ili kuyatimiza mahitaji ya kijamii. Ni katika kutekeleza mahitaji haya umuhimu wa jagina katika jamii hujitokeza. Aidha, katika usawiri wa Mtume Muhammadi katika *Ukawafi wa Miiraji* tumejikita katika dini ya Kiislamu. Dini ni mojawapo ya asasi ambazo hulenga kutimiza mahitaji ya wanajamii.

### 1.8 Nadharia Tete

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amefaulu katika kumsawiri Mtume Muhammadi kama jagina wa dini ya Kiislamu.
ii. Kuna sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji.*
iii. Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza wafuasi wake masuala muhimu katika *Ukawafi wa Miiraji.*

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti wetu umejikita katika maktaba. Maktabani tumeyapitia mambo yanayohusiana na nadharia ya uamilifu. Nadharia ya uamilifu ndicho kifaa chetu muhimu cha kuchanganua *Ukawafi wa Miiraji.* Usomaji wa kina wa utenzi tunaoushughulikia umefanywa ili kubainisha jinsi mtunzi amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) na kuweza kuelezea mafunzo yake kwa wafuasi wake kama yanavyodhihirika katika utenzi huu. Aidha, tumerejelea tovuti mbalimbali kwenye mtandao ili kuelewa zaidi mambo yanayohusiana na nadharia ya uamilifu. Isitoshe, kwa sababu *Ukawafi wa Miiraji* umeandikwa katika mtazamo wa dini ya Kiislamu, tumevisoma vitabu vilivyotusaidia kuelewa zaidi utenzi huu.

Utenzi wa *Ukawafi wa Miiraji* umesomwa ili kupata data. Tumebainisha jinsi Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa katika utenzi huu. Tumezingatia matukio katika kazi hii ili kuweza kupata taswira za Mtume Muhammadi (S. A. W) ambazo tumezitumia katika utafiti huu. Data yetu imechanganuliwa kwa kutumia nadharia ya uamilifu. Mafunzo yake yanadhirisha umuhimu wake, na yametusaidia kuchora picha halisi ya jagina huyu wa Waislamu. Data ya maktabani imetumiwa kushadidia yale yaliyojitokeza kwenye utenzi wetu. Data imewasilishwa kwa kutumia njia ya maelezo na maandishi.

# SURA YA PILI

# USAWIRI WA MTUME MUHAMMADI KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI*

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia muhtasari wa *Ukawafi wa Miiraji*. Pia tumeangalia mazingira ya kihistoria anamopatikana Mtume Muhammadi (S. A. W). Baadaye tumechanganua usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji*.

Kimani na Chimera (2008) wamedai kuwa ushairi ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kuu kwa njia ya mkato na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Kutokana na kauli hii ya Kimani na Chimera (khj) tumeonelea ni vizuri kwanza kushughulikia muhtasari wa utenzi wetu ili tuweze kuueleza bila kutumia lugha ya mkato. Majagina hawazuki katika ombwe tupu, kwa sababu hiyo tumeamua kuangalia kwa kifupi tu mazingira ya kihistoria anamopatikana Mtume Muhammadi (S. A. W). Sehemu ya mada yetu inahusu usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa hivyo, tumeangalia dhana ya usawiri na mbinu ambazo mtunzi anaweza kuzitumia kumsawiri mhusika yeyote yule katika kazi ya kifasihi. Matendo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) yanaongozwa na Mwenyezi Mungu, kwani yeye ndiye alimchagua kama Mtume wa mwisho ili awaongoze wanadamu wote kuelekea njia ya ubinadamu. Isitoshe, matendo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) yanadhihirisha wazi kuwa yeye ni jagina wa dini ya Kiislamu.

## 2.2 Muhtasari wa *Ukawafi wa Miiraji*

### 2.2.1 Fomula ya Mtunzi

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* ametanguliza utenzi huu kwa fomula ambayo watunzi wa tenzi za kidini hutumia. Anaanza kwa kulitaja jina la Mwenyezi Mungu na kisha kumrudikia sifa si haba (ubeti 1). Kisha analitaja jina la Mtume Muhammadi (S. A. W), familia yake na maswahaba wake na kuwasihi Waislamu wawaombee kama wanatamani kuingia Peponi kama hao, ili nao Siku ya Kiama wasimame wawaombee wapate kuingia Peponi (ubeti 2). Mtunzi anasema kuwa hataki kuwa na utangulizi mrefu kwa sababu ana mambo muhimu anayotaka kuyaeleza, kwa njia ya ushairi juu ya usiku wa Miiraji, ambapo Mtume Muhammadi (S. A. W) alipandishwa hadi mbinguni (ubeti 3).

### 2.2.2 Kuitwa na Kutakaswa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W).

Wakati ulipofika wa kudhihirisha kazi ya Mtume Muhammadi (S. A. W), Mwenyezi Mungu alimtuma malaika Jibrili amwendee ampeleke kwake. Jibrili alimkuta Mtume Muhammadi (S. A. W) usingizini. Alimwamsha mara moja na kumwambia kuwa Mwenyezi Mungu alimwita haraka. Alipoamka, malaika huyu alimpasua kifua chake na kutoa maovu yote yaliyokuwa ndani yake. Kisha akamshona kama kwamba hakumpasua. Halafu akamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa alikuwa ametumwa amwite aende naye alipo Mwenyezi Mungu.

Alimwambia ampande Buraki haraka lakini mnyama huyu alisita kumbeba Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa kuwa alihofia mkono wake ulikuwa umeshika masanamu. Malaika Jibrili alimwambia Buraki asikatae kumbeba Mtume Muhammadi (S. A. W), kwa sababu ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Alikubali kumbeba na akamwomba Mtume Muhammadi (S. A. W) amuweke mahali pazuri Peponi. Buraki alifurahi alipoahidiwa mahali pema Peponi. Alinyenyekea na Mtume akampanda huku akimwomba Mwenyezi Mungu.

### 2.2.3 Safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi

Katika safari hii, Mtume aliomba mara tatu kwa ushauri wa Malaika Jibrili. Mara ya kwanza Jibrili alimwambia aombe walipofika Madina, kwa sababu mahali hapo ndipo pangekuwa na kaburi lake baadaye, kwa hivyo patakuwa mahali patakatifu. Mara ya pili, aliambiwa aombe walipofika mlima wa Sinai, kwa sababu ni mahali ambapo Mwenyezi Mungu alijidhihirisha kwa mtume Musa. Mara ya tatu, akamwambia aombe walipofika Betilahamu, alipozaliwa mtume Isa kwa sababu ni mahali pema. Kutoka hapo, walikutana na jini likiwa na kijinga cha moto huku likimmulika Mtume Muhammadi (S. A.W). Malaika Jibrili akamwambia Mtume akariri aya fulani kutoka kwa *Kur'ani Tukufu*. Mtume Muhammadi (S. A. W) alifuata ushauri wa malaika Jibrili na jini likazima mara moja.

Waliendelea na safari na wakaona mambo mengi. Mambo aliyoonyeshwa Mtume Muhammadi (S. A. W) yanajitokeza kutoka ubeti wa14 hadi 35. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na: Watu ambao walikuwa wakipanda na kuvuna baada ya muda mfupi baadaye. Malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa ni wale watu ambao walikufa katika vita vitakatifu. Kulingana na dini ya Kiislamu roho za watu hawa huingia Peponi mara moja bila kungojea Siku ya Kiama katika makaburi yao.

Kisha wakaenda wakanukia harufu nzuri na Jibrili akamwambia kuwa ni harufu ya mwanamke mwema, alipokuwa akichana nywele za binti ya Firauni ambaye hakuwa amesilimu kichana kilianguka. Bintiye Firauni alilaani Mwenyezi Mungu, naye mwanamke yule akamwuliza kwa nini alifanya hivyo na akamwambia kama ana Mungu mwingine aseme. Isitoshe, alisema Mungu wake ni muumba wa nchi na mbingu. Firauni aliposikia habari hizo, alimchukua mwanamke mwema pamoja na watoto wake na kuwatia katika mafuta yachemkayo na hiyo ilikuwa harufu nzuri ya watu wema. Aidha, waliwaona watu wabaya wakipondaponda vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Akaelezwa kuwa wale walikuwa wazembe wa kusali sala za asubuhi. Pia, sala zao hazikuwa zinakamilika. Waliendelea na safari na wakaona watu ambao walikuwa wamevalia nguo zenye viraka wakila sumu. Malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) ni wale ambao hawatoi zakat na mali yao ni ya Jehanamu.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa wazinifu. Mbele yao kulikuwa na nyama nzuri iliyonona vizuri na pembeni mwao kulikuwa na nyama duni iliyooza yenye uvundo. Wakawa wanakula ile nyama duni iliyooza yenye uvundo na wanaiacha ile nzuri iliyonona. Kisha akaonyeshwa mti ukiwa njiani ambao ulikuwa unararua nguo za wapita njia. Akaelezwa kwamba wale ni watu ambao hukaa vingojini na kuzuia wengine kumwabudu Allah na mahali pao ni Jehanamu. Licha ya hayo, waliuona mto wa damu, ambao ulikuwa na watu ndani wakila sumu. Hawa ni wale walikula chakula ambacho kimekatazwa.

Alionyeshwa watu wakikatwa ndimi zao kwa makasi huku zikirejea tena. Malaika Jibrili akamwambia Mtume kuwa ni waongo na hawamtii Mwenyezi Mungu. Aidha, alionyeshwa watu wabaya wakiparura nyuso zao kwa kucha za shaba. Akaelezwa kwamba hao ni wale wasiotenda haki na siku ya ufufuko nyuso zao hazitakuwa na nyama. Kutoka hapo, waliona shimo ndogo, ng'ombe akatokea hapo na alipokuwa akitaka kurudi hangeweza. Akaelezwa kwamba hao ni wale wazungumzao maneno bila kufikiria na baadaye wanajutia maneno hayo, kwa sababu yanaleta madhara. Kisha wakaona uwanja mkubwa tambarare halafu wakasikia sauti nzuri zenye harufu nzuri. Malaika Jibrili akamwambia Mtume asikilize sauti za Peponi ambazo humzungumzia Mwenyezi Mungu. Halafu akasikiliza sauti mbaya za watu ambao walikuwa Jehanamu kwa kutotii Mwenyezi Mungu.

### 2.2.4 Ndani ya Msikiti wa Beti Mukaddasi

Walipofika kwenye msikiti wenye baraka waliona mwangaza ukitokea pande mbili, upande wa upembe wa Daudi na upande wa kaburi la Mariamu. Waliingia ndani na kuanza kusali kwa unyenyekevu. Baadaye, waliwaona mitume wengine wakiingia ndani ya msikiti, naye malaika Jibrili akasimama mbele yao na kuadhini, lakini hawakujua imamu angekuwa nani. Jibrili akamchagua Mtume Muhammadi awe imamu wa mitume wengine wote, huku akimwambia kuwa yeye ana uwezo mkubwa na mitume wengine wako nyuma yake. Walipomaliza kusali waliyataja majina ya Mwenyezi Mungu na kuzitaja sifa zake zisizo na idadi. Mtume Muhammadi (S. A.W) alihisi kiu na akaletewa vikombe viwili, kimoja kikiwa kimejazwa maziwa na kingine kimejazwa mvinyo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alichagua kikombe kilichojazwa maziwa. Maziwa yalikuwa ishara ya dini ya Kiislamu na mvinyo ishara ya maovu.

### 2.2.5 Safari ya Mbingu Saba

Ngazi iliyokuwa imepambwa kwa fedha na dhahabu ilishuka kutoka mbinguni na Mtume Muhammadi (S. A. W) akapandishwa katika uwingu wa dunia akifuatana na malaika Jibrili, aliyekuwa akibisha hodi kwa niaba yake. Akafunguliwa katika mbingu ya kwanza na akamwona Adamu, baba wa watu wote. Alionyeshwa roho za watu wema wakiwa upande wake wa kuume na roho za watu waovu zikiwa upande wake wa kushoto. Adamu alimsalimu, akamkaribisha na akamjibu salamu yake na akaukubali utume wake. Baada ya hapo, akapandishwa hadi mbingu ya pili. Jibrili akaomba kuingia na wakaitikiwa kama awali. Waliwaona Isa na Yahya, ambao walifanana kama wazaliwa na mama mmoja. Alipowasalimia walisimama, wakampa heshima na kumwita kwa jina lake, ishara ya kuwa waliitikia utume wake.

Kutoka hapo, Mtume akapandishwa mpaka mbingu ya tatu, walibisha kwa taadhima na wakaitikiwa kwa heshima ambako walimwona Yusuf mwenye sura njema, akamsalimia naye akamjibu salamu yake, akamkaribisha na akaukubali utume wake. Kisha akapandishwa katika mbingu ya nne alipomkuta Idiris ambaye alimkaribisha Mtume Muhammad (S. A. W) na kumwambia awe na amani na apumzike kiasi. Aidha, Idiris alimwambia kuwa alikuwa Mtume mwenye baraka isiyo na kikomo.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alipandishwa hadi mbingu ya tano. Hapo walikutana na nabii Haruni ambaye aliwakaribisha kwa heshima. Walimwomba Mwenyezi Mungu na wakaagana kwa dua njema. Walipoingia katika mbingu ya sita walikutana na Musa ambaye alizungumza na Mwenyezi Mungu hapo awali na wakaliona jeshi lake likiwa ange. Mtume aliambiwa ainue kichwa chake alitazame jeshi lile na hakuuona mwisho wake. Aliambiwa kuwa jeshi alilokuwa akilitazama lilikuwa lake. Musa alikuwa na umbo zuri na nywele zikiwa zimesimama wima kichwani. Mtume Muhammadi (S. A. W) akamsalimia naye akaitikia salamu zake. Musa aliukubali utume wake kwa kumwambia kuwa umati wake ulikuwa bora kuliko umati mwingine wowote. Pia, alimwambia akipewa ukarimu wake mola awakumbuke ili Mungu awaridhie wawe watumishi wake. Mwishowe, walifika katika mbingu ya saba, wakakaribishwa kwa heshima, wakafunguliwa na wakaingia ndani. Mtume Muhammadi (S. A. W) alimwona mtu mwenye hadhi kubwa na akasaili ajue alikuwa nani, naye malaika Jibrili akamwambia kuwa ni rafikiye Mwenyezi Mungu Iburahimu. Mtume alimsalimia naye akajibu salamu zake na akamwambia aende ahubirie umati wake ili uweze kuingia Peponi.

Wakiwa hapo, wakawaona watu wengi weupe kama karatasi na wengine wenye madoadoa . Malaika Jibrili akamwambia watu weupe kama karatasi walikuwa roho za watenda wema, ambao waliingia Peponi bila kupata adhabu yoyote na wenye madoadoa ni watenda dhambi lakini wakatubu wakawa wema.Walipita na wakaona nyumba iliyokuwa imejengwa chini ya Pepo. Waliingia ndani na kusali. Waliwaona malaika 700,000 na idadi hii iliingia katika nyumba hii kila siku. Mwadhini wao ni malaika Jibrili na imamu ni malaika Mikaili. Mwishowe, walipita wakielekea kwenye kiti cha enzi, hatua ya nane ya daraja la utume mahali palipo na mti wa ajabu ambao ni mwisho wa vitu vyote. Waliona maajabu mengi yasiyo na mwisho. Chini ya mti huo waliiona mito minne iliyojaa maziwa, asali na divai. Matunda ya mti huo ni matamu sana. Aidha, matawi yake hufunika mataifa yote. Kisha Mtume Muhammadi (S. A. W) akauona mto wake mwenyewe, zawadi kutoka kwa Mungu uitwao Kauthari. Waliufuata mpaka wakafika katika nyumba njema ambako waliona viumbe wengi ambao hawajawahi kuwaona au kusikia hadithi kuwahusu. Mtume aliona Pepo na hakuwa ameuona mfano wake. Ilikuwa imepambwa vizuri sana. Kisha, wakatoka nje na kuuona moto mkali. Aliona adhabu kali iliyokuwa ikipatiwa wenye dhambi na hakukubaliwa kuwaokoa. Kwa kutokuvumilia alizirai na kupoteza fahamu. Malaika Jibrili alimkumbatia na akapata fahamu tena.

### 2.2.6 Mtume Muhammadi (S. A.W) na Mwenyezi Mungu

Walipofika daraja la nane, malaika Jibrili hakuruhusiwa kupita hapo kwani huo ndio ulikuwa mwisho wake. Mtume alinyanyuliwa kwa rafurafu, akapita vikwazo vyote na mwishowe akamwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Mtume Muhammadi (S. A.W) alimsalimu Mwenyezi Mungu kwa taadhima kubwa naye akamjibu salamu zake na kumwambia kuwa yeye ni mteule ambaye amewekwa mahali pema. Mtume Muhammadi (S. A. W) alipomwona Mungu wake macho kwa macho alishindwa kunena tena na akapiga magoti, lakini Mungu akamwambia aombe alichotaka na angepewa kikiwa kamili. Mtume Muhammadi (S. A. W) alimwambia mwenyezi Mungu kuwa Ibrahimu ni rafiki yake, na akasaili apate kujua nafasi yake. Aidha, aliendelea kumwambia Mwenyezi Mungu kuwa alimpatia Daudi zaburi, na Sulaimani uwezo wa kumiliki jini.

Isitoshe, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliongezea kuwa Isa alipewa uwezo wa kuponya vilema na kuwafufua wafu. Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume Muhammadi kuwa, yeye ni rafiki yake zaidi ya mitume wengine wote, na akamwambia kuwa jina lake likitajwa na la Mtume Muhammadi (S. A. W) litatajwa pia. Aidha, alimwambia kuwa umati wake ni bora kuliko umati mwingine wowote. Licha ya hayo, Mwenyezi Mungu alimwambia kuwa Siku ya Kiama atakuwa mwombezi wa wafuasi wake (wema na wabaya), ili waingie Peponi. Mwishowe, alimwambia kuwa Siku ya Kiama atawaona makafiri ambao hawakufuata ujumbe wa mitume wakiingia Jehanamu.

Mwenyezi Mungu alimpa Mtume sala hamsini awapelekee wafuasi wake na alipotoka mahali hapo, alimkuta malaika Jibrili alipomwacha na wakaandamana hadi alipokuwa Musa. Mtume Muhammadi (S. A. W) alimwelezea Musa yote yaliyojiri mbele ya Mwenyezi Mungu. Musa alimwambia kuwa watu wake hawangeweza kusali sala hamsini kila siku. Alimshauri arejee tena kwa Mwenyezi Mungu ili apunguziwe sala hizo. Mtume alirudi kwa Mwenyezi Mungu na akamwomba ampunguzie sala hizo, naye Mungu akazipunguza kwa tano, zikawa arubaini na tano. Alipofika alipokuwa Musa alimwambia arudi tena kwa Mwenyezi Mungu aombe zipunguzwe tena. Mtume Muhammadi (S. A. W) alifanya hivyo mara kadha hadi Mwenyezi Mungu akazipunguza zikawa tano. Mtume Muhammadi (S. A. W) alijaribu kumsihi Mwenyezi Mungu azipunguze sala hizo tena, lakini Mwenyezi Mungu hakuzipunguza sala hizo chini ya tano.

### 2.2.7 Safari ya kurudi Makka na kukataliwa kwa habari ya Mtume Muhammad (S. A. W)

Walishuka kutoka mbinguni usiku huo huo na wakawasili Beti Mukaddasi. Walimwona Buraki mahali walikuwa wamemwacha na Mtume akampanda. Safari ya kurudi Makka ikaanza. Walipokuwa safarini hii, waliuona msafara wa kibiashara wa ngamia wengi pamoja na watu wa Makka. Wanyama hawa walipomwona Buraki walitoroka na mmoja wao akavunjika mguu. Isitoshe, waliuona msafara mwingine na mara hii Mtume Muhammadi (S. A. W) akawasalimia nao wakaitambua sauti yake. Walifika Makka wakati wa usiku.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na hofu kuwa Makureshi hawangeamini habari kuhusu safari yake ya mbinguni. Abu Jahali alimwona akiwa katika hali hiyo na akamdadisi kwa dhihaka ili ajue hali hiyo. Mtume Muhammad (S. A.W) alimwambia ya kwamba usiku huo alienda safari ya mbinguni na akamwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe na alikuwa amempa mambo ya kuhifadhiwa moyoni mwake. Abu Jahali alikusanya Makureshi wote wasikilize habari hizo. Walizipinga na hawakutaka kuziamini. Katika kutafuta ukweli wa maelezo ya Mtume Muhammad (S. A. W) walimtaka awaelezee sifa za msikiti wa Beti Mukaddasi, kwa sababu walikuwa wanazijua. Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, malaika Jibrili akamdhihirishia sifa za msikiti huo machoni pake. Akawa anawaelezea sifa zake moja baada ya nyingine na wakashindwa na kupinga kwa vile ulikuwa ukweli mtupu. Mwishowe, aliwaelezea kuhusu ule msafara wa kibiashara aliokuwa amekutana nao. Aidha, aliwaambia wakati ambapo msafara huo ulitarajiwa kuwasili. Hata baada ya habari hiyo walizidi kuzikataa habari zake. Siku ilipofika, ulitimia wakati wa jioni na wafanyabiashara hawakuwa wamewasili. Mtume alimwomba Mwenyezi Mungu alisimamishe jua ili ahadi yake itimie. Jua lilisimama hadi msafara huo ulipowasili. Hayo hayakuwafanya wamwamini Mtume Muhammadi (S. A.W), waliendelea kuabudu masanamu yao.

### 2.2.8 Mwisho wa *Ukawafi wa Miiraji*

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemalizia kazi yake kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumwombea Mtume Muhammadi (S. A. W) na familia yake bila kuwasahau maswahaba wake. Anapiga dua kwa Mwenyezi Mungu ili amrehemu Siku ya Kiama pamoja na wote watakaosoma au kusikiliza utenzi huu. Mwishowe, analitaja jina lake na anatarajia zawadi kutoka kwa Mtume Muhammadi (S. A. W), ili awe mmoja wa wale watakaoingia Peponi.

## 2.3 Mazingira ya Kihistoria Anamopatikana Mtume Muhammadi

Mtume Muhammadi (S. A. W) alizaliwa katika mji mtakatifu unaoitwa Makka, mwaka wa 570 A. D. Alizaliwa katika familia ya Kiarabu, yenye heshima kubwa sana na iliyokuwa maarufu sana kila sehemu. Baba yake ni Abdullah, ambaye alifariki dunia kabla ya kuzaliwa kwake. Alinyonyeshwa na mwanamke maskini aliyeitwa Halima, na alirudishwa kwa mama yake akiwa na umri wa miaka minne. Pia, alimpoteza mama yake mzazi alipofikisha umri wa miaka sita. Akiwa na umri wa miaka minane babu yake (Abdul Mutwalib), aliyekuwa msimamizi wake naye pia aliaga dunia. Baadaye, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwekwa chini ya usimamizi na ulinzi wa baba yake mdogo Abu Twalib aliyempenda sana.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alizuka katika mazingira ambayo maadili na uadilifu ulikuwa umetoweka kabisa katika jamii ya wanadamu. Mwenye nguvu ndiye aliyekuwa akitamba na kuonekana dunia imeumbwa kwa ajili yake peke yake na wengine hawana haki katika dunia hii. Ubabe ulitawala kila sehemu. Dini ya Nabii Ibrahimu ilikuwa imebadilishwa na kuwa ya kuiabudu miungu mbalimbali. Waarabu walikuwa wakiishi katika maisha ya kikabila na hata baadhi ya miji yao kama vile Yemen na sehemu nyinginezo zilikuwa zikitawaliwa kwa misingi ya kikabila. Waarabu walikuwa wakiishi katika unyonge na hali za kubaki nyuma kimaisha.

Kulingana na Safeyy (2002:52-54) badala ya Waarabu kujishughulisha na utamaduni na ustaarabu, walijishughulisha na maovu kama vile ulevi na tamaa za kimwili. Zaidi ya hayo, baadhi yao walikuwa wakizika watoto wao wa kike wakiwa hai, maana walikuwa na itikadi za ajabu. Waliamini kuwa mtoto wa kike ni mkosi, hivyo akizaliwa walikuwa hawaoni shida wakimzika, akiwa hai. Safeyy (khj) anaongeza kwa kusema kuwa Waarabu hawa wakosa dini wakati mwingine, waliwaua watoto wa kike na wa kiume kwa kuogopa umaskini na ufukara lakini mauaji ya watoto wa kiume yalikuwa ni nadra, kwa sababu walihitajika kukinga jamii wakati wa mashambulizi ya maadui. Wengi wa Waarabu hao walikuwa wakiishi kwa njia za wizi, uharamia, uuaji na uporaji wa mali na mifugo ya wenzao. Unyama na umwagaji damu ni mambo yaliyokuwa yakichukuliwa kuwa ya heshima na ya kumletea mtu sifa kubwa. Walikuwa wakishindana kufanya uovu, ili mtu akishinda na kuonekana ni bingwa wa uovu apewe heshima kubwa na sifa ya hali ya juu.

Katika mazingira kama hayo; Mwenyezi Mungu mwenye rehema na mapenzi ya hali ya juu kwa watu wake, alimchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) ili kuwabadilisha na kuwaongoza walimwengu wote. Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, Mwenyezi Mungu alimwaru Mtume Muhammadi (S. A. W) awaite watu na kuwaelekeza katika maisha ya ubinadamu yenye kushikamana na haki kwa kukitumia kitabu cha *Kurani Tukufu.*

## 2.4 Dhana ya Usawiri na Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Usawiri wa mhusika ni kitendo cha kumchora, kumfafanua, kumtambulisha na kumjenga mhusika huku akipewa maneno, matendo, hadhi na uwezo unaolandana na kuwiana. Usawiri mzuri wa mhusika unawafanya wasomaji wajitambulishe naye kwa kuhisi anavyowaza.

Kuna mbinu kadhaa zinazoweza kutumiwa na mtunzi kumsawiri mhusika na ndizo msingi wa uhusika wa kazi ya kifasihi. Kulingana na Wamitila (2002) msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuteua namna ya kuwasilisha wahusika wenyewe. Kama wasomaji na wahakiki wa fasihi, tunategemea sifa kadha kuwaelewa wahusika kama vile mienendo na tabia zao, maumbile yao, lugha zao, vionja vyao, kiwango chao cha elimu, jamii yao na kadhalika. Baadhi ya mbinu zinazotumika ni mbinu ya kimaelezi, kimajazi, ulinganuzi, kidrama, kuwatumia wahusika kuwasawiri wengine, kistiari na nyinginezo.

Mwandishi hutumia mbinu ya kimaelezi kuzieleza sifa za mhusika na mara nyingine hutoa picha ya maneno inayomwelezea mhusika anayehusika. Mwandishi anakuwa na nafasi ya kubainisha mapenzi yake dhidi ya wahusika fulani. Mbinu hii haimpi msomaji nafasi ya kushiriki katika kutathmini tabia ya mhusika fulani. Analazimika kuukubali msimamo na kuridhika na maelezo ya mwandishi. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* ametumia mbinu hii. Katika utangulizi wake analitaja jina la Mtume Muhammadi (S. A. W) pamoja na familia yake, anatilia mkazo umuhimu wa kuwaombea ili nao Siku ya Kiama wasimame wawaombee waokoke waingie Peponi. Anaeleza:

> Siku ya kiyama wasimame watuombee
> Tupate wokovu siku nzito ya Jahannama (ubeti 2).

Maelezo haya ya mwandishi yanajitokeza katika sehemu ya mwanzo ya kazi yake na yanatuelekeza kuamini kuwa ana mtazamo fulani chanya kumhusu mhusika na ambao huenda ukatuelekeza kwenye njia fulani ya kumtazama mhusika huyo.

Mbinu nyingine ni ya majazi au matumizi ya majina ya watu au mahali yanayosadifu tabia na maana fulani. Mbinu hii imetumika tangu zamani katika fasihi mbalimbali, hasa kwa kuwa majina katika jamii nyingi huwa na maana. Hii inaweza kuelezwa kama njia sahihi na nyepesi sana ya uhusika. Waandishi wa kazi za kifasihi huweza kuyatumia majina ya wahusika ambayo huakisi mandhari yao, wasifu wao, tabia zao, itikadi zao, vionja vyao na kadhalika.

Uchunguzi wa majina ya wahusika lazima uhusishwe na msuko, mbinu za utunzi, ucheshi, dhamira au maudhui, itikadi au motifu katika kazi inayohuska. Mbinu ya majazi imetumika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Mtume Muhammadi (S. A. W) ambaye jina lake lina maana ya "anayesifiwa" amepewa majina mengine katika utenzi huu. Kwa mfano, Mwenye Jaha (ubeti 3), Kipendo kyema (ubeti 7), Muteule (ubeti 39), Rasuli (ubeti 45), Mwana mwema (ubeti 45) na Muombezi (ubeti 49).

Mbinu ya ulinganuzi ni njia moja ya jadi ambayo hutumiwa kati ya vitu viwili na kuviweka vitu hivyo katika muktadha sawa. Kwa njia hii ikiwa pana tofauti kati ya vitu hivyo itajitokeza kwa njia iliyo bayana zaidi. Kazi nyingi zilizoandikwa kwenye misingi ya kimaadili au zenye mwelekeo huo, hutegemea sana mbinu hii kuonyesha tofauti kati ya nguli na hasidi. Katika *Ukawafi wa Miiraji* Mtume Muhammadi (S. A.W), alionyeshwa Pepo na Jehanamu. Paradiso ni mahali pazuri ambapo pamepambwa vizuri. Watakaoingia Peponi watakuwa na furaha isiyo na kifani. Mtunzi anaeleza:

> Akaona p'epo, mfanowe hakuiona
> Ipambiwe fedha na dhahabu kwa marijuana (ubeti 71).

Jehanamu ni mahali pabaya na watakaoenda huko watapata mateso makali. Mtunzi anaeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) hakuweza kustahimili kuiona adhabu kali inayowapata wanaoingia Jehanamu. Alipoteza fahamu na malaika Jibrili akamkumbatia fahamu zikamrudia (ubeti 72).

Mbinu ya kidrama ni ya usawiri wa wahusika ya kuwaonyesha wakitenda matendo na kuzungumza na kuwaacha wasomaji wawaone na kuzichanganua tabia, kutokana na matendo au mazungumzo yao. Katika *Ukawafi wa Miiraji* kuna mazungumzo baina ya Mtume Muhammadi (S. A. W) na Mwenyezi Mungu (ubeti 77-84). Kupitia kwa mazungumzo yao, mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) yanadhihirika na tunauona unyenyekevu wa Mtume Muhammadi (S. A. W) mbele ya Mola. Licha ya hayo, tunafahamu kuwa Allah alimkabidhi Mtume Muhammadi (S. A. W) sala tano yeye mwenyewe.

Mbinu ya kuwatumia wahusika wengine hutumika pale ambapo msanii anamsawiri mhusika kupitia kwa mhusika mwingine. Wahusika wanaweza kuelezwa na wahusika wengine na tunawajua kutokana na maneno ya wahusika wenzao.

Katika *Ukawafi wa Miiraji* wahusika wengine wamesema mengi kumhusu Mtume Muhammadi (S. A. W) na kupitia kwa maneno yao, tumeweza kumjua Mtume Muhammadi (S. A. W) zaidi. Kwa mfano, malaika Jibrili anamwambia Buraki asikatae kumbeba Mtume Muhammadi (S. A. W) ni rafikiye Mwenyezi Mungu (ubeti wa 7).

Maneno yanayotumiwa na manabii na Mitume kutoka mbingu ya kwanza hadi ya saba yanaonyesha kuwa walikuwa na heshima kubwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) na waliutambua utume wake (ubeti 42-56). Aidha, maneno ya Mwenyezi Mungu yametuwezesha kufahamu kwamba Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu anayempenda sana (ubeti wa 81-84).

Mbinu ya kistiari ni ulinganishi wa moja kwa moja ambao hautambulishwi na matumizi ya maneno 'kama' mithili ya, mfano wa na kadhalika. Maneno hutumiwa nje ya maana yake ya kawaida. Mbinu hii inaweza kutumiwa katika usawiri na uendelezaji wa wahusika kwa njia kadha. Katika *Ukawafi wa Miiraji*, mbinu hii inaonekana mara kadha. Kwa mfano, mtunzi anasema kuwa malaika Jibrili na Mtume Muhammadi (S. A. W) waliona mto wa damu, ndani yake mlikuwa na watu ambao walikuwa wakila sumu kwa sababu walikuwa wamekula chakula ambacho kilikatazwa (ubeti 22). Maana yake ni kuwa hawa watu walikula nyama ya mnyama ambaye alichinjwa bila kufuata sheria za Kiislamu. Kwa hivyo, walikula damu ya mnyama ambayo ni sumu maadamu kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, damu ni sumu kwa sababu huwa na roho ya mnyama.

### 2.5 Usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Mtume Muhammadi (S. A.W) ni mhusika mkuu katika *Ukawafi wa Miiraji* kwa sababu matendo yote katika utenzi huu yanamhusu. Dhamira kuu ya mtunzi inajitokeza kupitia kwake na mwingiliano wake na wahusika wengine ndiyo mbinu ya kufafanua dhamira hiyo. Yeye ndiye nguzo ya utenzi huu na ndiye anayesheheni utenzi mzima. Mtunzi *wa Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammad (S. A.W) kama ifuatavyo:

#### 2.5.1 Mtume wa Mwisho wa Mwenyezi Mungu

Mitume katika dini ya Kiislamu ni wale ambao Mwenyezi Mungu aliwatuma kwa watu mbalimbali, ili kuwaelekeza njia yake na kuwaepusha na njia za upotofu za shetani. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amewataja mitume mbalimbali na majukumu yao. Aidha, uwezo waliopewa

na Mwenyezi Mungu unadhihirika. Kwa mfano, Suleimani alipewa uwezo juu ya majini (ubeti 80), Daudi alipewa Zaburi (ubeti 80) na Isa uwezo wa kuwaponya vilema na kuwafufua wafu (ubeti 81). Aidha, amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu aliyeitwa kuwaongoza wanadamu wote kuelekea katika njia nyoofu na ya ufanisi wa milele. Katika utenzi huu mitume wengine wote wanamtambua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume wa mwisho wa Allah. Kwa mfano, katika ubeti wa 45 alipokaribishwa katika mbingu ya kwanza, Adamu anamwambia kuwa yeye ndiye yuko mbele na mitume wengine wote wako nyuma yake. Mwenyezi Mungu mwenyewe anamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa yeye ndiye wa mwisho.

Nawe ni awali ya Mitume, ndiwe aheri
Nidhukuriwapo na isimu yako i nyuma (ubeti 80).

### 2.5.2 Mcha Mungu

Mcha Mungu ni mtu ambaye anamwogopa na anampenda Mwenyezi Mungu. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W)) kama mcha Mungu. Anapoambiwa na malaika Jibrili kuwa Mwenyezi Mungu anamwita aende kwake, hakawii au kuuliza maswali, anatoka usingizini mara moja na wakaanza safari (ubeti 4-5). Mtume alianza kusali mara tu safari ilianza. Mtunzi anasema:

T'umwa kamupanda akaomba Mola Karima (ubeti 9)

Wakiwa safarini ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi Mtume Muhammadi (S. A .W) aliambiwa na malaika Jibrili ashuke kutoka kwa Buraki na asali katika vituo vitatu ambavyo ni muhimu. Vituo hivi ni: Madina, mlima Sinai na Betilahamu. Mtume Muhammadi (S. A.W) anafahamu umuhimu wa kusali, kwani kupitia kwa sala Mwenyezi Mungu anamtimizia mwanadamu mahitaji yake yote. Wanapofika Beti Mukaddasi wanaingia msikitini na wakasali. Mitume wote wanapoingia msikitini, malaika Jibrili anaadhini na akamchagua Mtume Muhammad (S. A. W) awe imamu. Mtume Muhammadi ( S. A.W) anapomwona Mwenyezi Mungu macho kwa macho, hakuweza kuongea tena alipiga magoti na Mwenyezi Mungu akamwambia aitishe chochote alichotaka.

### 2.5.3 Mwenye Akili Pevu

Mtunzi wa utenzi huu amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtu mwenye akili pevu. Katika ubeti wa 41, Mtume anahisi kiu na analetewa vikombe viwili. Kimoja kikiwa kimejazwa maji na maziwa na kingine kikiwa kimejazwa asali na mvinyo. Mtume anachagua maziwa na kwa kuchagua kinywaji cha maziwa, anachagua dini ya Kiislamu. Maziwa yalikuwa ni ishara tu kwa sababu ni rahisi kuyanywa wakati mvinyo ni "mama wa maasi na maovu" na chanzo cha matendo ya kikatili. Kwa hivyo, maziwa yanawakilisha matendo mema na mvinyo unawakilisha matendo maovu.

Wanapokutana na jini safarini ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, malaika Jibrili anamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) akariri aya kutoka kwa *Kur'ani Tukufu*. Mtunzi anasema kuwa Mtume alikariri aya hiyo na Jini likazima. Mtume alijua ni aya gani angesema kutoka kwa *Kur'ani Tukufu* ili jini lisiwadhuru. Mtunzi anaeleza:

> Kisha wakenenda wakaona jinni shadidi
> Na kinga kya moto kumulika T'umwa Sayyidi.
> Jburilu kamba: soma dua, omba Wadudi;
> Tumwa akasoma, 'ifuriti likazizima ( ubeti 13 ).

Isitoshe, katika ubeti wa 32 na wa 33, mtunzi anasema kuwa alizungumziwa na Myahudi na Mkristo lakini anawanyamazia. Malaika Jibrili anamwambia kama angezungumza nao umati wake ungepotea.

### 2.5.4 Hana Dhambi

Mtume Muhammadi (S. A W) amesawiriwa kama mtu asiye na dhambi. Malaika Jibrili alipasua kifua chake na akatoa uchafu wote. Neno uchafu limetumika kistiari na maana yake ni dhambi. Mtunzi anasema:

> Alipoamka muombezi wakapasua.
> Kifua na nyongo zote ghashi wakazitoa (ubeti 5).

Buraki anaposita kumbeba Mtume Muhammadi (S. A. W), malaika Jibrili anamwambia:

> .............mtukue kipendo kyema.(ubeti 7)

### 2.5.5 Aliitwa na Mwenyezi Mungu

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume aleyeitwa na Mwenyezi Mungu aende kwake. Jambo hili linajitokeza katika ubeti wa 4 hadi wa 6. Kwa mfano, ubeti wa 4 mtunzi anaeleza:

> Ilipowadia Mola wetu kudhihirisha
> Jaha ya Nabia Jiburilu alimushusha.
> Alipomwendea, alillele, kamuamusha:
> Ondoka silale, Mola wako akwita hima.

### 2.5.6 Kiongozi wa Dini ya Kiislamu

Kiongozi ni mtu mwenye madaraka ya kuelekeza watu wengine. Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama kiongozi wa dini ya Kiislamu. "Umati wake" katika utenzi huu ni maneno yanayomaanisha wafuasi wa dini ya Kiislamu na kiongozi wao ni Mtume Muhammadi (S. A. W). Beti ambazo zimetumia maneno haya ni kama 33 na 82. Aidha, Jambo hili linadhihirika katika ubeti wa 45. Mtunzi anaeleza:

> Akanza salamu muungamo; akiratili
> Kamba: marahaba mwana mwema T'umwa Rasuli
> Saada ni yako mwenye jaha, ndiwe awali;
> Ndiwe mwenye mbele na Mitume yote i nyuma.

Katika ubeti huu, Adamu anasema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mwenye bahati na ni kiongozi. Pia anasema mitume wengine wote wako nyuma yake.

### 2.5.7 Mtiifu na Msikivu

Mtu mtiifu ni mtu ambaye anafuata kanuni, sheria au amri kwa yale anayoambiwa bila kupinga. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtu mtiifu, jambo ambalo linajitokeza kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi yake. Malaika Jibrili alitumwa na Mwenyezi Mungu akamwite Mtume Muhammadi (S. A. W) aende kwake haraka, alikutwa akiwa usingizini. Alipoamshwa na kupashwa habari hiyo alitii mara moja (ubeti 4-5).

Wakiwa safarini ya kutoka Makka kwenda Beti Mukaddasi, malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) ashuke na aombe mara tatu, alitii na akaomba mara tatu kwenye kila kituo. Kwa mfano, ubeti wa 12 tunaelezwa:

Kisha wakenenda wakafika Betilahamu
Alipozaliwa T'umwa 'Isa buni Maryamu.
Jiburili kamba: Sali hapa utakadamu
Muombe Rabbuka sapa ndipo mahala pema.

Aidha, wanapokutana na jini safarini, malaika Jibrili anamwambia Mtume asome aya kutoka kwa *Kur'ani Tukufu* na Mtume Muhammad (S. A. W) anatii ushauri wake na lile jini linazizima (ubeti 13). Isitoshe, walipofika Beti Mukaddasi mitume wote walikuwa wamekusanyika ndani ya msikiti. Malaika Jibrili akaadhini lakini hawakuwa na imamu. Jibrili alimchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) awe imamu na akatii, na akaongoza sala msikitini mle (ubeti 39). Jambo hili linadhihirisha kwamba Mtume Muhammadi (S. A. W) amepewa hadhi ya juu miongoni mwa mitume wengine wote. Aidha, sala katika dini ya Kiislamu imetambuliwa kama njia inayofaa ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Licha ya hayo, Mtume anapofika mbele ya Mwenyezi Mungu na akamwona alishindwa kusema neno lolote, alipiga magoti naye Mwenyezi alimwambia aitishe chochote alichotaka (ubeti 78). Alitii na kutoka hapo mazungumzo baina ya Mwenyezi Mungu na Mtume yakaanza. Mtume Muhammadi (S. A. W) alipomwambia Musa kuwa alipewa sala hamsini awapelekee watu wake, Musa alimwambia kuwa watu wake hawawezi kuomba sala hamsini kila siku. Musa alimshauri arejee kwa Mwenyezi Mungu ili apunguziwe sala hizo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alitii na alipofika kwa Mwenyezi Mungu alipunguziwa kwa tano. Mtunzi anaeleza kwamba Mtume alirejea mbele ya Mwenyezi Mungu mara kadha. Mwishowe, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipunguziwa sala hizo zikawa tano. Alipowasili Makka, aliwaelezea Makureshi kuhusu safari yake katika mbingu saba na kuwa alimwona Mwenyezi Mungu. Walizipinga habari hizo na kusema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mwongo. Walimwambia kuwa mambo ya mbinguni hawakuwa wanayajua lakini walizifahamu sifa zote za Beti Mukaddasi Walimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) azitaje ( ubeti 102). Mtume alishikwa na woga kwani hakuzikumbuka sifa hizo lakini Mwenyezi Mungu alimwamuru malaika Jibrili kuzinakili na kuziweka machoni pake (ubeti 103). Mtume Muhammadi (S. A.W) alitii na mtunzi anaeleza:

Akawaswifia swifa zake kizikariri
Kapima kwa nyayo na dhira'a hatta shibiri.
Na Abubakari naye kamba: ai Bashiri
Ndizo swifa zake, uswibie zote 'alama ( ubeti 104).

Mtume Muhammadi (S. A. W) alimtii Mwenyezi Mungu na kuwapelekea wafuasi wake sala tano ambazo ni mojawapo ya nguzo muhimu katika dini ya Kiislamu mpaka leo.

### 2.5.8 Anaheshimiwa na Mitume na Manabii Wengine Wote

Kuheshimu ni kuonyesha mtu kuwa unamthamini au unamtukuza kwa kumweka katika daraja la juu. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume anayeheshimiwa na mitume na manabii wengine wote waliomtangulia. Malaika Jibrili anamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) mitume wote wako nyuma yake na kuwa ni mteule na mwombezi wa watu wote. Mtume anasimama mbele ya mitume wengine na kuwaongoza katika sala ndani ya msikiti Mtakatifu.(ubeti 39). Hii ni ishara ya heshima waliyokuwa nayo mitume hawa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W). Anapofika katika kila mbingu kuanzia ya kwanza hadi ya saba, mitume wote walimkaribisha kwa heshima na wakaukubali utume wake. Kwa mfano, katika ubeti wa 51 tunaelezwa:

Kisha wakakia wakafika wingu wa tano;
Wakangia ndani wakaona Nabi Haruno;
Kawakaribisha kwa heshima tukufu muno,
Wakaomba Mungu kuagana kwa dua njema.

### 2.5.9 Ni Mwombezi

Kulingana na TUKI (2004) mwombezi ni mtu anayeombea mtu kwa njia ya sala, ili kumwepusha kutokana na hatari fulani. Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mwombezi wa watu wote, ili waepukane na madhara ya Jehanamu, waingie Peponi Siku ya Kiama. Mtunzi mwenyewe anamtambua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mwombezi katika ubeti wa 2, ubeti wa 52 na ubeti wa 54. Kwa mfano, anasema:

Katoa salamu muombezi kutakadama (ubeti 54).

Malaika Jibrili alipomchagua awe imamu katika msikiti mtakatifu alimwambia kuwa yeye ni mwombezi wa watu wema. Aidha, walipowasili katika mbingu ya nne, walibisha na wakafunguliwa kwa heshima. Mtume Muhammadi (S. A. W) alitambuliwa kama muombezi. Isitoshe, mitume wa awali kama vile Musa na Iburahimu wanamtambua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mwombezi. Kwa mfano, Iburahimu anamkaribisha katika mbingu ya saba na kumwambia:

Ai muombezi, wahubiri umati wako (ubeti 58).

Mwenyezi Mungu alimchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume wa mwisho wa kuwaongoza watu wake katika njia njema naye mwenyewe akampa uwezo wa kuwa mwombezi wa watu wake. Haya yanajitokeza katika ubeti wa 83. Mwenyezi Mungu anasema:

> Ai muombezi wa awali hatta aheri,
> Muombea umma siku nzito ya mahashari;
> Siku ya swirata kutandikwa yuu la nari,
> Ndiwe muombezi siku hiyo wawi na wema.

**2.5.10 Anapendwa na Mwenyezi Mungu**

Kupenda ni kuvutiwa na kitu au mtu, kuwa na mapenzi na kitu au mtu kwa sababu ya uzuri wake. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama anayependwa sana na Mwenyezi Mungu. Mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) yako wazi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utenzi huu. Katika ubeti wa 4 hadi wa 6, mtunzi anaeleza kuwa wakati ulipofika wa Mwenyezi kudhihirisha jaha ya Mtume Muhammadi (S. A. W) alimtuma malaika Jibrili amwendee ampeleke kwake. Aidha, alimtuma Buraki ambaye angembeba katika safari hiyo, hii ni ishara ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume huyu kwa sababu jaha ni zawadi ya kipekee kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Malaika wa Mwenyezi Mungu wanafahamu bila shaka kuwa Mtume huyu ni mpenzi wake Mola, na kwa sabubu hiyo malaika Jibrili anamwambia Buraki:

> Simkengeuke kipendo kye Mola Karimu (ubeti 7).

Aidha, mitume wengine wanamtambua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume anayependwa sana na Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, Musa anamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W):

> Ndiwe ndugu mwema muombezi wa watu jama
> Ni wako umati afudhali ya wote uma;
> Wendapo kwa Mola ukipawa yake karama
> Nasi tukumbuke ngwatujali wako huduma (ubeti 55).

Mazungumzo baina ya Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammadi ( S. A. W) yanaonyesha wazi kuwa Mola anampenda Mtume huyu sana. Mazungumzo yao yalionyesha utaratibu maalum wenye heshima ya hali ya juu. Mwenyezi Mungu alithibitisha kuwa anampenda Mtume Muhammadi (S. A. W).

Mola yumuwene kwa matoye yote mawili
Akanza salamu tahiyatu yake Jalili.
Mola kamujibu: na salamu yako Rasuli,
Ndiwe mutaule wa kuwekwa mahala pema (ubeti 77).

Isitoshe, Mola alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa ndiye mtumwa wa mwisho na jina lake litatajwa pamoja na jina la Mwenyezi Mungu (ubeti 80). Mwishowe, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipowaeleza watu wa Makka kuhusu safari katika mbingu saba na kuwa alikuwa amemwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake, walikataa kumwamini na wakamwambia awaelezee sifa za Beti Mukaddasi kwa sababu walikuwa wanazijua na hawakuwa wanafahamu habari za mbinguni. Mtume Muhammadi (S. A. W) alishikwa na wasiwasi kwa sababu hakuwa anazikumbuka. Mwenyezi Mungu alimwamrisha malaika Jibrili amdhihirishie sifa hizo machoni pake naye akazikariri moja kwa moja. Licha ya hayo, aliwaeleza watu hao siku ambayo wanabiashara aliokuwa amekutana nao wangewasili nyumbani. Siku hiyo ilipowadia, jua lilikuwa karibu kuzama kama hawajawasili na Mtume Muhammadi (S. A. W) akamwomba Mwenyezi Mungu jua lisimame hadi wakati wanabiashara hao wengewasili. Jua lilisimama hadi walipofika. Mwenyezi Mungu alionyesha mapenzi yake kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) kupitia miujiza hiyo (ubeti wa 96-107).

### 2.5.11 Mwenye Huruma

Kuwa na huruma ni kuwa na moyo wa wema. Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mwenye huruma katika *Ukawafi wa Miiraji*. Alipewa sala hamsini na Mwenyezi Mungu awapelekee wafuasi wake, alipofika alipokuwa Musa, alimshauri arudi kwa Mwenyezi Mungu ili apunguziwe sala hizo kwani ungekuwa mzigo mkubwa kwa umati wake kusali sala hamsini kila siku. Mtume aliwaonea watu wake huruma, akafuata ushauri wake Musa na akarudi mbele ya Mwenyezi Mungu kumwomba awapunguzie wafuasi wake sala hizo. (ubeti 86-88). Mtunzi anasema kuwa Mtume alirejea mbele ya Mwenyezi Mungu mara kadha.

Ikawa kunenda na kurudi kuyikallifu (ubeti 88).

Katika wa ubeti wa 72, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaona watu waliokuwa wakiteseka sana wakiwa Jehanamu, hakuwa na ruhusa ya kuwaokoa kutoka kwa mateso hayo. Mtume aliwaonea huruma mpaka akapoteza fahamu na kuzirai lakini malaika Jibrili alimkumbatia na fahamu zikamrudia.

### 2.5.12 Ni Mvumilivu

Mtu mvumilivu ni mtu anayestahimili taabu au mambo mazito. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtu mvumilivu katika utenzi huu wote. Mtume anaamushwa kutoka usingizini na malaika Jibrili, anaamka mara moja, malaika Jibrili anamwambia kuwa Mola alimtaka aende kwake haraka. Mambo haya ni mazito lakini Mtume Muhammadi (S. A. W) aliyavumilia. Kisha akapasuliwa kifua na kutolewa maovu yote yaliyokuwa ndani yake na akashonwa kana kwamba hakupasuliwa. Buraki alikuwa amesimama mbele yao na alipoambiwa ambebe Mtume Muhammadi (S. A. W) alisita na kusema kuwa Mtume alikuwa mwenye dhambi (ubeti 4-7). Mtume hakusema lolote na hii ni ishara ya uvumilivu.

Katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, Mtume anaonyeshwa mambo mengi na akayavumilia. Kwa mfano, mtunzi anaeleza:

> Kisha wakenenda wakaona watu shakiya;
> Wakikatwa ndimi kwa makasi zikirejea.
> Ndio hali yao wakatwapo ndimi kumea.
> iburilu kamba: ni waongo wasyo kalmia (ubeti 24).

Anapofika Makka na kuwaambia Makureshi kuwa alikuwa amesafiri mbinguni na kumwona Mwenyezi Mungu walizikataa na kumdharau Mtume Muhammadi (S. A. W). Mtume anayavumilia madharau yao na anapoambiwa awaelezee sifa za Beti Mukaddasi, anafanya hivyo baada ya Mwenyezi Mungu kumwamrisha malaika Jibrili azidhihirishe machoni pake.( ubeti 104). Hawakukomea hapo, walimwambia awaelezee wakati wafanyabiashara waliokuwa safarini wangewasili nyumbani. Mtume Muhammadi (S. A. W) akawambia wengewasili siku ya tano kutoka siku hiyo.

Siku ilipofika, hawakuwa wamefika wakati jua lilikuwa likizama na Mtume akamwomba Mwenyezi Mungu ili jua lisimame aweze kutimiza ahadi yake. Mola aliyajibu maombi yake lakini Makureshi waliendelea kumdharau Mtume Muhammadi (S. A. W) na akayavumilia yote. Mtunzi anasema:

> Wakamba: ni kweli swifa ndizo mezifaswili;
> Naye ni sahiri kama hayo kwake kalili,
> Kwani yuapenda dini yetu kuibatili,
> Hatumufuati tukawata wetu sanama (ubeti 108).

### 2.5.13 Ana Uwezo wa Kipekee

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume aliye na uwezo wa kipekee. Uwezo huu wa Mtume huyu unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Mazungumzo baina ya Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammadi (S. A. W) yanadhihirisha kuwa uwezo alionao Mtume Muhammadi (S. A. W) unatoka kwake. Kwa mfano, katika ubeti wa 81 Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume:

> Nawe nikupele kufufua na mangi kama
> Ni yako kanizi ya'arishi isiyokoma.

Buraki alikuwa anafahamu kwamba Mtume Muhammadi (S. A. W) ana uwezo wa kipekee na kwa sababu hiyo, alimwomba apate mahala pema katika Pepo. Aidha, hata malaika wa Mwenyezi Mungu waliutambua uwezo wake Mtume Muhammadi (S. A. W), jambo ambalo lilimfanya malaika Jibrili amwambie Mtume:

> ...................haja yangu niitakayo,
> Siku ya swirata niwe kinga ya umatiyo (ubeti 75).

Mitume wengine wanautambua uwezo wa kipekee wa Mtume Muhammadi (S. A. W) kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Musa anamwambia Mtume kuwa akienda kwa Mwenyezi Mungu atapewa karama na awakumbuke ili Mwenyezi Mungu awape nafasi ili wawe watumishi wake ( ubeti 55). Isitoshe, mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* anafahamu kwamba Mtume Muhammadi (S. A. W) ana uwezo wa kipekee. Akimalizia kazi yake anasema:

> Na mwenye kutunga mja wako Muhuyi Dini,
> Atuma'i jaza kwa hidima yake amini
> Mwenye kuhudumu watu wema hupata mema (ubeti 112).

Mwenyezi Mungu anampa Mtume Muhammadi (S. A. W) uwezo hata wa kutenda miujiza. Anawaleza Makureshi kuwa msafara wa wafanyabiashara ungewasili siku ya tano kutoka siku hiyo. Siku inapofika, jua linaanza kuzama kama hawajawasili. Mtume alimwomba Mwenyezi Mungu alisimamishe jua, ili atimize ahadi yake. Jua linasimama mpaka wakati wafanyabiashara hao wanawasili. Suala hili la uwezo wa Mtume Muhammadi (S. A. W) wa kutenda miujiza tumelijadili kwa kina katika sura ya tatu, ambapo tumeangazia sifa za ujagina.

### 2.5.14 Alionyeshwa Pepo na Jehanamu

Pepo ni mahali panapoaminiwa na waumini wa dini ya Kiislamu na dini ya Kikristo kuwa ndipo watakapoishi kwa furaha baada ya kufufuliwa. Jehanamu ni mahali panaposadikiwa kuwa ndiko roho za watu waliomwasi Mwenyezi Mungu zinakokwenda; motoni. Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mtume aliyeonyeshwa Pepo na Jehanamu. Katika ubeti wa 71, mtunzi anasema kuwa Mtume aliona Pepo na hakuwahi kuuona mfano wake. Anasema kuwa mahali hapa ni pazuri sana kwani pamepambwa kweli kweli. Kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, hakuna mtu amewahi kuiona Pepo akiwa hai. Tena akoanyeshwa Jehanamu na mtunzi anaeleza:

> Kisha wakatoka kaonyeshwa moto mukali,
> Kaona vituko vya ‘adhabu hakuhimili.
> Kakosa fahamu ikazulu yake ‘akili,
> Jiburili thamma kamudhumu akafahama (ubeti 72).

### 2.5.15 Anapenda Kufahamu Mambo

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtu ambaye anapenda kufahamu mambo. Wakiwa safarini aliuliza maswali kadha ili aelewe matukio ya ajabu ambayo alikuwa akiyaona. Kwa mfano, katika ubeti wa 52, Mtunzi anasema kuwa Mtume alipowaona watu weupe kama karatasi na wengine wenye madoadoa waliokuwa wakiingia motoni na kuwa weupe kama wenzao, aliuliza malaika Jibrili waliokuwa na heshima walikuwa akina nani. Naye akamjibu kuwa wale weupe kama karatasi ni watu wema ambao hawakutenda dhambi. Waliokuwa na madoadoa ni watenda dhambi, lakini wakitubu dhambi zao wanaungana na hao wengine. Mfano mwingine uko katika ubeti wa 92. Tunaelezwa:

> Kisha wakashuka wakafika wingu wa tini;
> Wakaona vumbi na sauti na moshi ndani.
> Tumwa kamuliza Jiburilu: ni watu gani?
> Kamba: Sheitani wazuiwa kuona sama.

### 2.5.16 Alimwona Mwenyezi Mungu

Katika *Ukawafi wa Miiraji*, Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mtume aliyemwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake, na akazungumza naye. Mwenyezi Mungu mwenyewe alimwita Mtume aende kwake na akamtuma malaika Jibrili amwendee. Walipofika daraja la nane malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa alikuwa amefika

mwisho wake na hakuruhusiwa kwenda mbele. Kutoka hapo, Mtume alikalia rafurafu na akaenda alipokuwa Mwenyezi Mungu. Kutoka ubeti wa 78 hadi wa 84 mtunzi anaelezea mazungumzo baina ya Mwenyezi na Mtume Muhammadi (S. A. W). Kwa mfano:

Kamba: Mola wangu, muja wako Iburahimu
Ni wako mwendani, name nini yangu sehemu?
Mola kamwambia: nawe T'umwa wangu fahamu
Ni kipendo kyangu afudhali ya wote T'umwa (ubeti 79).

### 2.5.17 Alipewa Sala Tano na Mwenyezi Mungu

Sala ni dua zinazotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa lengo la kumshukuru au kumwomba asaidie wanaosali. Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mtume aliyepewa sala tano na Mwenyezi Mungu awapelekee wafuasi wake. Mtunzi anaeleza kuwa mwanzoni Mtume alikuwa amepatiwa sala hamsini:

Saya upeweyo, haku mtu aliyepewa;
Uhimidi kwayo ushukuru zangu zipawa
Nikufaridhie hamusini sala tukuwa,
Wewe na umati kulla siku Sali timama (ubeti 84).

Musa alimwambia kuwa itakuwa vigumu kwa umati wake kuomba sala hamsini kila siku. Musa alimshauri arudi kwa Mwenyezi Mungu amwombe ampunguzie sala hizo. Mtume aloporejea mara kadha mbele ya Mola. Mwishowe, sala hizo zilipunguzwa hadi tano.

### 2.5.18 Mwenye Heshima

Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama Mtume aliye na heshima ya hali ya juu katika utenzi huu. Mtunzi anadhihirisha heshima hii mara nyingi katika kazi yake. Kwa mfano, Mtume alikuwa anampa malaika Jibrili nafasi abishe na aelezee Mtume alikuwa nani kuanzia mbingu ya kwanza hadi ya saba. Aidha, kupitia kwa salamu baina yake na mitume wengine na hata watu aliokutana nao wakiwa katika msafara wa kibiashara alipokuwa akielekea Makka kutoka mbinguni, mtunzi anadhihirisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na heshima kubwa. Isitoshe, heshima hii mtunzi anaiweka wazi Mtume anapozungumza na Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa 78 tunaelezwa:

Alipomuona Mola wake aso mithili,
Asiweze neno kutamuka yake kauli;
Akenda sijida. Kamwambia Mola Jalili:
Omba utakalo utapewa yote timama

### 2.5.19 Ni Mwaminifu

Mtu mwaminifu ni mtu anayeahidi na kutenda jambo kama alivyoagizwa. Mtume Muhammadi (S. A W) amesawiriwa kama mtu mwaminifu katika *Ukawafi wa Miiraji*. Katika ubeti wa 7 na wa 8, Buraki anamwomba Mtume zawadi ya kupata nafasi nzuri katika Pepo. Mtume anakubali kuyatimiza matakwa ya mnyama huyu, jambo ambalo linamfanya ambebe Mtume Muhammadi (S. A. W).

Mwenyezi Mungu ametia uaminifu huu ndani ya moyo wa Mtume Muhammadi (S. A. W) na kwa sababu hiyo, alimpa sala tano awapelekee watu wake. Mtume aliwafikishia watu wake sala hizo tano. Mpaka leo kila Muislamu anapaswa kufuata utaratibu maalum na kuhakikisha amezisali sala hizo tano kila siku.

### 2.5.20 Ni Mkweli

Mtu mkweli anasema ukweli. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amamsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtu mkweli. Mtunzi anaeleza kuwa, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipofika Makka kutoka safari ya mbingu saba, alikuwa na hofu kuwa Makureshi hawangeamini habari kuhusu safari yake ya mbinguni. Abu Jahali alimwona akiwa katika hali hiyo na akataka kujua kilichokuwa kikisababisha hali hiyo. Mtume hakusema uongo, bali alimwambia ya kwamba usiku huo alienda safari ya mbinguni na akamwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Aidha, alimpa mambo ya kuhifadhiwa moyoni mwake. Abu Jahali alipowakusanya Makureshi wote wasikilize habari alizokuwa nazo Mtume Muhammadi (S. A. W), Mtume alionyesha kuwa alikuwa mkweli kwa sababu aliwaelezea habari hizo bila kuficha chochote. Mtunzi anaeleza:

> Akamba: na'amu, t'akwambia yangu habari;
> Usiku wa leo nalikwenda mbali safari,
> K'afika mbinguni nikaona Mola Jabbari,
> Akanipa mambo ya kutunza wangu mutima (ubeti 99).

### 2.5.21 Alionyeshwa Wanayopitia Watenda Maovu na Watenda Mema

Wema na uovu ni dhana kinzani. Wema ni mambo mazuri anayoyafanya mtu ilhali uovu ni hali ya kutenda maovu. Katika *Ukawafi wa Miiraji,* Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama mtume aliyeonyeshwa wanayopitia watenda maovu na watenda mema.

Mtunzi wa utenzi huu ameeleza haya kuanzia ubeti wa 14 mpaka 36. Kwa mfano, katika ubeti wa 14, mtunzi anaeleza kuwa Mtume anaonyeshwa watu wakipanda na kuvuna baada ya muda mfupi. Malaika Jibrili anamweleza kuwa, hao ni wale walikufa katika vita vitakatifu na wameingia Peponi. Hawa walikuwa katika hali ya furaha kubwa.

Kinyume na haya, katika ubeti wa 20, Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa wazinifu. Mbele yao kulikuwa na nyama nzuri iliyononа vizuri na pembeni mwao kulikuwa na nyama duni iliyooza yenye uvundo. Wakawa wanakula ile nyama duni iliyooza yenye uvundo na wanaiacha ile nzuri iliyonona. Aidha, alionyeshwa watu wakikatwa ndimi zao kwa makasi huku zikirejea tena. Mtume Muhammadi (S. A. W) akaelezwa kuwa hao ni waongo na hawamtii Mwenyezi Mungu (ubeti 24). Hawa walikuwa katika hali ya dhiki kubwa.

### 2.5.22 Anazungumza na Malaika wa Mwenyezi Mungu.

Malaika ni kiumbe asiyeonekana ambaye hudaiwa kuwa mtumishi wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alimtuma malaika Jibrili amwongoze Mtume Muhammadi (S. A. W) katika safari ya kutoka Makka hadi mbinguni, na kutoka mbinguni hadi Makka. Mtunzi wa utenzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawari Mtume Muhammadi (S. A. W) kama mtume ambaye anazungumza na malaika wa Mwenyezi Mungu. Mazungumzo baina ya Mtume Muhammadi (S. A. W) na malaika Jibrili yanadhihirika kuanzia mwanzo wa utenzi huu mpaka mwisho wake. Kwa mfano, katika ubeti wa 57 tunaelezwa:

> Akaona mutu mwenye jaha kuu jalili,
> Kauliza T'umwa: mutu gani? Kamba: Halili.
> Mwendaniwe Mola ndiye jaddi yako aswali.
> Kamupa salamu yake jaddi Iburahima.

### 2.5.23 Ni Jagina

Jagina ni mtu mwenye ujasiri, awezaye kukabili mambo ya hatari bila hofu. Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina. Kuna matukio mengi katika utenzi huu yanayodhihirisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni jagina katika dini ya Kiislamu. Kwa mfano, kwenda kwa safari katika mbingu saba, safari ambayo haikuwa rahisi kwani mtunzi anaeleza kuwa kuna wakati mmoja Mtume Muhammadi (S. A. W) alipoteza fahamu baada ya kuona vile watu wanapitia adhabu kali katika Jehanamu.

Pia, alipomwona Mwenyezi Mungu anashindwa na kusema neno lolote. Kama ilivyo kwa majagina wengine, wanapoenda safari katika nchi nyingine huwaletea wanajamii zawadi. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaletea wafuasi wake zawadi ya sala tano.

Alipowasili Makka kutoka safarini hii, hakunyamaza hata ingawa alikuwa na hofu kwamba wanajamii wenzake wangezikataa habari hizo. Aliwaelezea yote yaliyokuwa yametendeka usiku huo: Katika ubeti wa 99 mtunzi anatueleza:

> Akamba: na'amu, t'akwambia yangu habari;
> Usiku wa leo nalikwenda mbali safari,
> K'afika mbinguni nikaona Mola Jabbari,
> Akanipa mambo ya kutunza wangu mutima.

**2.6 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeangalia muhtasari wa *Ukawafi wa Miiraji*. Tumeangazia fomula ya mtunzi. Ametanguliza utendi huu kwa fomula ambayo watunzi wa tenzi za kidini hutumia kama vile kulitaja jina la Mwenyezi Mungu na kumpa sifa kadha. Aidha, analitaja jina la Mtume Muhammadi ( S. A. W), aila yake na masahaba wake. Mwishowe, akadhihirisha umuhimu wao katika dini ya Kiislamu. Tumeangalia vile malaika Jibrili alimwendea Mtume akiwa usingizini na kumwambia kuwa Mwenyezi Mungu alimtaka aende kwake. Tumeelezea kutakaswa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) na kubebwa na Buraki .

Tumeshughulikia safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi. Tumeelezea vituo ambavyo malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) asali. Aidha, katika safari hii Mtume alionyeshwa maajabu mengi ya mambo ambayo watenda mema na maovu huyapitia na tumeelezea vile Mtume Muhammadi (S. A. W) alichaguliwa na malaika Jibrili awe imamu wa mitume wengine walipofika katika msikiti mtakatifu.Tumeshughulikia safari ya kutoka Beti Mukaddasi hadi mbingu saba na jinsi malaika Jibrili na Mtume Muhammadi (S. A.W) walikaribishwa katika mbingu saba. Alikutana na mitume wengine wa awali na wakaukubali utume wake. Tumeangalia maajabu ya mbinguni ambayo Mtume alionyeshwa. Tumeelezea mazunguzo kati ya Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammadi (S. A. W) na kukabidhiwa sala hamsini. Mwishowe, sala hizi zilipunguzwa na Mwenyezi Mungu zikawa tano.

Katika sehemu hii tumemalizia kwa kuangalia safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) ya kutoka mbinguni hadi Makka. Vile vile, tumeelezea kukataliwa kwa habari ya Mtume Muhammadi

(S. A. W) na Makureshi. Isitoshe, katika sura hii tumeangalia ingawa kwa kifupi tu mazingira ya kihistoria anamopatikana Mtume Muhammadi (S. A. W) na tumeona kuwa Mwenyezi Mungu alimwita Mtume wakati jamii ilikuwa imekumbwa na maovu mengi katika nyanja zote za maisha. Tumeangalia pia maana ya usawiri na mbinu ambazo mtunzi anaweza kuzitumia kumsawiri mhusika fulani katika kazi ya kifasihi. Tumezitaja mbinu hizo na kutoa mifano ya jinsi zimetumika katika utenzi tunaotumia. Mwishowe, tumeangalia jinsi Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa mfano, tumeona amesawiriwa kama mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu, mwaminifu, mwombezi, mtiifu na kama mtume aliyemwona Mwenyezi Mungu na ni jagina.

## SURA YA TATU

## SIFA ZA UJAGINA NA MATUKIO YA UJAGINA KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI*

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeangalia muhtasari wa *Ukawafi wa Miiraji* na usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika utenzi huu. Tumeeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama jagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa hivyo, tumeonelea kuwa ni muhimu kuzichanganua sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika utenzi huu. Hata ingawa tumezichanganua sifa za ujagina, si zote zitadhihirika katika utenzi tunaoshughulikia, kwa sababu *Ukawafi wa Miiraji* unahusu safari ya Mtume Muhammadi (S. A. W) katika mbingu saba. Sifa za ujagina ambazo tumezishughulikia ni pamoja na: aghalabu jagina huwa wa kiume, jina la jagina, jagina huwa na akili pevu, maisha na matendo ya jagina huwa ya kimiujiza na jagina huwa haeleweki kwa urahisi.

Mwishowe, tumeyachanganua matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Jagina huenda safari ya ajabu na anapotoka safirini hiyo huwaletea wanajamii zawadi. Mtume Muhammadi (S. A. W) ni jagina wa kidini na alienda safari ya ajabu katika mbingu saba, ambapo alikutana na mitume wengine wote wa awali. Mwishowe, alimwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Mwenyezi Mungu alimpatia sala tano awapelekee wafuasi wake. Kwa hivyo, sala ambazo Waislamu husali mara tano kwa siku kwa kufuata utaratibu maalum zilitoka kwa Mwenyezi Mungu. Isitoshe, kuna matukio mengine mengi ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa mfano, uchaguzi wa dini ya Kiislamu, Mtume Muhammadi (S. A. W) kuongoza sala katika Beti Mukaddasi na kuwaelezea Makureshi juu ya safari yake katika mbingu saba.

### 3.2 Sifa za Ujagina

Mutiso (1999: 1) anaainisha majagina katika makundi matatu. Anasema jagina wa kwanza ni kiumbe wa kweli ambaye amekuzwa na amejikuza mwenyewe hata akaonekana kiumbe wa ajabu. Kiumbe huyu huwa ni mashuhuri na husifika kwa ujasiri, nguvu, (hata kama amelemaa, ulemavu huu ni onyo kuwa baadaye atakuwa na nguvu za ajabu) na kwa kila jambo lionekanalo kubwa au la ajabu katika jamii husika, hata kama jambo hilo twaliona ni la kipuuzi. Mabadiliko yote mazuri yatokeayo katika jamii, jamii husika huamini ya kwamba yameletwa na jagina wao, hata kama jagina huyo hausiki kamwe.

Kwa kawaida, jagina huyu hutokana na familia maskini lakini jamii yake huamini ya kwamba ametokana na familia tajiri ya kifalme. Maisha yake huwa ni taabu na dhiki na ya kutangatanga. Yumkini, watu humwabudu baada ya kifo chake. (kwa kawaida hata akifa huaminika ya kwamba yu hai na anayaona tuyatendayo).

Mutiso (khj) anaendelea kufafanua aina ya pili ya jagina kama kiumbe wa kihurafa, ambaye ameumbwa na jamii yake. Kiumbe huyu pia huwa na sifa ambazo si za kawaida na ghalibu awe ni Mungu au yote mawili. Yumkini, iaminike ya kwamba jagina huyu ndiye mzazi wa jamii husika. Anaendelea kueleza kuwa jagina wa tatu ni mhusika mkuu wa katika utenzi, tamthilia, riwaya, hadithi, ngano, sinema, kitendo au jambo. Mpaka kati ya aina hizi tatu za majagina ni mwembamba, kwani mhusika mkuu anaweza kuwa ni mmojawapo wa aina mbili zingine za majagina.

Kwa sababu hii, tunapomjadili Mtume Muhammadi (S. A. W) ambaye ni jagina wa kidini, tunamweleza kwa kuzingatia makundi matatu ya ujagina kulingana na Mutiso (khj). Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mhusika mkuu katika *Ukawafi wa Miiraji*, ni jagina katika dini ya Kiislamu na ana uwezo usio wa kawaida. Waislamu huamini kuwa Mtume huyu yu hai na anayaona wanayoyatenda. Kulingana na Gaster, kama anavyonukuliwa na Gichamba (2005) jagina ni mtu ambaye humliki uwezo zaidi kuliko uwezo wa watu wa kawaida na hutumia uwezo huu kiujasiri na huwa tayari kuyahatarisha maisha yake kwa manufaa ya watu wengine.

Kutoka na madai ya wataalamu hawa, jagina huwa na sifa za kipekee na uwezo usio wa kawaida. Aghalabu, wafuasi wa dini mbalimbali huamini kuwa uwezo wa majagina wao, hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ili kueleza sifa za ujagina, tumerejelea *Ukawafi wa Miiraji*. Huu ni utenzi ambao msingi wake ni katika *Kur'ani Tukufu*. Kwa hivyo, tumerejelea *Kurani Tukufu* na inapobidi *Biblia* na vitabu vingine vya kidini, ili kuchanganua sifa za ujagina ambazo hazijajitokeza katika utenzi huu. Aidha, tumetalii mitandao tofauti ili kuchanganua maisha na matendo ya kimiujiza ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Isitoshe, tumetoa mifano mingine ya majagina wa kidini ili kubainisha sifa za jagina wa kidini.

### 3.2.1 Kabla ya Kuzuka kwa Jagina

Jamii ni mfumo ambao huwa na mahitaji mengi. Mahitaji haya huzua asasi mbalimbali mojawapo ikiwa ni asasi ya ujagina. Asasi hii ni muhimu katika kusawazisha hali zilizoenda

kombo katika jamii. Kama tulivyosema katika sura ya pili, jagina huwa hazuki katika ombwe tupu, bali huzuka katika kipindi, mazingira na wakati maalum katika jamii yake na huishi hadi pale ambapo atatekeleza dhamira yake. Ni kutokana na sababu hii, ambapo wanajamii wanamtazama jagina kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wengi wa majagina, kama wale wa kidini huzuka katika mazingira ambamo mna vita na maovu mengi.

Kwa mfano, Mtume Muhammadi (S. A. W) alizuka katika mazingira ambayo yalijaa maovu mengi. Maovu hayo yalijikita katika nyanja zote za maisha. Kwa mfano, hakukuwa na mfumo wowote wa kisiasa ule. Hakuna sehemu ya Arabia ilikuwa na serikali isipokuwa Yemen. Waarabu hawakutambua mamlaka yoyote ile, isipokuwa ya machifu wa makabila yao. Kabila lilikuwa na jukumu la kulinda watu wake, hata kama walitenda maovu. Ukabila ulichukua nafasi ya kwanza kabla ya maadili. Kwa vile hapakuwa na serikali, hapakuwa na sheria na utulivu. Hali hii ilisababisha mapigano yasiyokuwa na kikomo. Vita vilikuwa ni desturi ya kudumu ya jamii ya Kiarabu. Vita hivi vilidumisha uthibiti mkali juu ya ongezeko la watu. Aghalabu, waarabu walipigana bila kuwa na sababu yoyote ya kufanya hivyo.

Kiuchumi, Wayahudi ndio walikuwa viongozi wa Arabia. Walikuwa ndio wenye ardhi nzuri yenye kulimika, na walikuwa wakulima wazuri zaidi nchini humo. Isitoshe, walikuwa ndio wawekezaji wa viwanda vilivyokuwepo Arabia wakati huo. Aidha, walishikilia ukiritimba wa utengenezaji wa zana za kivita. Utumwa ulikuwa ni asasi ya kiuchumi ya Waarabu. Watumwa wa kike na wa kiume walikuwa wakiuzwa kama wanyama.Waliunda tabaka la waliokandamizwa zaidi katika jamii ya Kiarabu. Tabaka lenye nguvu zaidi la Waarabu, liliundwa na mabepari na wakopeshaji fedha. Viwango vya riba walivyotoza vilikuwa vikubwa sana. Viliundwa ili viwafanye matajiri waendelee kutajirika, na wakopaji wawe maskini zaidi.

Kijamii, Arabia ilikuwa ni jamii iliyoshikiliwa na wanaume. Wanawake hawakuwa na hadhi ya aina yoyote ila kuwa bidhaa vya ngono. Idadi ya wanawake mtu angeweza kuoa haikukadiriwa. Mwanamume alipokufa, mwanawe “alirithi” wake zake wote, isipokuwa mama yake mzazi. Kama tulivyosema katika sura ya pili, Waarabu walikuwa na tabia ya kikatili ya kuwazika watoto wao wa kike wakiwa hai. Hata kama Mwarabu hakutaka kumzika binti yake akiwa hai, ilimlazimu adumishe mila hii, kwa vile hakuwa na uwezo wa kuhimili shinikizo la jamii. Ulevi na uchezaji kamari ulikuwa ni mazoea mabaya ya Waarabu. Wanawake wengi waliuza mapenzi ili kupata riziki ya kila siku.

Kabla ya Uislamu, Waarabu walikuwa na dini mbalimbali. Kwa mfano, Waarabu wengi walikuwa wakiabudu masanamu, kuna wale waliamini kuwa hakukuwa na Mungu, na dunia ilikuwa ya milele. Aidha, kulikuwa na Mayahudi na Wakristo. Idadi ya walioamini Mungu mmoja ilikuwa ya kiwango cha chini sana. Kulikuwa na Waarabu wachache walioweza kusoma na kuandika. Wengi wao hawakuwa na hamu ya kujifunza fani hizi. Elimu ya ushairi ndiyo ilipewa kipaumbele.

Kulingana na Gathara (2015) Nabii Isa alizuka kama jagina kwa Wayahudi ambao baada ya kutawaliwa na kulipishwa kodi na mataifa mengine hata kutumika kama watumwa, walitarajia kutimizwa kwa ubashiri wa Nabii Isaya kuhusu kuzaliwa kwa mfalme wa wafalme ambaye, angewakomboa kutoka kwa maadui zao. Wayahudi walitarajia kiongozi wa kijeshi.

Kabla ya kuzuka kwa Musa, Waisraeli walikuwa wakitendewa unyama na Firauni (mfalme wa Misri). Firauni aliogopa kuwa wana wa Israeli wangeungana na taifa lingine na kumtoa mamlakani. Kwa hivyo, akawafanya kuwa watumwa. Walipitia mateso mengi, lakini Mungu aliwabariki. Waliendelea kuongezeka na kadri idadi yao ilivyozidi kuongezeka, ndivyo Firauni alvyozidi kuwaogopa. Licha ya hayo, Kabla ya kuzuka kwa Samsoni, wana wa Israeli walikuwa mikononi mwa Wafilisti kwa muda wa miaka arobaini.

### 3.2.2 Ubashiri wa Kuzaliwa kwa Jagina

Ubashiri ni maelezo ya mambo ambayo yatakuja kutukia siku za mbele. Kulingana na Mutiso (1999: 4) kuzaliwa kwa jagina huwa kumebashiriwa na kusipobashiriwa huthibitishwa baada ya jagina kuzaliwa. Hali ya ubashiri inadhihirika sana katika kuzaliwa kwa majagina wa kidini ambapo kabla hawajazaliwa kunatokea mbashiri ambaye anawatia moyo wanajamii wazidi kuwa na uvumilivu huku akiwaambia kuwa jagina atazaliwa, ambaye atakuwa na uwezo mkubwa na ufalme wake utakuwa mkubwa kuliko falme zingine zote. Mwishowe, atawakomboa watu kutoka dhiki zao. Kwa mfano, kuja kwa Mtume Isa kulitabiliwa na nabii Isaya na hata malaika Jibrili. Isaya alipeleka ujumbe dhahiri kwa nyumba ya Daudi akisema:

"Tazama bikira atashika mimba na kuzaa mwana ambaye ataitwa Immanueli" (*Isaya* 7: 14).

Pia, Isaya alitabiri juu ya ufalme wake kwa kusema kuwa utawala wake hautakuwa na mwisho. Malaika Jibrili alipomtokea Mariamu alimwambia kazi maalum ambayo Isa angefanya. Anasema:

> Na tazama utashika mimba na kuzaa mtoto wa kiume ambaye utamwita Yesu. Atakuwa mkuu na ataitwa mwana wa aliye juu na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake: na atatawala juu ya nyumba ya Yakobo, milele na kuhusu utawala wake hautakuwa na mwisho (*Luka* 1: 31-33).

Aidha, Waislamu huamini kuwa kuja kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) kumebashiriwa mara nyingi katika *Biblia*. Kwa mfano, katika *Kumbukumbu la Torati* 18: 16-20 tunaelezwa kuwa siku ya mkutano katika Horeb, wana wa Israeli walipokataa kusikia sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu alimwambia Musa:

> Wametenda vyema kusema walivyosema, mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyeyasikiliza maneno yangu atakayoyasema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake, lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwangazia kulinena au atakayenena kwa jina miungu wengine, nabii yule atakufa.

Waislamu huamini kuwa anayetabiriwa na Mwenyezi Mungu ni Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa kuwa ana sifa zote zinazotajwa katika bashiri yenyewe. Kwa mfano, Mtume Muhammadi (S. A. W) anaambiwa na Mwenyezi Mungu afikishe yote aliyoteremshiwa (*Kurani Tukufu* 5: 68).

Mutiso (Khj) anasema kuwa hata kuzaliwa kwa majagina wengine wa kidini huwa kumetabiriwa. Tena anaeleza kwamba kuzaliwa kwa Gautama Buddha kwa mfano, kulitabiriwa na watabiri sitini na wanne walioifasiri ndoto ya mamake kabla ya kuzaliwa kwake. Kulingana naye, kuzaliwa kwa Samsoni aliyewakomboa Waisraeli kutoka kwa Wafilisti kulitabiriwa na malaika (*Waamuzi* 13:3 kwenye *Biblia*).

Aidha, kuzaliwa kwa Musa kulitabiriwa na wachawi na wapiga ramli wa Misri. Katika *Kurani Tukufu* 7:127 tunaelezwa kuwa siku moja Firauni aliota moto ukiwa umetoka Baiti Mukaddasi,

ukielekea Misri. Moto huo uliunguza nyumba za Wamisri ukiacha nyumba za Waisraeli. Alipoamka, aliwaita wachawi na wapiga ramli ili wamfasirie ndoto yake. Walimwambia kuwa atatokea kijana miongoni mwa Waisraeli, ambaye ataangamiza utawala wake na kuibadili dini yake.

Jagina anapozaliwa kunakuwa na ishara inayoonyesha kuwa mtoto aliyezaliwa ni mtoto wa kipekee. Sifa hii inajitokeza vyema zaidi katika *Biblia*. Kwa mfano, baada ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, malaika wa Mungu aliwatokea wachungaji waliokuwa wakichunga wanyama wao karibu na Bethlehemu. Malaika huyo alitangaza:

> "Leo katika jiji la Daudi Mwokozi ambaye ni Kristo Bwana amezaliwa kwenu".
> (*Luka* 2: 8-11) kisha, umati wa jeshi la mbingu ukawa pamoja na yule malaika, ukimsifu Mungu wakisema: Utukufu katika vilele vilivyo juu kwa Mungu na juu ya duniani kwa watu wa nia njema" (*Luka* 2: 13, 14).

Aidha, kulingana na Hakeem (1956) mama yake Mtume Muhammadi aliona katika ndoto nuru kubwa ikitoka katika mwili wake, na kutapakaa katika nchi zote.

### 3.2.3 Utoto na Ujana wa Jagina

Mara nyingi utoto na ujana wa jagina hauelezwi na ukielezwa, huwa si kwa undani kama inavyostahili. Wakati mwingine wanahistoria huchanganya utoto wa kuzaliwa kwa jagina na ujana wake na kuwa kitu kimoja. Hii ni kwa sababu jagina anapozaliwa, hukua kama mtu wa kawaida tu. Lakini baadaye ndipo watu humtambua kutokana na matendo, tabia na uwezo wake usio wa kawaida na ndipo watu huanza kumtukuza.

Kulingana na Safeyy (2002:67) kama ilivyokuwa desturi ya watu wa Makka, kuwapeleka watoto wao wachanga kwenda kulelewa na wanawake wa vijijini ambako hewa ya huko ilikuwa nzuri zaidi kuliko ya mjini, Mtume Muhammadi (S. A. W) alilelewa na Halima. Mwanamke ambaye alikuwa maskini. Halima alimrudisha Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa mama yake akiwa na miaka minne. Tabia ya Mtume Muhammadi (S. A. W) ilikuwa tofauti sana na ya watoto wengine wa umri wake, kwa sababu kila mtu aliyemjua aliona matendo yake yenye fikra. Baba yake mdogo alimpenda sana hata alitaka Mtume awe naye kila wakati.

Katika ujana wake, Mtume Muhammadi (S. A. W) hakushiriki katika maovu yaliyokuwa yamekithiri katika jamii wakati huo. Waarabu walikuwa wakiona fahari juu ya maovu kama vile ulevi, na wanawake kuuza miili yao. Maisha ya Mtume Muhammadi (S. A. W) ya utotoni na ujanani yalikuwa mazuri na safi. Alijitenga na watu wote wabaya na alikuwa na marafiki wachache sana, lakini marafiki hao walifuata mafundisho yake na mwishowe wakasilimu. Katika *Kurani Tukufu* tunaelezwa utukufu wa tabia ya Mtume Muhammadi (S. A. W):

> " Nimeishi wakati mrefu na ninyi, na mwajua vizuri sana kwamba sijapata kusema uwongo hata juu ya mtu. Vipi sasa nitawezaje kusema uwongo juu ya Mungu. Kwa nini hamwamini mafundisho yangu?"(*Aya* 10: 17)

Mtume Muhammadi (S. A. W) alioa bibi wake wa kwanza akiwa na umri wa miaka ishirini na mitano.Nabii Isa alifahamu toka utotoni mwake kuwa alikuwa na nafasi muhimu kama masihi na hivyo hakushiriki michezo kama watoto wengineo.

Katika *Biblia* (1*Samweli* 1/ 2: 1-11) utoto na ujana wa Nabii Samweli umechanganywa. Tunaelezwa kuwa Hana, mkewe Elikana alikuwa tasa. Aliomba Mungu kwa muda mrefu ili ampatie mtoto. Aliahidi Mungu kuwa kama angempatia mtoto, angempeleka kanisani ili amtumikie. Mungu aliyajibu maombi yake. Alimwita mtoto wake Samweli, jina lenye maana ya "habari za Mungu". Mtoto alipoachishwa maziwa, mama yake alifunga safari kwenda Shilo, kumpeleka kwa huduma ya Mungu. Alimwachia Eli, ambaye alikuwa mtumishi wa Mungu. Samweli akiwa kijana, alijionea waziwazi upotovu na uovu wa watoto wa Eli. Aidha, tunaelezwa tu kuwa Samweli alikua kulingana na mapenzi ya Mungu.

Gautama Buddha alipozaliwa, familia yake ilikuwa na hamu kubwa sana, kwamba angekua kama mtoto wa mfalme mpiganaji, halafu baadaye aurithi ufalme wa baba yake. Mtabiri mzee alisema kuwa mtoto huyo angekuwa nabii mkubwa. Baba yake alipanga njia za kuzuia utabiri huo kutimia. Mtoto hakuruhusiwa kutoka nje peke yake. Matembezi yake yalipaswa kuongozwa, na hakuruhusiwa kukutana na yeyote aliyekuwa maskini au mwenye mateso. Gautama alikuwa kijana mwenye ari isiyokuwa ya kawaida. Siku moja, bila wazazi na walimu wake kufahamu, aliongozwa na mtumishi aliyemchagua kwa uangalifu, na akaenda matembezini kwa gari lake nje ya kasri. Kwa mara ya kwanza, aliyaona mateso ambayo watu wa tabaka la chini walikuwa

wakiyapitia. Kwa mfano, aliona mzee aliyekuwa mgonjwa, kibofu, mtu mwenye huzuni, ambaye alikuwa amekonda sana, na akitoa wadudu kutoka kwa mwili wake. Baba yake alijaribu kuzuia hali hii lakini akashindwa. Gautama alikata shauri moyoni mwake, kuondoka katika maisha ya kifalme na kutafuta maisha ya utawa.

### 3.2.4 Jagina kwa Kawaida Huwa ni Mwanamume

Mara nyingi majagina huwa ni wanaume. Jagina huzuka katika jamii ambayo imekumbwa na misukosuko ya aina mbalimbali. Kwa mfano, ya kivita, kiuchumi na kisiasa. Wanajamii huamini kuwa jagina atawakomboa kutoka kwa dhiki ambazo wanazipitia. Kwa mfano, kama tulivyosema awali, baada ya utabiri wa kuzaliwa kwa nabii Isa, Wayahudi walitarajia kiongozi wa kivita. Kwa vile jamii inamsawiri mwanamke kama mwoga na dhaifu, ni nadra kuwa na jagina wa kike. Wanajamii huwa na dhana kuwa mwanamume huwa na nguvu ya kumwezesha kukabiliana na hali yoyote ngumu katika jamii, kama vile vita. Mifano ya majagina wa kiume ni pamoja na: Mtume Muhammadi (S. A. W), Yesu Kristo, Samsoni, Musa, Samweli, Suleimani, Buddha na wengine wengi.

### 3.2.5 Jina la Jagina

Mara nyingi jagina hupewa jina linaloakisi hulka, matendo na tabia yake. Kwa hivyo, jagina hapewi jina vivi hivi tu. Jina lake huashiria sifa fulani aliyo nayo. Kutokana na jina la jagina tunaweza tukaielezea hulka yake. Majina ya kimajazi pamoja na lakabu mbalimbali hutegemea mitazamo ya wanajamii kuhusiana na sifa za jagina wao.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na majina ya majazi. Jina la Mtume alipatiwa na mama yake kabla ya kuzaliwa kwake. Mama yake aliota kesha mzaa Mtume na lazima aitwe "Muhammadi" jina ambalo lina maana ya asifiwaye. Mtume Muhammadi (S. A. W) alizaliwa katika mazingira yaliyohinikiza matendo maovu. Yeye alijizuia na uovu, utovu wa nidhamu na vitendo vyote vya kuaibisha. Alikuwa mwerevu, mkweli, mwaminifu na mwenye bidii. Kwa hivyo, alipata umashuhuri sana na kupendwa sana. Kutokana na tabia nzuri zisizokuwa na kifani walizoziona kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) na ambazo walikuwa hawajawahi kuziona kwa binadamu yeyote kabla yake, ziliwafanya wakaamua kumpatia jina la heshima la "Al-Amin", neno la Kiarabu lenye maana ya "Mwaminifu mkweli".

Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mhusika mkuu katika *Ukawafi wa Miiraji*. Amesawiriwa kama kiongozi wa dini ya Kiislamu katika utenzi huu. Mwenyezi Mungu alimchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) kama Mtume wa mwisho na akampa uwezo wa kipekee wa kutenda miujiza. Kwa hivyo, Muhammadi amepewa majina mengine. Kwa mfano," Rasuli" jina lenye maana ya mjumbe aliyeletwa na Mwenyezi Mungu ili kutangaza ujumbe wake na kuwaongoza watu wake katika njia njema. Visawe vya jina hili ni Mtume, Rasua, Nabii na Mukhtari. Muombezi ni jina lingine la Mtume Muhammadi (S. A. W). Jina hili linatumiwa kurejelea mtu anayeombea au kuwatetea watu au mtu mwingine. Mtume Muhammadi (S. A. W) amerejelewa kama Muombezi wa Waislamu Siku ya Kiyama. Nafasi muhimu ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwaombea Waislamu, inampa hadhi ya juu kuliko mitume wengine wote. Majina mengine ya Mtume Muhammadi ni pamoja na: Muungamu, Nyota, Mustafa, Muhimidiwa, Sharifu, Siraji, Kipingo, Taa, Bashiri na Habibu.

Katika *Biblia* Nabii Isa anaitwa simba wa Yuda, Mshauri mwema, Mwalimu, Mchungaji mwema, Mwokozi, Mwanakondoo, mwana wa Daudi, Emanueli (Mungu pamoja nasi).

### 3.2.6 Jagina Hutoka Katika Ukoo wa Kifalme

Aghalabu jagina hutoka katika ukoo ambao umechukuliwa na wanajamii kuwa ni ule ambao umetengwa na kuteuliwa na Mwenyezi Mungu ili uongoze jamii na kuikomboa kutokana na shida za misukosuko inayokumba wanajamii husika. Majagina wa kidini, akiwepo Nabii Isa, Mtume Muhammadi na Gautama Buddha walitokana na ukoo bora. Nabii Isa alitokana na ukoo wa mfalme Daudi, Mtume Muhammadi (S. A. W) alitokana na ukoo wa kabila la Kikureshi na Gautama Buddha alitokana na ukoo bora ulioitwa Sakya, ulioaminika kutokana na mayai yaliyoanguliwa na jua (Mutiso 1999:5). Aidha, Samsoni alitokana na ukoo bora wa Wadani.

### 3.2.7 Majagina Huwa na Akili Pevu

Majagina ulimwenguni huwa na akili pevu na uwezo wa kung'amua mambo yaliyofichika. Uwezo huu mara nyingi huwasaidia kuepuka mambo ambayo si mazuri. Aidha, unamwezesha kutatua shida ambazo zinaikumba jamii. Licha ya hayo, jagina huwa na uwezo wa kutabiri yale yatatokea baadaye. Kwa mfano, Isa ambaye ni jagina wa wakristo aliyatabiri mambo mengi ambayo hatimaye yalitokea. Kwa mfano, alitabiri kifo chake, kufufuka na hata kupaa kwake mbinguni.

Katika *Ukawafi wa Miiraji* Mtume Muhammadi ( S. A. W), alichagua dini ya Kiislamu kwa kutumia akili zake pevu. Mtume Muhammadi (S. A. W) alipohisi kiu, aliletewa vyombo viwili vikiwa vimejazwa kwa vinywaji tofauti tofauti, kimoja kikiwa kimejazwa maziwa na maji na cha pili, asali tamu na mvinyo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alichagua kile kilikuwa na maziwa. Kwa kuchagua maziwa, Mtume alichagua dini ya Kiislamu kwa sababu maziwa yalikuwa ni ishara ya dini hiyo. Maziwa yaliwakilisha matendo mema na mvinyo uliwakilisha matendo maovu (ubeti 41).

Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na akili pevu ambayo iliwasaidia wanajamii kutatua shida zao. Kwa mfano, siku moja Waarabu walipokuwa wakijenga upya Kaaba Tukufu, kulitokea ugomvi mzito wa kutosikilizana kati ya makabila kuhusiana na uwekaji wa jiwe jeusi mahala pake kwenye Kaaba hiyo. Hivyo ikawa ni nivute nikuvute na amani ikawa iko hatarini ya kutoweka kati yao. Watu wote wakamchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa msuluhishi wa ugomvi wao. Mtume aliwaamuru watu hao waliweke jiwe hilo jeusi katika shuka lenye ncha nne, kisha akawaamuru wakuu wa makabila hayo kila mtu ashike pembe za shuka hilo na kulinyanyua juu. Wakuu wa makabila hayo wakafanya hivyo na kisha Mtume Muhammadi (S. A. W) akapanda juu ya Kaaba mpaka usawa wa kukaa jiwe hilo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alilipokea na kuliweka mahala pake kwenye Kaaba hiyo Tukufu, ambako mpaka leo hii jiwe hilo liko mahala pale.

Aidha, majagina wengine wa kidini huwa na akili pevu. Kwa mfano, kupevuka kwa akili ya Nabii Isa kunaweza kudhibitishwa na mafundisho aliyoyatoa. Alifunza kwa kutumia vielelezo mbazi ambavyo viliufanya umati uliomfuata kuajabia mafundisho yake. Umati uliohutubiwa na Nabii Isa uliajabia mafundisho ambayo yalitokana na mtu ambaye Wakristo wanaamini kuwa hakusoma.

Isitoshe, Mwenyezi Mungu alimpa Sulemani hekima, ambayo aliitumia kutatua matatizo ya jamii. Kwa mfano, wakati mmoja wanawake wawili walimfikia Sulemani wakiwa na tatizo gumu. Mwanamke mmoja alimweleza mtume kuwa, waliishi pamoja wakiwa wanawake wawili, na kila mmoja akajifungua mtoto wa kiume. Aliendelea kusema kuwa wakati mtoto wa mwenzake alikufa, alimweka karibu naye, na akamchukua mtoto wake. Alipoamka, alimtazama mtoto aliyekufa na akaona hakuwa wake. Naye mwenzake alisema mtoto aliyekuwa hai alikuwa wake. Sulemani aliitisha upanga amkate mtoto vipande viwili ili ampe kila mwanamke nusu

yake. Mama mtoto alilia na akamwambia asimwue mtoto. Aidha, alisema mtoto apewe mama mwenzake. Naye mama mwenzake alitilia mkazo mtoto akatwe vipande viwili kila mmoja wao apewe kipande chake. Sulemani aliamua mtoto apewe mama wa kwanza. Alijua hivyo, kwa sababu mama wa kweli alionyesha mapenzi ya hali ya juu kwa mtoto wake. Suleimani aliamua kumpa mwanamke huyo mtoto wake asiuawe. Wanajamii waliposikia namna Suleimani alivyotatua tatizo hilo, walifurahi kuwa mfalme huyo ni mwenye akili pevu.

### 3.2.8 Maisha na Matendo ya Jagina ni ya Kimiujiza

Maisha ya majagina kote duniani yamejaa matendo ya kimiujiza. Wafuasi wa dini mbalimbali huamini kuwa uwezo wa majagina wao wa kutenda miujiza hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, wafuasi wa dini mbalimbali humchukulia Mwenyezi Mungu kuwa Jagina wa majagina. Miujiza wanayotenda pamoja na uwezo wao usio wa kawaida hutoka kwa Mwenyezi Mungu na huwafanya wanajamii kuwaajabia. Mtume Muhammadi (S. A. W) alitenda miujiza mingi kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu. Katika *Ukawafi wa Miiraji*, alimwomba Mwenyezi Mungu alisimamishe jua ili wafanyabiashara wafike Makka kwa wakati ambao alikuwa amewaambia Makureshi wangewasili. Jua lilisimama hadi akatimiza ahadi yake. (ubeti 107).

Aidha, alitenda miujiza mingine maishani mwake. Kwa mfano, kububujika maji katika vidole vya Mtume pindi maswahaba wake walipopatwa na kiu na wakawa hawana maji isipokuwa katika chombo kidogo tu, wakati makafiri wa Makka walimwomba awaonyeshe muujiza, Mtume aliwaonyesha kupasuka kwa mwezi na alilitemea mate jicho la Qatadana baada ya kuvimba jicho na jicho hilo kurudia hali yake ya kawaida. Pia, katika vita vya Badri, Mtume Muhammadi (S. A. W) alirusha vijiwe kwa ishara ya kimuujiza upande wa mapagani wa Makka, ambao walikuwa karibu 1000. Hakuna hata mmoja wa waabudu masanamu hawa alitoroka, bila kugongwa jichoni (*Kurani Tukufu* 3:11).

Kulingana na Mutiso (1996) Mtume Muhammadi (S. A. W) aliambia mti uende kwake. Mti ulisogea huku ukiinua mizizi yake kutoka ardhini ukielekea kwa Mtume. Ulikuwa ukivuta mizizi yake na ukitiririkwa na machozi hadi mbele ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Ulimwamkua kwa kusema, “Amani iwe nawe Mtume wa Mungu”. Mtume Muhammadi aliambia mti ule urudi mahala pake na ukafanya hivyo mara moja. Mutiso (khj), anasema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa ameombwa kutenda muujiza huu na Muarabu mmoja.

Isitoshe, Mtume Muhammadi (S. A. W) na Abu Bakari walipokuwa njiani wakielekea Madina, walihisi njaa na kiu. Jangwani kulikuwa na mwanamke wa Bedouin aliyekuwa katika hema. Walipofika hapo, walimwomba kinywaji, naye aliwaambia kuwa hakuwa na chochote, isipokuwa mbuzi mmoja mzee na hakuwa anatoa maziwa. Mtume Muhammadi (S. A. W) alipogusa kiwele cha mbuzi huyo, alitoa maziwa kwa wingi. Waliyanywa wakatosheka na kumwachia mwanamke huyo pamoja mume wake, maziwa mengi. Walipoondoka, mwanamke alishangaa, kwa sababu mbuzi huyo aliendelea kumpa maziwa chungu nzima.

Nabii Musa alitenda miujiza mbele ya Firauni kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, alitupa fimbo yake chini ikawa nyoka. Kisha, akaweka mkono wake kwenye mfuko wa kanzu yake, alipoutoa ukawa unameremeta kwa weupe. Watu wa Firauni wakasema kuwa Musa alikuwa mchawi mkubwa. Basi, walikusanyika ili wamshinde Musa. Lakini walipotupa kamba na fimbo zao, watazamaji wakaona kama ni nyoka wanaotembea. Nabii Musa akatupa fimbo yake, ikameza yote waliyoyabuni. Wale wachawi wakasilimu na kuamini utume wa Nabii Musa (*Kurani Takatifu* 7: 107-121).

Aidha, majagina wengine wa kidini walitenda mambo ya ajabu. Kwa mfano, miujiza ya Yesu Kristo ambaye ni jagina wa Wakristo imeelezwa katika vitabu vya *Injili*. Baadhi ya miujiza ambayo ilitendwa na jagina huyu wa Wakristo ni pamoja na: kuwawezesha vipofu kuona, kwa mfano, kwenye kitabu cha *Mathayo* (9: 27-31) ambapo tunaelezwa kuwa Yesu alipoingia chumbani, alifuatwa na vipofu wawili waliomlilia na kumwomba kuwa "Yesu mwana wa Nazareti, tuonee huruma" Yesu alipowauliza kama walikuwa na imani kuwa angewaponya, walionyesha imani yao kwa kuitikia. Yesu aliwaguza kwenye macho na wakaweza kuona. Zaidi ya hayo, Yesu Kristo aliwafufua wafu. Kwa mfano, katika kitabu cha *Yohana* 11: 1-45 tunaelezwa kuwa Lazaro alikuwa amekufa na Yesu alipofika nyumbani kwao, alikuwa kaburini kwa muda wa siku nne.Yesu aliomba kisha akasema " Lazaro, njoo huku nje". Lazaro aliyekuwa amekufa akatoka akiwa amefungwa sanda miguuni na mikononi na uso wake ulikuwa umefungwa kwa leso. Yesu akawaambia "mfungueni, mkamwache aende zake".

Isitoshe, Elisha aliyekuwa nabii miongoni mwa Waisraeli alitenda miujiza mingi. Kwa mfano, kufufua mtoto wa mwanamke Mshunami, kuongezeka kwa mafuta ya mjane, kumponya Naamani ukoma, kuongezeka kwa mikate na katika 2 *Wafalme* 6: 4-7, tunaelezwa:

> Nao walipofika Yordani, wakakata miti. Lakini mmoja wao alipokuwa katika kukata boriti, chuma cha shoka kikaanguka majini.; akalia, akasema, ole wangu! Bwana wangu, kwani kiliazimwa kile. Mtu wa Mungu akasema, kilianguka wapi? Akamwonyesha mahali. Akakata kijiti, akakitupa pale pale, chuma kikaelea. Akasema, kiokote. Basi akanyosha mkono, akakitwaa.

### 3.2.9 Safari ya Ajabu Ya Dunia Nyingine Na Kurudi Kwake

Jagina huwa anaenda safari ya ajabu ya dunia nyingine na anaporudi huwaletea wafuasi wake zawadi. Katika safari hii jagina huwa anaongozwa, kwa sababu ni safari ngumu. Asipoongozwa, jagina hushindwa na kuikamilisha. Aidha, jagina hukumbana na vikwazo vingi ambavyo huvishinda, akisaidiwa na kiongozi wake. Mtume Muhammadi (S. A. W) alienda safari katika mbingu saba akiwa amebebwa na mnyama wa ajabu aitwaye Buraki. Safari hii iliongozwa na malaika Jibrili. Kabla ya kuanza safari hii Mtume Muhammadi (S. A. W) alitakaswa kwa kupasuliwa kifua na kutolewa maovu yote kisha akashonwa kama kwamba hakupasuliwa. Safari hii imegawa katika awamu tatu.

Katika awamu ya kwanza Mtume Muhammadi (S. A. W) alisafari kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi. Katika safari hii Mtume anaonyeshwa adhabu za watenda maovu kama vile wazinifu ambao walikuwa wakiacha nyama nzuri na kula nyama mbaya. Malaika Jibrili alikuwa akimwelezea Mtume adhabu mbalimbali ambazo zilipatiwa watenda dhambi tofauti tofauti. Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) alikutana na jini, ambalo lilikuwa likimmulika kwa kijinga cha moto. Malaika Jibrili alimshauri akariri aya katika *Kurani Tukufu* na jini likazima. Walipofika Beti Mukaddasi Mtume Muhammadi (S. A. W) aliongoza mitume wengine katika sala. Katika awamu ya pili Mtume Muhammadi (S. A. W) alipandishwa kutoka mbingu ya kwanza hadi mbingu ya saba. Katika awamu hii Mtume alikutana na mitume wa awali, kuanzia Adamu mpaka Iburahimu. Mitume hawa waliukubali utume wa Mtume Muhammadi (S. A. W). Mwishowe Mtume alikutana na Mwenyezi Mungu na akapewa sala tano ambazo aliwapelekea wafuasi wake. Katika awamu ya tatu Mtume alianza safari ya kurudi Makka na alimkuta malaika Jibrili alipokuwa amemwacha. Waliteremka kutoka mbinguni na walimwona Buraki mahali walikuwa wamemwacha. Mtumwa alimpanda na wakaanza safari ya kurudi Makka. Njiani walikutana na misafara ya ngamia na wafanyabiashara. Walipofika Makka, Mtume Muhammadi

(S. A. W) aliwaelezea Makureshi kuwa alikuwa amesafiri hadi mbinguni usiku huo, na akazungumza na Mwenyezi mungu. Hawakuzikubali habari hizo, walimdharau.

Aidha, Yesu Kristo ambaye ni jagina katika dini ya Kikristo aliend safari ya siku tatu. Aliongozwa na Mwenyezi Mungu. Wakristo wanaamini kuwa Yesu aliikabidhi roho yake kwa Baba yake, akafa na wakati fulani toka kufa mpaka kufufuka, akatembelea kuzimu. Kuzimuni aliwasilisha ujumbe kwa viumbe wa kiroho waliokuwa na uhusiano na nyakati za kabla ya gharika ya Nuhu (1 *Petro* 3: 18-19). Yesu Kristo aliwaletea wafuasi wake zawadi ya wokovu.

### 3.2.10 Majagina na Suala la Ndoa

Majagina duniani kote, kwa kawaida hawaoi na wakioa huwa wanaoa wake wengi. Wakati mwingine, mwanamke anayeolewa na jagina huwa chanzo cha mauti yake. Wakristo huamini kuwa Yesu Kristo hakuoa. Mtume Muhammadi (S. A. W) alioa wake wengi. Safeyy (2002:73) ameelezea vile Mtume alimwoa mke wake wa kwanza Khadija. Safeyy (Khj) anasema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipokuwa na umri wa miaka ishirini, mwanamke mmoja tajiri mkubwa wa Makka, aliyekuwa akiitwa Khadija, baada ya kuona sifa nzuri za Mtume na uaminifu wake wa hali ya juu, alimchagua kuwa mwakilishi wake katika masuala ya biashara zake. Khadija alipata faida kubwa sana kutokana na ukweli, uaminifu, busara na bidii ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Mwanamke huyu aliendelea kuvutiwa zaidi na uzuri wa Mtume na hatimaye akatoa pendekezo la kutaka kuolewa naye. Mtume Muhammadi (S. A. W) alikubali pendekezo hilo na katika umri wa miaka ishirini na mitano akamuoa mwanamke huyo aliyekuwa tajiri mkubwa. Khadija alipokuwa hai, Mtume hakuoa mwanamke mwingine. Baada ya kifo chake Khadija, Mtume Muhammadi (S. A. W) alioa wanawake wengine wakiwemo masuria wawili. Mmoja wao alikuwa Bibi Maria aliyemzalia mwanawe Ibrahimu. Lengo la msingi la Mtume Muhammadi (S. A. W) kuoa wake wengi lilikuwa ni kupata walimu wanawake wa Kiislamu. Walimu hawa walipaswa kufunza wanawake wenzao masuala yanayohusu sheria za wanawake waislamu. Kwa mfano, hukumu za hedhi na masuala ya ndoa. Wake za Mtume Muhammadi (S. A. W) wanajulikana kama mama za waumini.

Mfalme Sulemani aliwapenda wanawake wengi wa kigeni. Alioa wanawake mia saba binti za kifalme, na masuria mia tatu. Mungu alikuwa amewaonya wana wa Waisraeli dhidi ya kuwaoa wanawake wa kigeni. Sulemani alipokuwa mzee, wake zake walimgeuza moyo wake, akafuata miungu mingine. Mungu alikasirishwa na jambo hilo (1 *Wafalme* 11: 1-10).

Samsoni alimpenda Delila, mwanamke wa Kifilisti. Wakuu watano wa muungano wa Wafilisti walitaka sana kumwangamiza Samsoni. Kwa hivyo, walitafuta msaada wa Delila. Walimwendea na kumwambia:

> Mdanganye ili uone nguvu zake nyingi zinatokana na nini, na kile tunachoweza kutumia ili kumshinda. Kila mmoja wetu atakupatia vipande elfu moja na mia moja vya fedha (*Waamuzi* 16: 4, 5).

Delila alimdadisi Samsoni hadi akajua siri ya nguvu zake. Alimlaza usingizi magotini pake, kisha akamwita mtu akamnyoa nywele zake. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa mateso ya jagina huyu. Wafilisti walimkamata, wakamng'oa macho; wakaenda naye mpaka Gaza, wakamfunga vifungo vya shaba. Alikuwa akisaga ngano katika gereza. Mwishowe alikufia hekaluni pamoja na Wafilisti chungu nzima.

### 3.2.11 Jagina Huhusishwa na Zaidi ya Jamii Moja

Jagina huhusishwa na na zaidi ya jamii moja. Mara nyingi hatambuliwi na kuhusishwa tu na watu wake bali pia na watu kutoka jamii zingine. Hata hivyo, jagina wa kidini hujitolea kufa kupona ili kuwakomboa watu kutoka kwa maovu na kuwaelekeza kwenye njia inayofaa. Lengo la jagina wakidini ni kuwa na wafuasi wengi. Majagina wa kidini kwa mfano, Mtume Muhammadi (S. A. W), Isa (Yesu) na Buddha walikuwa si wa jamii moja bali wa ulimwengu mzima. Licha ya Yesu Kristo kutoka katika ukoo wa Daudi, alichukuliwa na Wakristo wote kama mkombozi wao. Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) ni jagina wa Waislamu wote duniani naye Buddha ni jagina wa wafuasi wake wote ulimwenguni.

Watu wa kawaida hufa na kusahaulika baada ya miaka michache. Wanajamii huwa hawaamini kuwa jagina wao ameaga na wengi huchukulia kuwa ameenda safari na kuwa atarudi siku moja. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliishi duniani miaka mingi iliyopita na hukumbukwa daima kama ilivyo kwa majagina wengine wa kidini kama vile Buddha na Isa. Kila jamii inawajibika kuwafunza watoto kuwahusu majagina wao, ambao huzuka katika vipindi na hali mbalimbali katika jamii hiyo. Katika kukumbukwa mashujaa hutungiwa nyimbo, tenzi, mashairi, maandishi chungu nzima hutungwa kwa mambo mbalimbali na kuhifadhiwa kama kumbukumbu kwa minajili ya vizazi vijavyo. Inaaminika miongoni mwa wakristo na waislamu kuwa Nabii Isa atarudi ulimwenguni kuikamilisha kazi alioianzisha.

### 3.2.12 Wapinzani wa Jagina

Hakuna jagina yeyote ulimwenguni ambaye hana maadui, kwa kawaida mtu huwa na watu wanaomchukia na wale wanaompenda. Maadui wa jagina humwonea wivu kuona jinsi wanajamii wanavyomchukulia kama mkombozi. Wengine hata huwa na nia ya kumwua jagina.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na wapinzani wengi. El-Geyoushi (1985) anaeleza kuwa makafiri na maadui wa Mtume mjini Makka walikuwa na njama ya kumwua kabla ya kuhajiri kwake kwenda Madina. Mwenyezi Mungu alibatilisha njama hiyo na kumuepusha Mtume wake na hatari hiyo kubwa kwa njia ya muujiza. Watu wa Madina walimwalika Mtume Muhammadi (S. A. W) aelekee katika mji wao na kuahidi kumlinda dhidi ya hujuma ya kabila la Kureshi lililopanga kumuua na kuvuruga juhudi zake za kuwakomboa watu na kuwatoa kwenye ujahili. Waislamu wa Makka walianza kuhama taratibu kutoka mji huo kuelekea Madina.

Wakuu wa Kureshi walipogundua mpango huo na kuhisi hatari, walianza kupanga njama ya kuuvuruga. Walikutana katika majilisi ya mashauriano mjini Makka ili kupanga mikakati ya kukabiliana na dini tukufu ya Kiislamu na kusimamisha ujumbe wa Mtume Muhammadi (S. A. W). Kila mmoja katika majilisi hiyo alitoa maoni na mawazo yake hadi fursa ilipofikia Abu Jahili ambaye alisimama na kusema:

> "Mimi nina fikra sahihi kuhusu suala hili wala siamini fikra nyingine. Tutamchagua kijana mmoja shujaa na mpiganaji hodari kutoka kila kabila na kisha kuwapa mapanga makali ambayo watayatumia kumshambulia kwa pamoja Mtume Muhammadi (S. A. W). Kwa njia hii umwagaji wa damu yake italihusu kila kabila lililoshiriki mauaji hayo na sidhani kama ukoo wake utaweza kukabiliana na koo zinginezo zote za Kureshi. Kwa hivyo, utafidiwa na sisi na kwa upande wa pili tutakuwa tumeondokana na Muhammadi (S. A. W)".

Mwenyezi Mungu alimfahamisha Mtume wake njama hiyo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alitumia mbinu ya kupoteza nyayo na alama na kwa msingi huo katika usiku ambao makafiri walikuwa wamepanga kumuua, alishauriana na Ali na kumwomba alale kwenye kitanda chake ili kuwahadaa maadui na hivyo kuokoa roho ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Mtume Muhammadi ( S. A. W) alikuwa na wapinzani wengine kama vile Herekali katika *Utenzi wa Tambuka*.Herekali alikuwa kiongozi wa Wakristo. Alikuwa kiongozi katili ambaye aliwadhulumu watu, hasa Waislamu. Ukatili wake ulidhihirika kutokana na kitendo chake cha kumwua Jaffari, aliyekuwa mpwa wa Mtume Muhammadi (S. A. W) pamoja na washirika wake wengine sita. Mungu alimtuma malaika Jibrili kumwamuru Mtume Muhammadi alipize kisasi. Mtume Muhammadi (S. A. W) alichukua hatua ya kutuma waraka kwa mfalme Herekali asilimu la sivyo apigwe vita. Mfalme Herekali alipokataa kusilimu, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwatuma wajumbe miongoni mwa makabila ya Kiislamu ya Uarabuni akaitisha vita. Baada ya maandalizi ya kutosha, kulizuka vita baina ya Waislamu na Wakristo katika mji wa Tambuka, vikiongozwa na Mtume Muhammadi (S. A. W) na mfalme Herekali mtawalia. Vita vilipiganwa kwa awamu mbalimbali. Majeshi ya kila upande yalipigana kwa ujasiri ili washinde. Waislamu waliendelea kushindwa lakini Ali, mkwewe Mtume Muhammadi (S. A. W), aliletwa katika uwanja wa vita kimiujiza na kuchangia kuleta ushindi wa mwisho kwa Waislamu.

Isitoshe, siku moja Mtume Muhammadi (S. A. W) alipokuwa amepiga magoti, na ameinamisha mgongo wake akisali katika Kaaba, Abu Jahili alichukua mtoto mchanga wa ngamia, ambaye siku zake za kuzaliwa hazikuwa zimetimia, na akamweka shingoni pa Mtume. Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na tabia ya kutoka nyumbani alfajiri kwenda kusali. Wapinzani wake waliweka matawi ya miti ya miiba katika njia yake, ikawa katika giza alijiumiza kwa miiba hiyo. Mara nyingine wapinzani wake walimtupia mchanga na mawe. Hakeem (1956) anaeleza kuwa siku moja kikundi cha Makureshi walimshambulia Mtume Muhammadi (S. A. W). Mmoja wao alirusha kilemba chake na kukizungusha katika shingo ya Mtume. Kwa kukivuta kwa nguvu alikaza shingo ya Mtume hata ikawa maisha yake yaliokolewa na Abu Bakari aliposema:

> “Mwataka kumwua mtu huyu kwa sababu
> anasema kuwa Mungu ni Mola wake”.

Aidha, naye Yesu Kristo aliteswa na wapinzani wake mpaka wakamuua. Vitabu vya *Injili* katika *Biblia* vina habari ya jinsi Yuda alimsaliti Yesu Kristo, Wayahudi Waandishi na Mafarisayo walimkamata na kumtesa hadi kufa. Aidha, jagina huyu wa wakristo alipozaliwa, Herode Mkuu, mfalme wa Yudea, aliwatuma watu wakawaue wavulana wote waliokuwa chini ya miaka miwili huko Bethlehemu akiwa na lengo la kutaka kumwua Yesu kwa sababu aliohofia kupokonywa ufalme wake na jagina huyu.

### 3.2.13 Jagina Huwa Kipenzi cha Wanajamii

Hata ikiwa jagina huwa na maadui zao, pia huwa kipenzi cha jamii. Maadui zake huwa na wivu kuona jinsi wanajamii wanavyomchukulia kama mkombozi wao na hivyo kumwenzi na vile vile kutarajia mambo makubwa zaidi kutoka kwake, hasa kuleta mabadiliko yanayotarajiwa kuwapeleka hadi ufanisi wa hali ya juu. Si ajabu kuwa wanajamii wengi huhusisha mambo yote mazuri katika jamii na shujaa wao. Kwa hivyo, umaarufu wa jagina huenea kila mahali.

Kifo cha yesu Kristo kwa mujibu wa *Biblia* kilipoteza matumaini ya watu waliokuwa wakimwamini, ndugu zake, wanafunzi pamoja na wafuasi wake. Watu walilia na kuombeleza pale msalabani kwa kuwa mtetezi wao ametoweka japokuwa waliahidiwa kuwa siku ya tatu atafufuka.

Umaarufu wa Mtume Muhammadi (S. A. W) ulinea haraka sana, si tu katika Makka bali hata katika sehemu zingine za ulimwengu. Jambo hili lanadhihirika katika maisha yote ya Mtume Muhammadi (S. A. W), kutoka kuzaliwa kwake hadi kifo chake. Umaarufu wake ulimwezesha kueneza dini ya Kiislamu katika sehemu nyingi kama Madina, licha ya kuwa alikuwa na maadui wengi waliokuwa wakimtesa hata wengine wakiwa na nia ya kumwua. Kutokana na umaarufu wake, baadhi ya watu wa Madina walikwenda Makka kwa hija ya kila mwaka, walionana na Mtume Muhammadi (S. A. W) naye akawaeleza mafunzo ya dini ya Kiislamu. Walipendezwa sana na wakakiri Uislamu. Waliporejea Madina watu hao waliwasimulia watu wa Madina habari za Uislamu. Mwaka uliofuata watu wengi zaidi walimtembelea Mtume Muhammadi (S. A. W) na wote walikubali Uislamu. Walimwomba Mtume ahamie Madina na afanye mji huo kuwa maskani yake. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwajibu kuwa wakati wake wa kutoka Makka haukuwa umefika lakini aliwaahidi kuwa angekwenda huko baadaye.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na marafiki wengi kama vile Abu Bakari, ambaye anatajwa mara kadhaa katika maisha ya Mtume Muhammadi (S. A.W). Kulingana na Ibraheem (1985) Mtume aliwashauri wafuasi wake wengi wahamie Madina, lakini alimwambia rafiki yake Abu Bakari aachwe naye Makka. Watu wa Makka walipopanga kumwua Mtume, Mwenyezi Mungu alimwambia ahamie Madina. Abu Bakari alikaa na Mtume Muhammadi (S. A. W) katika pango la Thaur kwa muda wa siku tatu, wakijificha maadui wa Makka. Baadaye Abu aliandamana na Mtume Muhammadi (S. A. W) hadi Makka.

Aidha, Waislamu huamini kwamba Abu Bakari ndiye aliyekuwa mwanamume wa kwanza kuukubali Uislamu. Naye Ali alikuwa tayari kila wakati kuyahatarisha maisha yake ili kumwokoa Mtume Muhammadi (S. A. W) kutoka kwa hatari yoyote ile. Kwa mfano, kama tulivyosema awali, alikubali kulala katika kitanda cha Mtume wakati watu wa Makka walikuwa na nia ya kumwua Mtume. Aliwahadaa maadui na kuokoa roho ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Ali alichukua hatua ya kuhatarisha maisha yake mwenyewe, kwa kukubali kulala katika kitanda cha Mtume. Alikuwa akifahamu vyema makafiri wa Makka walipanga kumshambulia, na kumwua Mtume Muhammadi (S. A. W) katika kitanda hicho. Licha ya hayo, Ali alikuwa akisaidia kwa kiwango kikubwa, wafuasi wa Mtume Muhammadi (S. A. W) kushinda wapinzani wao vitani.

### 3.2.14 Kugura kwa Jagina Kutoka Nyumbani Kwao

Mara nyingi jagina hutoroka nyumbani kwao na kwenda kuishi mahali pengine mbali na nyumbani. Sababu ya kufanya hivi ni kuhepa maadui zake ambao mara nyingi huwa ni viongozi. Viongozi hao aghalabu hufikiria kuwa jagina ambaye ana uwezo usio wa kawaida huenda akavamia wakati wowote na kupindua dola zao. Kwa mfano, wale watu wa Makka ambao walijipatia riziki za maisha yao kama watunzaji wa makanisa ambako masanamu yaliabudiwa, hawakuweza kumsikiliza mtu yeyote ambaye alifundisha watu kuabudu Mungu Mmoja. Mtume Muhammadi (S. A. W) alihama kutoka Makka na kwenda Madina. Waabudu masanamu wa Makka walibuni mpango wa siri wa kumwua Mtume Muhammadi ( S. A. W). Wakati wa usiku waliizunguka nyumba yake kwa nia ya kuivamia mwishoni mwa usiku na kumkatakata vipande vipande akiwa kitandani, lakini Mwenyezi Mungu alimjulisha mpango huo na akamuamuru kuondoka na kwenda Madina.

Mtume alimwambia Ali alale kitandani mwake ili kwamba maadui wasigundue kutokuwepo kwake; bila ya kusita Ali alikubali kutoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Kisha akaondoka hapo nyumbani chini ya ulinzi wa kimbinguni, akiwapitia maadui zake katikati yao na akachukua hifadhi ndani ya pango karibu na Makka. Baada ya maadui zake kumtafuta kwa siku tatu kila mahali, walikata tamaa ya kumkamata na wakarudi Makka. Mtume naye akaondoka kuelekea Madina. Watu wa Madina, ambao walikuwa tayari wamekwisha ukubali ujumbe wake Mtume Muhammadi (S. A. W), walimkaribisha kwa ukarimu kabisa na wakayaweka maisha na mali yao chini ya mamlaka yake.

Kugura kwa Yesu Kristo kumeelezwa katika Biblia. Kama ilivyo desturi ya majagina wengi, punde tu baada ya kuzaliwa, Yesu alikutana na vikwazo vya kutaka kuuawa na Mfalme Herode, ambaye alihofia kunyang'anywa madaraka, jagina huyu atakapokuwa mkubwa (*Mathayo 2:13*). Malaika wa Mungu alimtokea Yusufu (baba wa Yesu) katika ndoto na kumweleza amchukue mtoto Yesu na mama yake (Mariamu) kisha wakimbilie Misri. Baada ya Mfalme Herode kufa, jagina Yesu alirudishwa na wazazi wake mji wa Nazareti.

Nabiii Musa aligura kutoka Misri akaenda Midiani. Kugura kwake kumeelezwa katika *Biblia* kitabu cha *Kutoka*. Siku moja  Musa aliona Mmisri akimpiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. Alipohakikisha hakuna aliyekuwa akimwona, alimpiga Mmisri hadi akafa na akamficha ndani ya mchanga. Siku ya pili, aliwaona Waebrania wakipigana. Aliuliza mmoja wao kwa nini alikuwa anamdhulumu mwenzake. Naye akamwuliza kama alikuwa anataka kumuua vile alikuwa amemwua Mmisri. Nabii Musa alipojua siri yake ilikuwa imegunduliwa, aliguria nchi ya Midiani, ambako aliishi mpaka wakati Mwenyezi Mungu alimtuma Misri kuwaokoa wana wa Israeli kutoka utumwani.

### 3.2.15 Majagina Aghalabu Huwa Magwiji Katika Vita

Majagina mara nyingi huwa magwiji katika vita kwa sababu wanazuka ili kuikomboa jamii yao. Majagina huwa hawagopi chochote. Ni kutokana na hali ya kivita ndipo ujagina wao hudhihirika.

Kulingana na Hakeem (1956) Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa uwezo wake  Mwenyezi Mungu alikuwa hodari katika vita. Aliwaongoza Waislamu katika vita vingi kati ya washirikina wa Kiarabu na Wayahudi. Waislamu waliibuka washindi katika mengi ya mapambano hayo. Katika mapigano yote makubwa kama vile vita vya Badr, uhud, Hunayn na kadhalika, Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwepo mwenyewe katika uwanja wa mapambano. Katika vita vyote vikubwa na vidogo, ushindi ulipatikana zaidi kwa kupitia juhudi za Ali bin Abi Talib. Kwa mfano, katika vita vya Badr watu wa Makka waliendeleza majaribio yao ya kuvunja Uislamu. Waliendelea kuwasumbua waliokuwa wamebakia hapo Makka na pia walichukua mali na vitu vyao. Abu Jahili, kiongozi wa watu wa Makka, alituma hata barua kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) akimtisha na shambulio kutoka kwa watu wa Makka. Ilikuwa ni katika kujibu uchochezi huu ambapo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume ruhusa ya kuwapiga makafiri wa Makka. Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na takriban waislamu 300 wasioandaliwa vizuri, walikabiliana

na jeshi lililoandaliwa vyema kutoka Makka lenye takriban wapiganaji 1000. Ingawa walizidiwa idadi, Waislamu waliweza kuwashinda Makafiri katika pambano la kwanza la silaha dhidi ya maadui.

Hakeem (khj) anaendelea kueleza kuwa, siku moja jeshi la Waislamu lilikuwa likipita katika njia iliyokuwa kati ya milima. Maadui walikuwa wamejificha pande zote mbili za njia hiyo. Waislamu hawakujua mpango wa maadui, ambao walipowaona walianza kuwapiga mishale. Jambo hili liliwashtua farasi na ngamia wa Waislamu, na wapandaji walishindwa kuwaongoza kama walivyotaka. Mtume Muhammadi (S. A. W) akiwa na wafuasi kumi na sita peke yao, waliachwa katika jeshi la maadui lenye askari elfu nne. Vikosi vingine vya Waislamu vilitawanyika pande zote. Mtume Muhammadi (S. A. W) bila woga alimwongoza farasi wake kuwaelekea kwenye maadui. Wafuasi wale wachache waliokuwa na Mtume hawakujua watafanya nini, lakini mmoja wao alishuka kwenye farasi wake na akamshika farasi wa Mtume na kumwambia:

> Maadui wanakuja mbele, jeshi la Waislamu halijajitayarisha, na usalama wa Waislamu unategemea usalama wako. Tafadhali rudi nyuma ili Waislamu waweze kukusanyika na kuwa pamoja.

Mtume alimwambia asimzue farasi wake. Kisha, alisema kwa sauti ya juu:

> “Mimi ni Mtume wa Mungu. Mimi si msemaji wa uwongo. Mwache anidhuru awezaye”.

Akisema maneno haya, aliendelea mbele kwa kuwahujumu maadui. Hakuna mkono wa binadamu ulioweza kumdhuru. Mtume alimwamrisha mmoja miongoni mwa wafuasi wake kuwaita waliokuwa wamekimbia. Yeyote aliweza kumgeuza farasi wake au ngamia alirudi, na wale ambao hawakuweza kufanya hivyo walishuka na kumkimbilia Mtume Muhammadi (S. A. W).

Samson katika *Biblia*, kwa mfano, anasawiriwa kama jagina wa kivita aliyetumia utaya wa punda na kuwaua Wafilisti elfu moja (*Waamuzi* 15: 14-17). Uwezo wake wa kivita uliwawezesha Waisraeli kujikomboa kutoka kwa Wafilisti baada ya miaka mingi ya dhuluma na

unyanyasaji. Naye Yesu Kristo amesawiriwa kama jagina ambaye hakutumia nguvu za kimwili kupigana na maadui zake bali alitumia nguvu za kiroho.

### 3.2.16 Maisha ya Jagina Huwa ni Dhiki Tupu

Lengo kuu la jagina huwa ni kuikomboa jamii yake kutokana na matatizo yanayoikumba. Katika jitihada hizi, majagina hukumbana na upinzani na mateso ya kila aina kutoka kwa wapinzani wao. Mateso haya huwa ni pamoja na kuonewa, kudhulumiwa, kusingiziwa, kusalitiwa na hata kuuawa. Kawaida, ulimwenguni majagina huishi maisha ya dhiki kutoka kuzaliwa kwao mpaka kufa kwao kutokana na majaribio wanayoyapitia. Kama tulivyoona hapo mbeleni, majagina hugura makwao ili kuwaepuka maadui wanaowasaka ili kuwaua au kuwaangamiza.

Jagina huwa haoni raha hasa anapoiona jamii yake ikiteseka na anaweza kufanya lolote kadri ya uwezo wake kuhakikisha kuwa anaikomboa jamii yake kutoka mikononi mwa adui. Matarajio waliyo nayo wanajamii juu ya jagina wao, humkuza na kumtia shime zaidi jagina. Mtume Muhammadi (S. A. W) alianza kukumbana na matatizo kutoka utotoni mwake. Baba yake mzazi aliaga dunia kabla ya kuzaliwa kwake naye mama yake alifariki akiwa na umri wa miaka sita. Alipofikisha umri wa miaka minane, babu yake aliyempenda sana na ailiyekuwa msimamizi wake naye pia aliaga dunia. Hata baada ya hayo, maisha ya Mtume Muhammadi ( S. A. W) yalikumbwa na dhiki na mateso mengi, alikuwa hatulii kila mara alikimbia hapa na pale ili kuhakikisha kuwa wafuasi wake pamoja na maisha yao yako shwari.

Katika Biblia tunaelezwa kuwa Yesu Kristo alizaliwa horini mwa ng’ombe kwa sababu wazazi wake walikuwa wamesafiri Bethlehemu kwa sababu ya sensa iliyokuweko na hawangemudu kukodisha chumba cha malazi. Maisha yake vile vile yalijaa dhiki na mwishowe akayapitia mateso makubwa hadi kufa.

Aidha, maisha ya Gautama Buddha yalikuwa yamekumbwa na dhiki kubwa. Kwa mfano, baba yake alitumia mbinu zote, ili kumzuia awe nabii mkubwa (kulingana na utabiri wa awali) kama vile kumfungia ndani ya nyumba. Mwishowe, Gautama alitafuta nguo zilichokaa kama wanazovaa maskini.Usiku mmoja alivaa nguo hizo, na akaondoka na maskini waliokuwa wanatolewa ndani ya kasri usiku. Akaenda msituni, mbali na njia kuu na watu, kwa kuhofia kwamba kutofahamu mambo ya maisha ya kila siku kungefanya agundulike. Alisafiri usiku wote, akijaribu kufika mwisho wa ufalme wa baba yake. Hakuwagopa wanyama wakali kama

chui na wengine waliokuwa mawindoni usiku. Maisha yake yalikuwa yamekingwa sana kiasi kwamba hakufahamu hatari hiyo. Gautama aliendelea kutembea msituni, akijitahidi kukwepa kukutana na watu. Alikula matunda, nafaka na akanywa maji ya visima.

### 3.2.17 Majagina Huwa Hawaeleweki kwa Urahisi

Watu katika jamii mbalimbali huwa na mitazamo mbalimbali kuwahusu majagina wao. Jambo hili linakubalika haswa katika fasihi simulizi ambapo mtu ana uhuru wa kueleza masuala kwa namna ambayo anaona yanafaa. Kwa mfano, jagina huwa na maadui na wafuasi wake wanaompenda. Kila jamii kwa hivyo huchukua mielekeo tofauti kuhusiana na usawiri wa majagina. Kila jamii ina uhuru wa kumlimbikizia jagina wake sifa tele na hata kuna uwezekano wa wengine kuzitilia sifa hizo chumvi.

Lakini, maadui zake huenda wakampatia jagina sifa chache na za kumkashifu na hivyo kuwafanya majagina kuwa na mitazamo mingi ya kuwasawiri. Hivyo basi, kuwafanya kutoeleweka kwa urahisi kwa sababu kuna mitazamo mingi kuhusiana na majagina Itatulazimu kuelewa kuwa majagina watabaki katika hali ya kutoeleweka kwa urahisi jambo ambalo linakubalika katika usomi. Kwa mfano, katika *Ukawafi wa Miiraji*, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipowaelezea Makureshi kuwa alikuwa amesafiri hadi mbinguni usiku mmoja, hawakumuelewa kabisa. Aidha, katika Biblia, Yesu Kristo hakufahimika kwa urahisi. Kwa mfano, alisema kuwa angebomoa hekalu la Yerusalemu na kulijenga kwa muda wa siku tatu.

### 3.2.18 Majagina Aghalabu Huwa Hawarithiwi na Wana Wao

Kwa kawaida, jagina hata akiwa na watoto, hakuna anayerithi hadhi yake baada ya kufariki. Sababu yake ni kuwa jagina huzuka katika kipindi, muktadha au hali mahsusi katika jamii kutatua matatizo au migogoro iliyopo. Jagina hufa tu baada ya kutimiza dhamira yake. Kwa hivyo, hakuna haja ya mtu mwingine kuchukua nafasi yake.

Mtume Muhammadi ( S. A. W) alikuwa na malengo mengi ambayo yalikuwa ni pamoja na kuangamiza ibada ya masanamu na ushirikina, kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wanadamu, kukamilisha mfumo wa dini na sheria, kukomesha dhuluma, uovu, ujinga na kuanzisha mfumo wa amani na haki. Ndani ya ile miaka ishirini na mitatu ya kazi yake kama Mtume wa Mwenyezi Mungu, Muhammadi alikuwa amefanikisha malengo hayo yote. Aidha, lengo kuu la nabii Musa lilikuwa ni kuwatoa Waisraeli utumwani Misri.

### 3.2.19 Kifo cha Ajabu cha Jagina

Jagina hujua wakati wa kufa kwake, vile vile mambo ya ajabu hutokea wakati wa kifo chake. Wanajamii huwa na huzuni mwingi, kwa sababu ya mapenzi yao kwa jagina wao. Kwa nfano, Kadiri (1986: 66) ameelezea juu ya hotuba ya mwisho ya Mtume Muhammadi (S. A. W) pale Arafat. Katika hotuba hii Mtume Muhammadi (S. A. W) anasema:

> Enyi watu! Nisikilizeni ninayowafafanulia, maana sijui pengine sitakutana nanyi tena baada ya mwaka huu mahali hapa.

Kulingana na Kadiri (khj) katika kumalizia hotuba yake, aliwauliza wafuasi wake wakiulizwa na Allah kuhusu kazi yake watasema nini. Wote walijibu kwa pamoja kuwa Mtume alifikisha ujumbe wa Allah kwao. Naye Mtume Muhammadi (S. A. W) alitazama mbinguni na akasema:

> Ewe Allah! Kuwa shahidi kwamba nimetekeleza wajibu wangu.

Katika *Biblia* tunaelezwa mambo ya ajabu, ambayo yalitokea wakati wa kifo cha Yesu Kristo. Kwa mfano, giza liligubika nchi nzima kutoka saa sita hadi saa saba, na pazia la hekalu likapasuka katikati. Licha ya hayo, katika kitabu cha Waamuzi 16: 23-31 tunaelezwa vile Samsoni alivyomwomba Mungu ampe nguvu alipize kisasi kwa Wafilisti, kwa sababu walikuwa wamemtoa macho yake. Mungu alisikia maombi yake, na alishika nguzo mbili za katikati za nyumba waliokuwemo Wafilisti. Aliinama kwa nguvu zake zote, na ile nyumba ikawaangukia watu wote waliokuwa ndani yake. Tunaelezwa kuwa wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake.

### 3.2.20 Anamoishi Jagina na Kurudi Kwake Safari ya Mwisho

Mtume Muhammadi (S. A. W) ni jagina wa kidini kama tulivyotangulia kusema. Mutiso ( 1999: 39) anadai kuwa majagina wa kidini kwa kawaida huhubiri kuwa kuna ulimwengu mwingine ambao waliotenda matendo mema huenda baada ya mauko yao. Ulimwengu huu hauna matatizo ila raha na shibe. Anaendelea kusema kuwa makazi haya katika dini ya Usiva huitwa Kilaisa, katika Uislamu huitwa Peponi na katika dini ya Ukristo ni Mbinguni. Ulimwengu huu ni ruwaza ya utakatifu, utulivu, raha, uhuru, maisha ya milele, umoja, upendo, kutosheka, utangamano na kila jambo zuri. Mutiso (Khj) anasema kuwa mahali hapa ndipo makao ya miungu, Mungu na

majagina. Ni majagina miungu na Mungu ambao wanaweza kufika huko. Ni hadi siku ya mwisho tu ambapo waliofuata sheria za jagina wataweza kuingia mahali hapo.

Wajibu wa jagina, hasa wa kidini ni kutoka katika ulimwengu huu wetu na kwenda katika ulimwengu mwingine au kuja katika ulimwengu wetu au kufanya yote mawili. Hii ni safari ya mwisho ya jagina. Ndio wakati wa kuwahukumu wale wote ambao hawakufuata sheria zake duniani na kuwaongoza wale waliomtii katika kuingia makazi ya raha mustarehe. Ndio wakati wa kuwafufua wafu na kuwaadhibu vikali watenda maovu. Wakristu na Waislamu wanaamini Isa atarudi tena duniani kuikamilisha kazi alioanzisha ulimwenguni. Wakristo huamini kuwa anakaa kwenye upande wa kuume wa Mungu na kwamba wataungana naye mbinguni na waliotenda kinyume na mafundisho yake hawataenda mbinguni. Waislamu huamini kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) yu Peponi na siku ya kiama atasimama kuwaombea ili waweze kuingia Peponi.

Baada ya kuchanganua sifa za ujagina, tutashughulikia matukio ya ujagina katika utenzi huu. Sifa za ujagina zimetuongoza kuyachanganua matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*, Katika sura ya pili, tumeeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama jagina katika utenzi huu. Matukio ya ujagina yametuwezesha kumsawiri Mtume kama jagina katika dini ya Kiislamu.

### 3.3 Matukio ya Ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*

Matukio hayo ya ujagina yanadhihirika kuanzia mwanzo wa Ukawafi wa Miiraji hadi mwisho. Matukio hayo ni kama yafuatayo:

#### 3.3.1 Safari ya Mtume Muhammadi

Mtume Muhammadi (S. A. W) alisafari kutoka Makka, akafika Beti Mukaddasi, akapandishwa katika mbingu saba, akakutana na Mwenyezi Mungu na mwishowe, akarudi Makka katika usiku mmoja. Mtume alibebwa na Buraki ambaye ni mnyama mweupe, mrefu kuliko punda na mfupi kuliko nyumbu. Mnyama huyu akipanda mlima hunyoosha miguu yake ya nyuma na akiteremka mlima hunyoosha miguu yake ya mbele. Aidha, ana mbawa mbili na huonyesha ushupavu mkubwa. Safari hii haikuwa rahisi na kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu alimtuma malaika Jibrili ili awe kiongozi wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika safari hii.

Kuna matukio kadhaa ambayo yanaoonyesha kuwa safari hii haikuwa rahisi. Kwa mfano, Kabla ya kufika Beti Mukaddasi walikutana na jini likiwa na kijinga cha moto huku likimmulika Mtume Muhammadi (S. A. W). Malaika Jibrili alimwambia Mtume aseme aya fulani kutoka kwa *Kur'ani Tukufu* na aliposema likazima (ubeti 13). Baada ya kutoka mbingu ya saba Mtume Muhammadi alionyeshwa Peponi na Jehanamu. Katika Jehanamu, aliuuona moto mkali kisha akaona adhabu kali iliyokuwa ikipatiwa wenye dhambi na hakukubaliwa kuwaokoa. Hakuweza kuvumilia kuyaona mateso hayo na kwa sababu hiyo akazirai na kupoteza fahamu. Mtunzi anaeleza:

> Jiburilu thamma kamudhumu akafahama
> (ubeti 72).

Si jambo rahisi kukutana na Mwenyezi Mungu na kuzungumza naye. Mtume Muhammadi (S. A. W) anapofika mbele ya Mwenyezi Mungu, alimsalimu kwa taadhima kubwa naye akamjibu salamu zake. Katika ubeti wa 78 mtunzi anasema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipomwona Mungu wake macho kwa macho alishindwa kuzungumza tena na akapiga magoti, lakini Mwanyezi Mungu akamwambia aombe alichotaka na angepewa kikiwa kamili.

Malaika Jibrili alimwongoza Mtume tena katika safari ya kurudi mpaka Makka. Tumeonelea kuwa kama safari hii ingekuwa rahisi, Mwenyezi Mungu hangemtuma malaika huyu amwongoze Mtume Muhammadi (S. A. W) mpaka kwake na katika safari ya kurudi tena Makka.

### 3.3.2 Kutakaswa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Mwenyezi Mungu alimtuma malaika Jibrili amchukue Mtume Muhammadi (S. A. W) ampeleke kwake. Kabla ya safari hii kuanza Mtume Muhammadi alitakaswa na malaika Jibrili alimpasua kifua chake kisha akamtoa uovu wote uliokuwa ndani yake. Mwishowe alimshona kama kwamba hakumpasua. Mtunzi anasema:

> Alipoamuka muombezi wakapasua
> Kifua na nyongo zote ghashi wakazitoa (ubeti 5).

Ni dhahiri kuwa Mtume alipasuliwa kifua akiwa hayuko usingizini, jambo ambalo linadhihirisha kuwa Mtume Muhammadi alikuwa na ujasiri mwingi. Mtunzi hajaeleza kama Mtume alikuwa anahisi uchungu au la. Hata kama hakuwa anahisi uchungu aliyaona yote na ni tukio la ujagina.

### 3.3.3 Kulizima Jini

Katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, walikutana na jini. Jini hilo lilikuwa na kijinga cha moto huku likmmulika Mtume Muhammadi (S. A. W). Mtume hakuogopa hata kidogo. Malaika Jibrili alimwambia Mtume akariri aya fulani kutoka kwa *Kur'ani Tukufu* na aseme sala kwa Mwenyezi Mungu. Mtume alifuata ushauri wa malaika Jibrili na mara moja lile jini likazima. Tunaonelea kuwa jini lile lilikuwa katika hali ya moto na kwa sababu hiyo mtunzi anasema:

> T'umwa akasoma, 'ifuriti likazizima (ubeti 13)

Waislamu huamini kuwa aya ambayo Mtume Muhammadi (S. A. W) alikariri kutoka kwa *kurani tukufu* huyakinga makao yao kutokana na moto wa aina yote.

### 3.3.4 Kuvumilia Kutazama Mateso ya Watenda Maovu

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* anasema kuwa katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa mateso makali tofauti tofauti ambayo watenda maovu mbalimbali walikuwa wakiyapitia. Baadhi ya mates hayo ni pamoja na:

Watu wakipondaponda vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Malaika Jibrili alimwambia Mtume kuwa wale walikuwa wazembe wa kusali sala za asubuhi na sala zao hazikuwa zinakamilika (ubeti 18). Katika ubeti 19 tunaelezwa:

> Kisha wakaona watu wawi mbele na nyuma,
> Wana vitambaa vya ziraka wala zakuma.
> Jiburilu kamba: watu sao si watu wema
> Hawatoi zaka, mali yao Jahannama.

Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa wazinifu ambao walikuwa wakiacha nyama nzuri iliyonona vizuri na kwenda kula nyama duni iliyooza yenye uvundo (ubeti 20) Mtume alionyeshwa watu wakikatwa ndimi zao kwa makasi huku zikirejea tena, malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) kuwa wale ni waongo na hawamtii Mwenyezi Mungu. Isitoshe, Mtume alionyeshwa watu wabaya wakiparura nyuso zao kwa kucha za shaba, hawa ni wale wasiotenda haki na siku ya ufufuko nyuso zao hazitakuwa na nyama. Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa. Mtume huyu ni jagina kwani mtu wa kawaida hawezi kuvumilia kuyatazama matukio kama hayo.

### 3.3.5 Kuwanyamazia Myahudi na Mkristo

Katika ubeti wa 32, mtunzi anasema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) na malaika Jibrili walisikia mtu akiitana lakini Mtume hakuitika. Malaika Jibrili alimwambia kuwa yule alikuwa Myahudi na kama angeitika umati wake ungekuwa kama wa yule Myahudi. Aidha, katika ubeti wa 33 mtunzi anaeleza:

> Tena kasikia mlingani jiha shimali
> T'umwa kanyamaa asitike yake makali.
> Jiburilu kamba: ni Nasara muja dhalali.
> Ataka poteza umatio tariki njema.

Kwa kutowazungumzia watu hawa Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyesha jagina wake na alidhihirisha alikuwa mwenye akili pevu. Kwa hivyo, akawa mfano mwema wa kuigwa na wafuasi wote wa dini ya Kiislamu. Waislamu wote huamini kuwa wanapaswa kufuata njia nyoofu inayoelekea kwa Mwenyezi Mungu na peponi bila kuwasikiliza wayahudi na wakristo ambao ni watumwa wa dhambi na wamefuata njia ambayo haifai.

### 3.3.6 Kuwa Imamu katika Beti Mukaddasi

Kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, imamu ni mtu aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu na kila neno na kitendo cha imamu ni katika kumtii yeye, vita vyake na amani yake ni kioo cha amali chenye kufaa na msimamo wake ndio mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Mitume wengine wa awali, kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, wanakusanyika katika Beti Mukaddasi si tu kusali na Mtume Muhammadi (S. A. W) bali pia Mtume awaongoze katika sala. Inadhihirika kuwa hata malaika Jibrili anaongozwa katika sala na Mtume Muhammadi (S. A. W). Kwa kukubali Mtume awe imamu, mitume wa awali wana heshima kuu kwake. Mtume Muhammadi (S. A. W) ni kiongozi jasiri wa dini ya Kiislamu na anakubalika na wafuasi wote wa dini hii. Katika ubeti wa 39 mtunzi anasema:

> Jiburilu kamba: tangulia, ndiwe imamu;
> Mitume i nyuma yako, mbele utakadamu;
> Saada ni yako na heshima na taadhimu,
> Ndiwe muteule muombezi wa wote wema.

### 3.3.7 Uchaguzi wa Dini ya Kiislamu

Baada ya kusali katika Beti Mukaddasi na kabla ya Miiraji kuteremshwa kutoka mbinguni, Mtume Muhammadi (S. A. W) alihisi kiu. (Waislamu huamini kuwa Mwenyezi Mungu ndiye

aliyemfanya Mtume ahisi kiu ili amjaribu). Mtume aliletewa vyombo viwili na kila kimoja kikiwa kimejazwa kwa kinywaji cha aina yake. Cha kwanza kilikuwa kimejazwa kwa maji na maziwa na cha pili kilijazwa kwa mvinyo na asali tamu. Malaika Jibrili alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) achague kinywaji kati ya hivyo viwili. Mtume kwa ujasiri alichagua maziwa, akainua kile chombo na kuyanywa. Mtunzi anaeleza:

Ikashika nyota muungamo, zikaja zombo
Kya ziwa na maji na ‘asali na tamu tembo
Kahitari ziwa muombezi, kasibu ombo
Ombo wa Imani taufiki yake Karima.

Jambo hili linadhihirisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na akili pevu kwa sababu kwa kuchagua maziwa, alichagua dini ya Islamu. Maziwa yalikuwa ishara ya dini ya kweli ambayo ni Kiislamu ilhali kinywaji cha mvinyo kilikuwa ishara ya maovu. Kupevuka kwa akili ni mojawapo ya sifa za ujagina ambazo tumezichanganua mwanzoni mwa sura hii.

### 3.3.8 Kukutana na Mitume wa Awali

Kutoka Beti Mukaddasi Mtume Muhammadi alipandishwa mbinguni kwa kutumia Miiraji ambayo ilikuwa imepambwa kweli kweli. Malaika Jibrili alikuwa anabisha kwa niaba ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Alikutana na Adamu, Isa na Yahya, Yusufu, Idiris, Haruni, Musa na Iburahimu. Mitume wote walimkaribisha Mtume Muhammadi (S. A. W) na kuukubali utume wake. Kwa mfano, tunaelezwa:

Wakaitikiwa: marahaba mwenye ‘adhama.
Uwene sadiki Yuusufu na sura njema;
Akanza salamu muungamo, ndio heshima.
Akakurubisha akaweka mahala pema (ubeti 48).

### 3.3.9 Kuyaona Maajabu ya Mbinguni

Mtume Muhammadi (S. A. W) alipotoka katika mbingu ya saba, aliwaona watu wengi weupe kama karatasi na wengine wenye madoadoa. Malaika Jibrili alimwambia kuwa waliokuwa weupe kama karatasi hawakuwa na dhambi na roho zao ziliingia peponi bila kupata adhabu yoyote na wenye madoadoa ni wale walitubu dhambi zao wakawa wema. Alipita na akaona nyumba ambayo ilikuwa imejengwa chini ya pepo aliingia ndani pamoja na malaika Jibrili na kusali. Aliwaona malaika 700,000 na idadi hii iliingia katika nyumba hii kila siku. Mwadhini

wao ni malaika Jibrili na imamu ni Mikaili. Alipita akielekea kwenye kiti cha enzi, hatua ya nane ya daraja la utume mahali penye mti wa ajabu ambao ni mwisho wa vitu vyote.

Aliendelea kuonyeshwa maajabu mengi yasiyo na mwisho. Chini ya mti huo aliiona mito minne iliyojaa maziwa, asali na divai, matunda ya mti huo ni matamu sana. Aidha, matawi yake hufunika mataifa yote. Kisha akauona mto wake mwenyewe, zawadi kutoka kwa Mungu uitwao Kauthari. Waliufuata mpaka wakafika nyumba njema ambako waliwaona viumbe ambao hawajawahi kuwaona au kusikia hadithi kuwahusu. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliona peponi na hakuwa ameuona mfano wake. Kulikuwa kumepambwa vizuri mno. Alipotoka nje, alionyeshwa moto mkali aliona adhabu kali iliyokuwa ikipatiwa wenye dhambi.

### 3.3.10 Mazungumzo ya Mtume Muhammadi na Mwenyezi Mungu

Malaika Jibrili hakupita daraja la nane kwani kila kiumbe cha Mwenyezi Mungu kina sehemu yake mbinguni. Ule ndio ulikuwa mwisho wake. Kwa hivyo, kutoka hapa Mtume Muhammadi (S. A. W) aliendelea na safari akiwa peke yake. Tunaelezwa:

> Kisha akakia rafurafu ikenda naye (ubeti 76).

Mtume Muhammadi (S. A. W) alipita vikwazo vyote mpaka akafika alipokuwa Mwenyezi Mungu. Alimwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake na akaonyesha heshima kubwa kwa kupiga magoti hadi Mungu alimwambia aitishe alichotaka na atapewa kikiwa kamili. Mtume Muhammadi (S. A. W) alipopatiwa nafasi hiyo alizungumza na Mwenyezi Mungu kwa ujasiri mwingi. Alimwambia Mwenyezi Mungu kuwa alikuwa Mwendani wa Iburahimu na akasaili apate kujua sehemu yake ilikuwa gani. Mwenyezi Mungu alimhakikishia kwamba alikuwa rafiki yake zaidi ya mitume wengine wote. Mtume Muhammadi (S. A. W) hakukomea hapo, alimwambia Mwenyezi Mungu kuwa alimpatia Daudi zaburi na Suleimani uwezo juu ya majini. Mwenyezi alimwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) yeye ndiye wa kwanza na ndiye wa mwisho na jina lake litatajwa pamoja na la Mwenyezi Mungu kila wakati.

Zaidi ya hayo, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliendelea kunena na Mwenyezi Mungu na kumwambia:

> Na kamaye ‘Isa akipoza kulla kilema,
> Na kuwafufua wafieo yake kalima (ubeti 81)

Naye Mwenyezi Mungu alimwambia kuwa alikuwa amempatia uwezo wa kuwafufua watu wengi na umati wake ulikuwa bora kuliko umati mwingine wowote. Kisha akamwambia kuwa siku ya kiama atasimama awe mwombezi wa umati wake, na atawaona makafiri wote ambao hawakufuata ushauri wake na wa mitume wengine wakiingia Jehanamu. Mwenyezi Mungu alimwambia kuwa uwezo aliokuwa amempatia hakuna mwingine alikuwa nao na mwishowe Mtume akapatiwa sala tano awapelekee wafuasi wake ambazo walipaswa kuzisali kwa ukamilifu kila siku.

### 3.3.11 Kurudi Mara Kadha kwa Mwenyezi Mungu

Mtume Muhammadi (S. A. W) alipotoka mbele ya Mwenyezi Mungu, aliienda alipokuwa malaika Jibrili na wakaendelea na safari mpaka alipokuwa Musa. Mtume alimwelezea Musa yote yaliyotendeka baina yake na Mwenyezi Mungu na akamalizia kwa kumwambia kuwa alikuwa amekabidhiwa sala hamsini aupelekee umati wake. Musa alimwambia kuwa umati wake haungeweza kusali sala hamsini kila siku, itakuwa kazi ngumu sana kwao. Musa alimshauri arudi tena kwa Mwenyezi Mungu amwombe ampunguzie sala hizo. Mtume Muhammadi alirejea tena mbele ya Mwenyezi Mungu na kumsihi ampunguzie sala hizo na Mungu akazipunguza kwa tano zikwa arubaini na tano.

Alipofika kwa Musa akamwambia kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa amempunguzia sala hizo kwa tano, alimwambia arudi tena mbele ya Mwenyezi Mungu ili zipunguzwe zaidi. Ikawa ni kwenda na kurudi mbele ya Mwenyezi Mungu mpaka sala hizo zikapunguzwa zikawa tano lakini Mwenyezi Mungu akamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W):

> Kwani aswiliye sala tano hatamukeni;
> Wapawa thawabu sala kumi twaa yakini;
> Ndio hesabu-ye sala tano kwa hamusini;
> Halitabadali neno lake Mola kadima (ubeti 89).

### 3.3.12 Kutonyamaza Aiporudi Makka

Mtume Muhammadi (S. A. W) alipofika Makka kutoka safarini hii ambayo aliienda kwa usiku mmoja hakuweza kunyamaza hata ingawa alikuwa na wasiwasi mwingi kwa sababu alijua Makureshi hawangemwamini. Abu Jahili alipomsaili kwa kumkejeli kuhusu hali yake, Mtume alimwambia kwa ujasiri kuwa usiku huo alikuwa amesafiri hadi mbinguni na akamwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Isitoshe, akamwambia kuwa alikuwa

amezungumza na Mwenyezi Mungu na akamwambia mambo ya kuhifadhi moyoni. Abu Jahili hakuziamini habari za Mtume Muhammadi (S. A. W) na mara moja alikusanya Makureshi wote wasikie habari hizo. Mtume aliwaelezea habari hizo kama alivyokuwa amemwelezea Abu Jahili. Tunaelezwa:

> Alipoweleza habariye yote kamili
> Pakawa kiteko na dhihaka na kumuzoma (ubeti 100).

Walimwambia Mtume kuwa habari zake zilikuwa za uongo na haingewezekana yeye asafiri hadi mbinguni usiku mmoja na kumwona Mwenyezi Mungu. Hawakukomea hapo, walimwambia kuwa habari za mbinguni pamoja na kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu hawakuwa wanazijua lakini walikuwa wanazifahamu sifa za Beti Mukaddasi, basi wakamwambia Mtume Muhammadi (S. A. W) awaelezee sifa za Msikiti huo. Mtume alianza kutafakari angefanya nini kwa sababu hakuwa anazikumbuka vizuri. Mwenyezi Mungu alimwamuru malaika Jibrili amdhihirishie sifa hizo machoni pake. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaelezea sifa hizo kwa ujasiri mwingi mpaka wakasema:

> …………………………..ai Amini,
> Ndizo swifa zake umeziye kuzibaini (ubeti 105).

Aidha, walimwambia awaelezee wakati watu wao waliokuwa safarini wangefika nyumbani. Mtume aliwajibu bila kuogopa kuwa watu wao walikuwa bado mbali na wangewasili siku ya tano kutoka siku hiyo lakini mtunzi anasema:

> Yalipowadia siyo siku wakangojea
> Wasione kuya hatta yua budi kuzama (ubeti10).

Mtume Muhammadi (S. A. W) alisali kwa Mwenyezi Mungu alisimamishe jua mahali pake ili aweze kutimiza ahadi yake kwa Makureshi. Mwenyezi Mungu alisikia sala ya Mtume wake. Jua lilisimama hadi pale watu hao walifika wote. Baada ya hayo yote, Makureshi hawakumwamini Mtume Muhammadi (S. A. W) na kuapa kuwa hawangemfuata awaache masanamu yao.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumezichanganua sifa za ujagina kwa jumla na tukaona kuwa si zote zinadhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji* kwa sababu utenzi huu hauhusu maisha yote ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Majagina wa kidini hutumia nguvu ambazo si za kawaida na wafuasi wao huamini kuwa nguvu hizo wanapatiwa na Mwenyezi Mungu. Majagina wa kidini wanapendwa na wafuasi wao kiasi cha kuchukiwa na walio mamlakani hadi wanapangiwa njama za kuuawa. Majagina ukumbwa na masaibu mengi maishani mwao wakijaribu kadri ya uwezo wao kuikomboa jamii kutokana na dhiki ambazo huwa zimekithiri na kwa sababu hiyo, majagina huwa hodari katika vita. Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa katika uwanja wa vita vikubwa ambavyo wafuasi wake walipigana dhidi ya maadui. Tumeona kuwa maisha ya jagina huwa hayaeleweki kwa urahisi, kwa kuwa wanajamii huwa na mitazamo tofauti kuwahusu. Mashujaa huwa wanayaathiri maisha ya wanajamii wao kila wakati.

Aidha, katika sura hii tumeyashughulikia matukio ya ujagina yanayojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji*. Matukio ambayo tumeyashughulikia yamemzingira Mtume Muhammadi (S. A.W) ambaye ni jagina wa dini ya Kiislamu. Mtume huyu alikuwa amepewa uwezo wa kipekee na Mwenyezi Mungu na kwa sababu hiyo, alienda safari ndefu kwa muda wa usiku mmoja huku akiwa amebebwa na mnyama wa ajabu aitwaye Buraki.  Malaika Jibrili aliongoza safari hiyo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alilizima jini kwa kusoma aya fulani kutoka kwa *Kur'ani Tukufu*. Isitoshe, anawaongoza mitume wote katika sala ndani ya Beti Mukaddasi. Anapofika mbele ya Mwenyezi Mungu, anampatia heshima ya hali ya juu, na kuzungumza naye kwa ujasiri. Musa alipomshauri arudi mbele ya Mwenyezi Mungu ili apunguziwe sala hamsini, alifanya hivyo mara kadhaa hadi zikapunguzwa hadi tano. Alipofika Makka hakunyamaza aliwaelezea Makureshi kuhusu safari yake ya mbimguni katika usiku mmoja.

# SURA YA NNE

## MAFUNZO YA MTUME MUHAMMADI KWA WAFUASI WAKE

### 4.1 Utangulizi

Baada ya kutalii usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) pamoja na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*, itatubidi tupige hatua kwa kuangazia mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake kama yanavyodhihirika katika utenzi huu. Kama tulivyosema katika sura ya pili, Mtume Muhammadi (S. A. W) amesawiriwa kama jagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Matendo yote ya Mtume Muhammadi (S. A. W) maishani mwake yalikuwa ni mafunzo kwa wafuasi wake. Kwa hivyo, hata safari yake ya kimuujiza mbinguni inafunza waumini wa dini Kiislamu masuala mengi. Muumini akiyazingatia mafunzo hayo, mwishowe ataishi maisha ya furaha Peponi. Aidha, akienda kinyume na mafunzo hayo, mahali pake ni Jehanamu penye matatizo mengi. Ili kuyachanganua mafunzo hayo, kwanza tutaangalia kwa kifupi tu safari hiyo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) mbinguni.

### 4.2 Safari ya Miiraji

Mtume Muhammadi (S. A. W) aliitwa na Mwenyezi Mungu aende kwake. Malaika Jibrili aliteremka kutoka mbinguni ili amwongoze Mtume katika safari hii. Kabla ya safari kuanza, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipasuliwa kifua na kutolewa maovu yote yaliyokuwa ndani yake. Kisha Jibrili akamshona kama kwamba hakumpasua. Katika safari hii Mtume Muhammadi (S. A. W) alibebwa na Buraki. Mtunzi anaeleza kuwa, Mtume alianza kumwomba Mwenyezi Mungu mara tu walipoanza safari. Aidha, Malaika Jibrili alimwambia ashuke mara tatu, kabla ya kufika Beti Mukaddasi na asali. Alisali walipofika Madina, mlima Sinai na Betilahamu.

Katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, Mtume alionyeshwa mambo mengi. Kwa mfano, watu wakipanda na kuvuna muda mfupi baadaye. Malaika Jibrili alimweleza kuwa hao ni wale waliokufa katika vita vitakatifu. Alionyeshwa watu waliokuwa wamevalia nguo za viraka wakila sumu. Alielezwa kuwa hao ni wale hawatoi zakat na mali yao ni ya Jehanamu. Aidha, alionyeshwa wazinifu, mbele yao kulikuwa na nyama nzuri iliyonona vizuri na pembeni mwao kulikuwa na nyama duni iliyooza yenye uvundo. Wakawa wanakula ile nyama duni iliyooza yenye uvundo na wanaiacha ile nyama nzuri. Vile vile, alionyeshwa watu wakikatwa ndimi zao huku zikirejea tena. Akaelezwa kuwa hao ni waongo na hawamtii Mwenyezi Mungu.

Licha ya hayo, alionyeshwa mto wa damu uliokuwa na watu wakila sumu. Alielezwa kuwa hao ni watu waliokula chakula ambacho kimekatazwa. Isitoshe, waliona watu wakipapura nyuso kwa makucha yao sufuri. Malaika Jibrili akamwambia hao ni watu dhalimu, na Siku ya Kiama nyuso zao hazitakuwa na nyama. Walipoendelea na safari walikutana na jini likiwa na kijinga cha moto. Lilikuwa linammulika Mtume Muhammadi (S. A. W). Malaika Jibrili akamwambia Mtume akariri aya kutoka kwa *Kurani Tukufu* na jini likazima.

Walipofika Beti Mukaddasi, mitume wote wa awali walikusanyika katika Msikiti Mtakatifu kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Malaika Jibrili aliadhini na akamchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) awe imamu. Malaika Jibrili alimwambia kuwa yuko mbele na mitume wengine wote wako nyuma yake. Baadaye, Mtume Muhammadi (S. A. W) alihisi kiu na akaletewa vyombo viwili. Kimoja kikiwa kimejazwa maziwa na kingine mvinyo. Mtume alichagua maziwa. Kwa kufanya hivyo, alichagua dini ya Kiislamu.

Miiraji iliyokuwa imepambwa vizuri iliteremshwa kutoka mbinguni. Mtume alipandishwa hadi mbingu ya kwanza hadi ya saba. Alikutana na mitume wengine wa awali kama vile Adamu, Musa, Isa na Yahya, Yusufu na Ibrahimu. Mitume hawa walimkaribisha, wakamsalimu na kuukubali utume wake. Baadaye, alionyeshwa Pepo na Jehanamu. Alionyehswa maajabu ya mbinguni. Kwa mfano, watu weupe kama karatasi ambao hawakutenda dhambi. Pia, aliwaona watu wenye madoadoa, na malaika Jibrili akamweleza kuwa hao ni wale walitenda dhambi na mwishowe wakatubu. Walipofika daraja la nane malaika Jibrili alifika mwisho wake. Mtume Muhammadi (S. A. W) alibebwa na rafurafu, akapita vizuizi vyote na akapelekwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mtume Muhammadi (S. A. W) alimsalimu Mwenyezi Mungu kwa taadhima kubwa naye akamjibu salamu zake na kumwambia kuwa yeye ni mteule ambaye amewekwa mahali pema. Mtume alipomwona Mwenyezi Mungu macho kwa macho alishindwa kunena na akapiga magoti. Mungu alimwambia aombe alichotaka na angepewa kikiwa kamili. Mwenyezi Mungu alithibitisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa mtume wake wa mwisho ambaye amemchagua kuwaongoza watu wote kuelekea njia ya utakatifu. Aidha, Mwenyezi Mungu anamwambia kuwa Siku ya Kiama atakuwa muombezi wa umati wake, wema na waovu. Pia, Mungu anamhakikishia kuwa umati wake ulikuwa bora kuliko umati mwingine wowote.

Mwishowe, Mwenyezi Mungu akampatia Mtume Muhammadi (S. A. W) sala hamsini awapelekee wafuasi wake. Alipofika alipokuwa Musa, alimwelezea yote yaliyojiri kati yake na Mwenyezi Mungu. Musa alimshauri arudi mbele ya Mwenyezi Mungu na amwombe ampunguzie sala hizo kwa sababu ungekuwa mzigo mkubwa kwa umati wake kusali sala hamsini kila siku. Alipofika mbele ya Mwenyezi mungu, alimsihi ampunguzie sala hizo . Naye Mungu alimpunguzia kwa tano. Musa alimwambia arejee tena mbele ya Mwenyezi Mungu amsihi azipunguze sala hizo tena. Ikawa ni kwenda na kurudi hadi Mwenyezi Mungu akazipunguza zikawa tano.

Mtume Muhammadi (S. A. W) na malaika Jibrili walishuka kutoka mbinguni usiku huo huo na kuwasili Beti Mukaddasi. Mtume alimpanda Buraki na wakasafiri hadi Makka. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaelezea Makureshi habari kuhusu safari yake ya mbinguni, walizikataa na wakamwambia awaelezee sifa za Beti Mukaddasi kwa sababu walikuwa wanazijua. Mwenyezi Mungu alimdhihirishia sifa hizo zote kupitia kwa malaika Jibrili. Isitoshe, walimwambia awaelezee wakati msafara wa kibiashara aliokuwa amekutana nao ungewasili. Akawaambia wakati ungewasili. Siku ilipofika, ulitimia wakati wa jioni na wafanyabiashara hawakuwa wamewasili. Mtume Muhammadi (S. A. W) alimwomba Mwenyezi Mungu alisimamishe jua ili ahadi yake itimie. Jua lilisimama hadi msafara huo ulipofika. Hayo hayakuwafanya wamwamini Mtume Muhammadi (S. A. W).

Utenzi huu una mafunzo yafuatayo:

### 4.2.1 Utakatifu wa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza, Mtume Muhammadi (S. A. W) ni Mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu. Aidha, alichaguliwa kuwaongoza wanadamu wote kuelekea njia inayofaa. Mtume Muhammadi (S. A. W) hana dhambi. Kabla ya kuanza safari, malaika Jibrili alimpasua kifua chake na kuyatoa maovu yote yaliyokuwa ndani yake. Mtume Muhammadi (S. A. W) alitakaswa kwa kutolewa nyongo ndani yake.  Katika sura ya tatu, tumeeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alitokana na kabila la Kureshi. Aidha, alizuka katika mazingira ya Kihistoria ambayo yalikuwa na maovu mengi. Maovu hayo yalidhihirika katika asasi zote za jamii kama vile dini na uchumi. Mwenyezi Mungu ni Mtakatifu, na alimwita Mtume Muhammadi (S. A. W) aende kwake. Kwa hivyo, sharti Mtume Muhammadi (S. A. W) angetakaswa kabla ya kwenda mbele yake.

Mwanzoni, Buraki alisita kumbeba Mtume Muhammadi(S. A. W) akisema:

> …….mkonowe ushishie muwi sanamu.
> Ndipo k'akataa kunishika yake jisimu (ubeti 7).

Malaika Jibrili alimwambia kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) hana dhambi, na ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Baadaye, Buraki alikubali kumbeba na akamwomba amuweke pahali pazuri Peponi. Kupitia tukio hili wafuasi wa dini ya Kiislamu wanafunzwa kuwa Mtume wao ni Mtakatifu.

### 4.2.2 Kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, lengo kuu la safari ya Miiraji lilikuwa ni kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W). Katika *Ukawafi wa Miiraji*, kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) kunadhihirika kupitia kwa matukio mawili. Kwanza, alisafiri hadi alipokuwa Mwenyezi Mungu. Mtunzi wa utenzi huu anaeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alimwona Mwenyezi Mungu kwa kwa macho yake mwenyewe. Tukio hili ndilo kilele cha safari hii ya Miiraji. Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) alizungumza na Mwenyezi Mungu. Kwa mfano katika ubeti wa 80 tunaelezwa:

> Kamba: tumupele Daaudi yake zaburi,
> Na Sulaimani kumiliki jinni na tweri;
> Nawe ni awali ya Mitume, ndiwe aheri
> Nidhukuriwapo na isimu yako i nyuma.

Pili, walipofika katika Beti Mukaddasi, mitume wengine wote walikusanyika katika msikiti huo. Malaika Jibrili aliadhini lakini hawakuwa na imamu. Malaika Jibrili alimchagua Mtume Muhammadi awe imamu akisema:

> Mitume i nyuma yako, mbele utakadamu (ubeti 39).

### 4.2.3 Nafasi ya Mtume Muhammadi

Mtume Muhammadi (S. A. W) amepewa nafasi kubwa miongoni mwa mitume wengine wote. Kama tulivyoeleza hapo awali, Mitume wengine wote walikusanyika katika Beti Mukaddasi kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Malaika Jibrili aliadhini, halafu akamchagua Mtume Muhammadi (S. A. W) awaongoze katika sala. Aidha, malaika Jibrili alimwongoza Mtume Muhammadi (S. A. W) katika safari hii. Alimweleza maana ya matukio yote ya ajabu alikuwa akiyaona. Jambo hili halimaanishi kuwa malaika Jibrili alikuwa na nafasi kubwa kuliko Mtume

Muhammadi (S. A. W). Katika Beti Mukaddasi, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliongoza mitume wengine pamoja na malaika Jibrili katika sala. Isitoshe, walipofika daraja la nane, malaika Jibrili alifika mwisho wake. Hakuruhusiwa kupita hapo. Malaika Jibrili anasema:

> …….siwezi kwenda mbele hatta shibiri,
> Sapa ndipo pangu, Muombezi katakadama (ubeti 73).

Mtume Muhammadi (S. A. W) aliendelea na safari mpaka mbele ya Mwenyezi Mungu. Licha ya hayo, malaika Jibrili alielewa nafasi kubwa ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Katika ubeti wa 75 Jibrili anamwambia:

> ……. Haja yangu niitakayo,
> Siku ya swirata niwe kinga ya umatiyo
> Ninyoshe mabawa yawe kinga ya zao nyayo,
> Usiwapateo moto harri ya Jahannama.

### 4.2.4 Mitume katika Dini ya Kiislamu

Mtume ni mtu anayeaminiwa kuwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mtume huwafundisha wanadamu mienendo inayompendeza Mungu. Majina ya mitume katika dini ya Kiislamu yanadhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Mtume Muhammadi (S. A. W) alikutana na mitume wa awali kuanzia mbingu ya kwanza hadi ya saba. Mitume hao ni Adamu, Isa na Yahya,Yusuf, Idiris, Nabii Haruni, Musa na Iburahimu.

Aidha, katika mazungumzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) na Mwenyezi Mungu baadhi ya uwezo uliopewa mitume hawa na Mwenyezi Mungu unadhihirishiwa wafuasi wa dini ya Kiislamu. Kwa mfano, Daudi alipewa zaburi na Sulaimani uwezo wa kumiliki jinni. Aidha, Iburahimu alikuwa rafikiye Mwenyezi Mungu. Isitoshe, tunaelezwa:

> Na kamaye ‘Isa akipoza kulla kilema,
> Na kuwafufua wafieo yake kalima (ubeti 81).

### 4.2.5 Adhabu za Watenda Dhambi

Katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa adhabu za watenda maovu. Mtume alionyeshwa watu wakipondaponda vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Malaika Jibrili akamwambia kuwa hao ni wazembe wa kusali sala

za asubuhi na sala zao hazikamiliki. Pia, alionyeshwa watu ambao hawakuwa na mbele wala nyuma.

Walikuwa wamevalia nguo zenye viraka huku wakila zakum. Mtume Muhammadi (S. A. W) alielezwa kuwa hao ni wale hawatoi zakat na mali yao ni ya Jehannamu. Aidha, Mtume alionyeshwa wazinifu wakila nyama mbichi, wakiwa wameiacha nyama nzuri. Isitoshe, waliona mto wa damu, ambao ulikuwa na watu ndani wakila sumu. Jibrili alimweleza kuwa watu hao walikula chakula ambazo kimekatazwa. Akaendelea kumweleza kuwa hiyo ndiyo itakuwa zawadi yao Siku ya Kiama. Vile vile, Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa watu ambao walikuwa wakikatwa ndimi zao kwa makasi, huku zikirejea tena baada ya muda mfupi. Mtume akaelezwa kuwa hao ni waongo. Waongo husema mambo ambayo ni kinyume na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Katika ubeti wa 23 mtunzi anaeleza:

Kisha wakenenda wakaona mutu dhalili
Hutaka jitweka haiwezi tweka thakili,
Kuzidia tena kuongeza haihimili;
Jiburilu kamba: ni amana katika dhima.

**4.2.6 Miji Mitakatifu**

Makka ni Mji wa kwanza mtakatifu kulingana na imani ya dini ya Kiislamu. Kama tulivyosema katika sura ya tatu, Mtume Muhammadi alizaliwa Makka. Aidha, Makka ni mji ambao Mtume Muhammadi (S. A. W) alikaa alipoanza kupokea aya za *Kur'ani Tukufu*. Katika Makka kuna jengo la Kaaba linaloaminiwa ni msikiti uliojengwa na Adamu, na ukatengenezwa upya na Ibrahimu. Isitoshe, katika sura ya tatu, tulieleza vile Mtume Muhammadi (S. A. W) aliweka jiwe juu ya Kaaba. Jiwe hilo liko mahali hapo mpaka leo. Kila mwaka mamilioni ya Waislamu wanakwenda Makka kwa hiji. Hiji ya kwenda Makka ni moja kati ya nguzo tano za dini ya Kiislamu.

Mji wa pili ambao ni mtakatifu katika dini hii ni Madina. Mtume Muhammadi (S. A. W) aliambiwa na malaika Jibrili ashuke kutoka kwa Buraki, na asali walipofika Madina. Madina ina nafasi muhimu katika imani ya dini Kiislamu. Kama tulivyoeleza katika sura ya tatu, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliguria Madina kutoka Makka kwa sababu ya upinzani dhidi yake. Alipokelewa vizuri Madina, na akawa kiongozi wa kiroho pamoja na kisiasa. Madina kuna msikiti wa Mtume penye kaburi lake. Kaburi lake liko mahali panapoaminiwa palikuwa na

nyumba yake, alikoaga dunia. Kando na kaburi la Mtume Muhammadi (S. A. W), kuna makaburi ya maswahaba wake.

Mji wa tatu ni Yerusalemu. Msikiti mtakatifu umo katika mji huu. Kama vile tumesema hapo awali, mitume wote walikusanyika katika Beti Mukaddasi, na Mtume Muhammadi (S. A. W) akawaongoza katika sala. Aidha, aliteremshiwa miiraji aliyoitumia kupandia mbinguni katika mji wa Yerusalemu. Isitoshe, hapo ndipo alitua alipotoka mbinguni. Vile vile, ni katika mji huu mtume alihisi kiu, na akaletewa vyombo viwili kimoja kikiwa na maziwa na kingine kikiwa na mvinyo. Mtume alichagua kinywaji cha maziwa ambacho kiliwakilisha dini ya Kiislamu. Yerusalemu huaminiwa kuwa ni mahali pa miiraji ya Mtume Muhammadi (S. A. W).

### 4.2.7 Tofauti kati ya Dini ya Kiislamu na Dini Zingine

Hapo awali, tumesema kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipohisi kiu, aliletewa vinywaji vya aina mbili, maziwa na mvinyo. Mtume alichagua kinywaji cha maziwa ambacho kilikuwa ishara ya dini ya Kiislamu. Kinywaji cha mvinyo kilikuwa ishara ya dini ya Wakristo na Wayahudi. Wafuasi wa Mtume Muhammadi (S. A. W) huamini kuwa Wakristo na Wayahudi hutumia fedha zao katika unywaji wa mvinyo. Aidha, huamini kuwa mvinyo ni " mama wa maasi na maovu" na chanzo cha matendo ya kikatili.

Isitoshe, katika ubeti wa 32, walisikia mtu akiwaita. Mtume alinyamaza. Malaika Jibrili akamwambia kuwa yule alikuwa Myahudi. Aliendelea kumwambia kuwa kama angeitika umati wake ungekuwa kama wa Myahudi. Vile vile, katika ubeti wa 33 tunaelezwa:

> Tena kasikia mlingani jiha shimali
> T'umwa kanyamaa asitike yake makali.
> Jiburilu kamba: ni Nasara muja dhalali.
> Ataka poteza umatio tariki njema.

Waumini wa dini ya Kiislamu wanapaswa waige mfano wa Mtume Muhammadi (S. A. W). Wafuate njia nyoofu ambayo inaelekea kwa Mwenyezi Mungu na Peponi. Hawapaswi kuwasikiliza Wayahudi na Wakristo ambao ni watumwa wa dhambi, na wamefuata njia isiyofaa. Kingozi wa dini ya Kiislamu ni Mtume Muhammadi (S. A. W). Yeye ndiye Mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu. Alipatiwa *Kur'ani Tukufu* aitumie kawangoza wafuasi wake kuelekea Peponi. Aidha, Wakristo na Wayahudi wameikataa *Kur'ani Tukufu* na Uislamu kwa jumla kwa sababu hawakuzingatia ujumbe wa mitume wao. Kwa mfano, Musa na Isa walihubiri ujumbe

kama ule wa Mtume Muhammadi (S. A. W), na walithibitisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipatiwa ujumbe wa mwisho na Mwenyezi Mungu.

### 4.2.8 Siku ya Kiama

Siku ya Kiama ni siku ya ufufuo. Hii ni siku ya mwisho ulimwenguni huu. Kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, Siku ya Kiama ni siku ambayo waliotenda mema duniani wataingia katika maisha ya furaha Peponi. Waliotenda kinyume cha sheria za dini ya Kiislamu wataingia Jehanamu ambapo watapata adhabu kali. Siku hiyo kutakuwa na daraja jembamba kama unywele ikiwa imepitia juu ya moto. Watu waliotenda wema watapitia juu ya daraja hilo bila adhabu yoyote na waingie Peponi, na watakuwa weupe kama karatasi. Vile vile, watenda dhambi watapitia juu ya daraja hilo, lakini itawachukua miaka mingi kufika Peponi. Watatubu dhambi zao, na mwishowe waingie Peponi. Watafika wakiwa weusi kwa sababu ya kupitia juu ya moto kwa miaka mingi.

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* ameitaja Siku ya Kiama mara kadha katika kazi yake. Kwa mfano katika utangulizi wake anaeleza:

> Na alize thumma na sahaba tuwasalie
> Tunali miradi maongoni mwao tungie.
> Siku ya kiyama wasimame watuombee
> Tupate wokovu siku nzito ya Jahannama (ubeti 2).

Siku ya Kiama Mtume Muhammadi (S. A. W) atakuwa hapo ili awaombee wafuasi wake, wema na wabaya waingie Peponi. Isitoshe, atashuhudia makafiri ambao hawakufuata ujumbe wa mitume wakiingia Jehanamu.

### 4.2.9 Ubinadamu wa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Ubinadamu ni ahali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya binadamu. Jambo hili linadhihirika Mtume anapofika mbele ya Mwenyezi Mungu. Baada ya Mungu kumwambia aombe alichotaka na angepewa kikiwa kamili, Mtume Muhammadi (S. A. W) alianza kumwambia uwezo aliowapa mitume wengine, na akasaili ili ajue nafasi yake ilikuwa gani. Kwa mfano, alimpa Daudi zaburi na Isa uwezo wa kuponya vilema na kuwafufua wafu. Mtume alikuwa hana uhakika kama angepewa uwezo mkubwa zaidi ya mitume wao, na kwa sababu hiyo akawaonea wivu. Mungu Mwenyezi anamhakikishia kuwa yeye ndiye mtume wa mwanzo na wa mwisho. Pia, uwezo wake ni mkubwa kuliko wa mitume wengine.

Mwishowe, Mtume Muhammadi (S. A. W) alipatiwa sala hamsini awapelekee wafuasi wake. Kila muumini alitakikana asali sala hamsini kila siku. Mtume Muhammadi (S. A. W) hakukumbuka kuwa ingekuwa vigumu kwa umati wake kusali sala hamsini kila siku. Aliandamana na malaika Jibrili hadi alipokuwa Musa. Alimweleza Musa kuwa alikuwa amepatiwa sala hamsini awapelekee Waislamu. Musa alimshauri kwa kumwambia:

> ………..umatiwo hawahimili
> Sala hamusini kulla siku zawa thakili;
> Rejea kwa Mola, umuombe yake fadhili,
> Akupunguzie, ni dhaifu wako kauma (ubeti 86).

Mtunzi anaeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alirudi tena kwa Mwenyezi Mungu, ambaye alizipunguza sala hizo kwa tano. Mtume alipofika kwa Musa, alimshauri arejee tena mbele ya Mwenyezi Mungu azipunguze sala hizo zaidi. Tunaelezwa kuwa Mtume alirudi mbele ya Mwenyezi Mungu mara kadha mpaka sala hizo zikapunguzwa hadi tano.

Hata hivyo, kama tulivyosema awali Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu, aliyeteuliwa kuwaongoza wadanamu wote katika njia nzuri

### 4.2.10 Nguzo za Dini ya Kiislamu

Katika *Ukawafi wa Miiraji*, Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza wafuasi wake baadhi ya nguzo za dini ya Kiislamu. Kwa mfano shahada, sala na zakat. Shahada ni nguzo ya kwanza katika dini ya Kiislamu. Hii ndio nguzo muhimu zaidi katika dini hii. Shahada ni ushahidi wa imani na ni kusema, hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu (Allah), na kwamba Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, shahada ni kanuni nyepesi ambayo inapaswa kutamkwa pamoja na kusadiki, ili mtu aweze kuingia katika dini ya Kiislamu.

Katika *Ukawafi wa Miiraji*, Mtume Muhammadi (S. A. W) alinukia harufu nzuri na malaika Jibrili akamwambia kuwa ilikuwa harufu ya mwanamke mzuri. Mwanamke huyu alikuwa amesilimu na alikataa kumwabudu Firauni. Mwanamke huyu aliamini kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu Muumba wa mbingu na nchi. Firauni aliposikia habari hizo kutoka kwa bintiye, alimchukua mwanamke mwema pamoja na watoto wake na kuwatia katika mafuta yachemkayo, na hiyo ilikuwa harufu nzuri ya watu wema.

Sala ni nguzo ya pili katika dini ya Kiislamu. Sala katika dini ya Kiislamu ni mawasiliano ya moja kwa moja kati ya mja na Mwenyezi Mungu. Kulingana na imani ya dini hii, ndani ya sala mtu hujisikia ndani mwake furaha, amani, faraja na kwamba Mwenyezi Mungu yuko radhi naye. Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza wafuasi wake umuhimu wa kusali, na adhabu za wasiosali kwa njia inayofaa. Kama tunavyoelezwa katika *Ukawafi wa Miiraji*, Mtume Muhammadi anasali mara kadha katika safari hii. Kwa mfano, anapompanda Buraki anaanza kusali. Aidha, anasali mara tatu katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi kwa ushauri wa malaika Jibrili. Isitoshe, malaika Jibrili anamchagua Mtume kuwa imamu wa mitume wengine wote katika Beti Mukaddasi. Isitoshe, katika ubeti 18, Mtume Muhammadi (S. A. W) anaonyeshwa watu wakipondaponda vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Malaika Jibrili anamweleza kuwa, hao ni wazembe wa kusali sala za asubuhi, na sala zao hazikamiliki.

Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza wafuasi wa dini ya Kiislamu watilie maanani suala la sala na walichukulie kwa uzito mwingi. Hivyo basi, waislamu husali sala tano kila siku, kama walivyoamrishwa na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume wake. Mtume anawafunza umuhimu wa kusali asubuhi kwa sababu ni wakati mzuri wa kuomba msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu (*Kur'ani Tukufu* 3: 17). Kila sala huchukua muda mfupi tu.

Kama tulivyosema katika ya kwanza, sala katika dini ya Kiislamu hufanyika wakati wa alfajiri, adhuhuri, alasiri, magharibi na jioni. Muislamu anaweza kusali mahali popote. Kwa mfano, ofisini, mashambani. Viwandani au vyuoni. Mtume Muhammadi (S. A. W) anawadhihirishia kwamba sala hizi tano zilitoka kwa Mwenyezi Mungu mwenyewe. Kwa hivyo, wafuasi wake hawana budi kuzitilia maanani.

Aidha, Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza wafuasi wake umuhimu wa kutoa zakat na adhabu ya wasiotimiza nguzo hii ya tatu. Katika ubeti wa 19, mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* anaeleza kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alionyeshwa watu ambao walikuwa wamevalia nguo zenye viraka wakila sumu. Alielezwa kuwa hao ni wale hawatoi zakat na mali yao ni ya Jehanamu. Kulingana na imani ya dini ya Kiislamu, maana ya kutoa zakat ni kutoa asilimia iliyotajwa bayana kutokana na mali fulani, ili kuwapatia makundi fulani ya watu wenye dhiki. Wafuasi wa dini ya Kiislamu huamini kuwa kila mali na kila kitu ni cha Mwenyezi Mungu, na wanavyomliki hutakasika kwa kutenga kiasi kidogo tu kwa ajili ya wenye dhiki katika jamii.

Kwa kutilia mkazo utoaji wa zakat, Matano na EL-Maawy (1984), wanasema kuwa Mwenyezi Mungu aliumba kila kitu na kila kitu ni chake, hata sisi ni wake na sharti tufuate amri zake. Mwenyezi Mungu anataka wale wana mali wawasaidie wale hawana.

### 4.2.11 Wapinzani wa Mtume Muhammadi (S. A. W)

Mtume Muhammadi (S. A. W) anapofika Makka kutoka safari ya mbinguni, alikuwa na hofu kuwa Makureshi hawangeamini habari kuhusu safari ya mbinguni. Abu Jahili, ambaye tumemtaja katika sura ya tatu, kama mmoja wa wapinzani wakuu wa Mtume Muhammadi (S. A. W), alimwona akiwa katika hali ya wasiwasi. Alimsaili kwa dhihaka ili ajue kilichosababisha Mtume awe katika hali hiyo. Mtume Muhammadi (S. A. W) alimweleza bila woga wowote kuhusu safari yake ya mbinguni. Abu Jahili hakuamini aliyoyasikia kutoka kwa Mtume Muhammadi (S. A. W). Aliwakusanya Makureshi wote wasikilize habari hizo. Mtume hakuogopa kamwe, aliwaeleza yote kuhusu safari yake ya mbinguni. Licha ya hayo, katika sura ya tatu, tumeeleza vile Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa tayari kuyahatarisha maisha yake, ili aieneze dini ya Kiislamu.

### 4.2.12 Uwezo Wake Mwenyezi Mungu

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, Mwenyezi Mungu huchukuliwa kama jagina wa majagina. Wafuasi wa dini mbalimbali huamini kuwa uwezo usio wa kawaida wa majagina wao, hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammadi (S. A. W) anawafunza kuwa Mwenyezi Mungu ana uwezo mkubwa sana. Kwa hivyo, Waislamu wanastahili kumpa heshima ya hali ya juu kila wakati. Katika *Ukawafi wa Miiraji* tunaelezwa kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipomwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe, alipiga magoti hadi pale Mungu alimwambia aombe chochote alichotaka na angepewa kikiwa kamili.

Isitoshe, katika *Ukawafi wa Miiraji*, kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, malaika Jibrili alimdhihirishia Mtume Mtume Muhammadi (S. A. W) sifa za Beti Mukaddasi machoni pake. Mtume aliwaelezea Makureshi sifa moja baada ya nyingine. Mtunzi anaeleza kuwa Makureshi hawakuzipinga kwa sababu ulikuwa ukweli mtupu. Aidha, Mwenyezi Mungu anasikia maombi ya Mtume Muhammadi (S. A. W), na kulisimamisha jua ili ahadi ya Mtume itimia. Mungu ana uwezo mkubwa. Jambo linaloonekana kwa binadamu gumu, kwake Mwenyezi Mungu ni rahisi sana. Aidha, kwake Mwenyezi Mungu yote yanawezekana hata yale binadamu anafikiria hayawezekani, Mungu Mwenyezi ana uwezo. Pale muumini anafikiria kuwa hana mbele wala

nyuma anapata tumaini kuwa Mungu anawajili wote, na kuwa yeye ndiye mtetezi wao jinsi alivyomtetea Mtume Muhammadi (S. A. W) mbele ya Makureshi.

### 4.2.13 Umuhimu wa ***Kur'ani Tukufu***

*Kur'ani* ni kitabu kitakatifu cha dini ya Kiislamu. *Kur'ani* hutazamwa na Waislamu kama "neno la Allah". Kulingana na wafuasi wa dini hii, kitabu hiki ni tofauti kabisa na maandiko ya vitabu vya dini zingine, kwa maana wanaamini kuwa kimeandikwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu, kupitia Mtume wake wa mwisho, Muhammadi. Aidha, waislamu huamini kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipatiwa *Kur'ani Tukufu* na malaika Jibrili kwenye pango la mlima Hira.

Mtume Muhammadi (S. A. W) na malaika Jibrili wakiwa katika safari ya kutoka Makka hadi Beti Mukaddasi, waliliona jini likiwa na kijinga cha moto, huku likimmulika Mtume Muhammadi (S. A. W). Malaika Jibrili alimshauri asome aya kutoka kwa *Kurani Tukufu*. Mtume alipofuata ushauri wa malaika Jibrili, jini lilizima. Maneno "jini likazima" yanatufanya tuamini kuwa jini lenyewe lilikuwa ni moto. Wafuasi wa Mtume Muhammadi (S. A. W) wanaamini kuwa aya ambayo Mtume alikariri, kutoka kwa *Kur'ani Tukufu*, hukinga makao yao kutokana na moto wa aina yote. Njia ya kuelekea Peponi ina vikwazo vingi kwa wafuasi wa Mtume Muhammadi (S. A. W) lakini wakizingatia mafunzo katika *Kur'ani Tukufu* watashinda.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) yanayodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Mafunzo hayo yanahusu maisha ya muumini wa dini ya Kiislamu. Mafunzo hayo ni kama vile, kutukuzwa kwa Mtume Muhammadi (S. A. W) alipomuona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Utukufu wa Mtume Muhammadi (S. A. W) baada ya kupasuliwa kifua na kutolewa nyongo zote. Mtume Muhammadi (S. A. W) ana nafasi kubwa miongoni mwa mitume wengine kwa sababu aliwaongoza katika sala. Aidha, nafasi yake ni kubwa kuliko ya malaika wa Mwenyezi Mungu. Miji mitakatifu katika dini ya Kiislamu ni Makka, Madina na Yerusalemu. Isitoshe, dini ya Kiislamu ni tofauti na dini zingine ulimwenguni. Fauka ya hayo, Siku ya Kiama Mtume Muhammdi (S. A. W) atasimama awaombee wafuasi wake. Siku hiyo kuna wale wataingia Peponi, na wengine wataingia Jehanamu. Mtume Muhammadi (S. A. W) alikuwa na wapinzani wengi kama vile Abu Jahili, lakini uwezo wake Mwenyezi Mungu ulimwezesha kuwashinda wapinzani wake kila wakati.

## SURA YA TANO

## TATHMINI NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo hitimisho la utafiti wetu. Tumeyatathmini madhumuni yetu ya utafiti huu. Ikiwa tumefaulu kuyatosheleza au la. Pia, tumezitathmini nadharia tete zetu. Mwishowe, tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu utenzi wa *Ukawafi wa Miiraji*.

### 5.2 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti wetu, tumehakiki usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji* na mafunzo yake kwa wafuasi wake. Nadharia tuliyoitumia katika utafiti huu ni ya uamilifu. Nadharia hii ilifaa sana katika uhakiki wetu kwa kuwa imethibitisha kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) ni jagina wa dini ya Kiislamu ambaye ana umuhimu wa kipekee kwa wafuasi wake. Ujagina ni asasi muhimu sana katika mfumo mzima wa jamii. Asasi hii huzuliwa na mahitaji fulani ya kijamii katika kipindi mahsusi katika historia ya jamii husika. Ujagina wa Mtume Muhammadi (S. A. W) unadhihirika katika safari yake mbinguni. Anamwona Mwenyezi Mungu kwa macho yake mwenyewe. Mwishowe, Mtume anapewa sala tano awapelekee wafuasi wake.

Tulikuwa na malengo matatu ya utafiti wetu. Lengo la kwanza ni kuchunguza usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W) katika *Ukawafi wa Miiraji*. Katika sura ya pili, tumegundua kuwa mtunzi wa utenzi huu amemsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama Mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu, mcha Mungu, mwenye akili pevu, hana dhambi, ni kiongozi wa dini ya Kiislamu, ni mwombezi, ni mvumilivu miongoni mwa sifa zingine za Mtume Muhammadi (S. A. W) zinazojitokeza katika utenzi huu. Mtume Muhammadi (S. A. W) ana uwezo mkubwa, hata wa kutenda miujiza. Uwezo huu unatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Lengo letu la pili lilikuwa kuangalia sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Tulieleza katika sura ya tatu kuwa, si sifa zote za ujagina zinadhihirika katika utenzi huu kwa sababu haujikiti katika maisha yote ya Mtume Muhammadi (S. A. W). Lakini tumevitumia vitabu vya dini pamoja na utenzi wa *Ukawafi wa Miiraji* kutoa mifano mwafaka ya sifa za ujagina ambazo tumeziangalia katika sura ya tatu.

Sifa za ujagina ambazo tumezishughulikia ni kama vile; kuzuka kwa jagina, jagina hutokana na ukoo au familia bora, kugura kwa jagina, safari ya ajabu katika ulimwengu mwingine, wapinzani wa jagina na maisha ya jagina huwa ya dhiki tupu. Aidha, tumeshughulikia kuwa, kuna matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraji*. Baadhi ya matukio haya ni pamoja na Mtume Muhammadi (S. A. W) kupasuliwa kifua na malaika Jibrili na kutolewa maovu yote yaliyokuwa ndani yake. Halafu akashonwa kama kwamba hakupasuliwa, kuvumilia kuona hatima ya watenda maovu kama vile waongo wakikatwa ndimi zao kwa makasi huku zikirejea tena, kulizima zini, kuwa imamu katika Beti Mukaddasi, na kumwona na kuzungumza na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, tumefaulu kudhibitisha lengo letu la pili.

Lengo letu la tatu lilikuwa kueleza na kubainisha mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake kama yanavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Katika uchunguzi wetu (sura ya nne) tumegundua kuwa Mtume Muhammadi (S. A. W) anafunza wafuasi wake masuala muhimu katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, Mtume Muhammadi (S. A. W) ni mtukufu kwa kuwa alitakaswa kwa kupasuliwa kifua na kutolewa maovu yote, kuna adhabu za watenda maovu, miji mitakatifu katika dini ya Kiislamu ni Makka, Madina na Yerusalemu. Siku ya Kiama watenda mema wataingia Peponi ilhali watenda maovu wataingia Jehanamu. Kuna tofauti kati ya dini ya Kiislamu na dini zingine, na Mtume Muhammadi (S. A. W) ana nafasi kubwa miongoni mwa mitume wengine.

### 5.3 Kuhusu Nadharia Tete

Nadharia tete yetu ya kwanza ilikuwa, mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* amefaulu katika kumsawiri Mtume Muhammadi (S. A. W) kama jagina katika dini ya Kiislamu. Matendo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) katika utenzi huu yanadhihirisha kuwa yeye ni jagina katika dini ya Kiislamu. Mambo ambayo anatenda (kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu) hayawezi kutendwa na binadamu wa kawaida. Matendo hayo huajabiwa na wafuasi wake. Kwa sababu hiyo, wao hujaribu juu chini kuiga matendo hayo ya kiongozi wao. Mtume Muhammadi (S. A. W) alisafiri hadi mbinguni, na mwishowe anakutana na kuzungumza na Mwenyezi Mungu ambaye anampa sala tano awapelekee wafuasi wake. Matukio hayo yote yanatendeka katika usiku mmoja. Safari hii ni ya kimuujiza.

Nadharia tete yetu ya pili ilikuwa, kuna sifa za ujagina na matukio ya ujagina katika *Ukawafi wa Miiraj*i. Tumeweza kuthibitisha ukweli wa nadharia tete hii katika sura ya tatu. Katika sura hii tumechanganua sifa za ujagina kama vile kuzuka kwa jagina, wapinzani wa jagina, jagina huwa na akili pevu na jagina huwa kipenzi cha jamii. Baadhi ya sifa za ujagina zinadhihirika katika utenzi huu. Kwa mfano, kupevuka kwa akili ya jagina na safari ya jagina katika ulimmwengu mwingine na anaporejea huwaletea wanajamii zawadi. Kwa mfano, Mtume Muhammadi (S. A. W) aliwaletea wafuasi wake sala tano. Vilevile, kuna mtukio ya ujagina katika utenzi huu ambayo yamemzingira Mtume Muhammadi (S. A. W). Kwa mfano, uchaguzi wa dini ya Kiiislamu, kulizima jini na kuwaelezea Makureshi kuhusu safari yake mbinguni.

Nadharia tete yetu ya tatu ni kuwa, Mtume Muhammadi (S. A. W) ana mafunzo kadha kwa wafuasi wake yanavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji*. Tumethibitisha ukweli wa nadharia tete hii katika sura ya nne ambamo tumechunguza mafunzo ya Mtume Muhammadi (S. A. W) kwa wafuasi wake katika *Ukawafi wa Miiraji.*

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti Huu**

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, kazi ambayo imefanyiwa utenzi huu ni kuhaririwa na kutafsiriwa. Jambo hili linadhihirisha kuwa kuna pengo kubwa la kiusomi ambalo linastahili kujazwa. Katika utenzi huu, tumeshughulikia usawiri wa Mtume Muhammadi (S. A. W), na mafunzo yake kwa wafuasi wake kwa kutumia nadharia ya uamilifu. Hatukuweza kushughulikia masuala mengine kwa sababu ya wakati. Tunapendekeza kuwa watafiti wengine washughulikie utenzi huu kwa kuchunguza kipengele cha fani, kama vile usimulizi na mandhari wakitumia nadharia tofauti.

## MAREJELEO


Abrams, M. H (1993*). A Glossary of Literary Terms.* 6th Edition. New York: Hartcourt & Brace.

Allen, J. T (1971). *Tendi*. Nairobi. Heinemann Books Ltd.

Achieng, O.B (1975). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao katika Jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere".Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Biblia (1997). *Agano la kale na Agano jipya*. Tanzania. Bible Society of Tanzania.

Campell, J (1949). *The Hero with Thousand Faces*. Novato. New World Library.

Carlyle, T (1924). *On Heroes, Hero-Worship and Heroic in History*. London. Macmillan & Co Ltd.

El-Geyoushi, I. M (1985). *Teachings of Islam*. London. The Islamic Cultural Centre.

Gatakaa, G (2013). "Uhakiki wa Maudhui Teule katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*". Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Gathara, F.K (2015). "Taswira ya Jagina katika Tendi; Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa". Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Gichamba, J. M (2005). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao kwa Jamii: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu".Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Hakeem, F. R (1956). *Maisha ya Mtume Muhammad* S. A. W. Dar es Salaam. Ahmadiyya Printing Press.

Innayal, M (1982). *The Authenticted Miracles of Mohammad*. New Delhi. Award Publishing House.

Kadiri, D. A (1986). *Hadithi za Mtume* S. A W. Nairobi. Acme Press Ltd.

Khuri, P. H (1968). *The History of Arabs from Earliest Times to the Present*. London. Macmillan.

Kimani N. / Rocha C.(2008). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Knappert, J (1966*). Miiraji: The Swahili Legend of Mohammed's Ascension*, Swahili Vol. 36/2 pp. 105-156.

Knappert, J (1967). *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of East* African *Islam as reflected in the Utenzi Literature*. Leiden. E. J. Brill.

Knappert, J (1971a). *Swahili Islamic Poetry Vol.1: Introduction to Celebration of Mohammed's Birthday: Swahili Islamic Cosmology*. Leiden. E. J. Brill.

Knappert, J (1971b*). Swahili Islamic Poetry Vol. 11: Mi'raj and Maulid*. Leiden. E. J. Brill.

Kunene, M (1979). *Emperor Shaka The Great*: A Zulu Epic. London. Heinemann.

Matano, S. M / EL-Maawy, A.A (1984). *Islamic Religious Education*. Book 5. Nairobi. Typesetters (K) Ltd.

Mbunda, M (1993). *Kamusi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers Limited.

McGee, J.R na Warms, R.L (2000). *Anthropological Theory: An Introductory History*. Boston. McGraw Hill

Mulokozi, M. M (1999). *Tenzi tatu za kale*. Dar es Salaam. TUKI.

Muniu, G. G (2013). "Ujagina wa mwanamke katika Pango". Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Ndumbaro, E (2013). "Shujaa wa Tendi na Matatizo ya Kijamii". Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Owallah, K (2011): "Uhakiki wa Maudhui Teule katika *Utenzi wa Nabii Isa"*.Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Okombo, P. L (2011). “Sitiari, Taashira na Tashibiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*: Uhakiki wa Kimtindo”. Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Qur’an (1999). *The Noble Qur’an; Interpretation of meaningsof the Noble Qur’an in the English Language*. India. Dar-us-Salam Publications.

Reglan, L (1936). *The Hero. A study in Traditional Myth and Drama*. Dover Publication Edition.

Safeyy, R. M (2002*). The Pure Nectar A Treatise on Prophet Muhammad’s Biograph*y. India. Dar-us-Salam Publications.

Siddiqui, A. M (1954). *Elementary Teachings of Islam*. Karachi. Taj Company Ltd.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Oxford University Press.

Wa Mutiso, K (1985). “Hurafa na Uyakinifu Katika *Hamziyyah*”.Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Wa Mutiso, K (1999). “Sira ya majagina: Budha na Muhammadi.” (Makala hayajachapishwa).

Wa Mberia (1989). “Fumo Liyongo”. Mulika Na.21 uk 25-43.

Wafula, R.M / Njogu (2007). *Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W (2003a*). Kichocheo cha Fasihi*.Nairobi. Focus Publication.

Wamitila, K. W (2003b). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications

Wamitila, K. W (2008). *Kanzi ya Fasihi-Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers Limited.

Were, G. S (I974*). A History of South African*. London. Evans Brothers.

TUKI (2005). TUKI: *English-Swahili Dictionary.3rd Edition*. Dar es Salaam. TUKI.

Toyoaki, U (1975). *Muhammed: The Hero of the Islamic Cons-ciousness*. TJR NO. 12. Tenri. University Press.

Vutugwa, F. L (2013). "Sifa za Kiuhalisiajabu na Umuhimu wake katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*". Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.